

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 30 Machi, 2021**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA  
AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Kwaya ya Bunge iliimba Wimbo wa Taifa na Wimbo  
wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitaleta kwenu Taarifa ya Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai.

Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo wote tunafahamu aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alifariki dunia tarehe 17 Machi, 2021 katika Hospitali ya Mzena, Jijini Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia msiba huo wananchi wa Tanzania walipata fursa ya kutoa heshima za mwisho kama ifuatavyo; tarehe 20 hadi 21 Machi, 2021 Mkoani Dar es Salaam, tarehe 22 Machi, 2021 Mkoani Dodoma ambapo pia ilifanyika hafla ya kitaifa. Tarehe 23 Machi, 2021 ilikuwa Zanzibar na tarehe 24 Machi, 2021 ilikuwa mkoani Mwanza.

Waheshimiwa Wabunge, nazisikia kelele sina hakika kama wote tuko pamoja kwenye jambo hili zito lillolipata Taifa letu. Tarehe 25 hadi 26 mkoani Geita na Chato.

Waheshimiwa Wabunge, mazishi ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yalifanyika siku ya Ijumaa tarehe 26 Machi, 2021 nyumbani kwake Chato, Mkoani Geita.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa leo ni siku ya kwanza kwa Bunge hili kukutana tangu ulipotokea msiba huo naomba Waheshimiwa Wabunge tusimame kwa dakika moja ili kumkumbuka mpendwa wetu.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumkumbuka aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli)*

**NAIBU SPIKA:** Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina la Bwana lihimidiwe.

Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:**

Azimio la Bunge la kuutambua na kuenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utumishi wake uliotukuka.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:**

Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

#### **Ukamilishiji wa Ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Magu kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali imeendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri 100 ikiwemo Halmashauri ya

Wilaya ya Magu ambazo kwa ujumla zimegharimu kiasi cha shilingi bilioni 147.33.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Magu ambalo litagharimu shilingi bilioni tano hadi kukamilika. Hadi mwezi Februari 2021, Serikali ilikuwa imekwishatoa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo ambalo tayari limeezekwa. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 750 kwa ajili ya kuendelea na hatua ya ukamilishaji wa jengo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura Kiswaga swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Kwa kuwa bajeti inayoendelea sasa tuko robo ya tatu na Serikali ilitenga shilingi milioni 750, ni lini Serikali itazileta hizi fedha za bajeti ya mwaka huu unaoendelea ili tuweze kuendelea na ujenzi wa jengo hilo la Halmashauri? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa jengo hili ni la muda mrefu na Serikali imewekeza fedha nyingi za kutosha na ili ufanisi wa shughuli za Halmashauri uweze kwenda vizuri, je, mwaka huu wa fedha Serikali itatenga fedha za utoshelevu ili kuhakikisha kwamba jengo hili linakamilika na majengo mengine ambayo yako kwenye nchi hii? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetangulia kujibu kwenye swali la msingi kwamba Serikali kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021 imekwishatenga shilingi milioni 750 kwa ajili ya kufanya shughuli za umaliziaji wa jengo la utawala katika Halmashauri ya Magu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Magu kwamba fedha hizo ziko katika hatua za mwisho za kutolewa ili ziweze kufikishwa katika Halmashauri hiyo kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo zilizokadiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na jengo hili kuwa la muda mrefu ni kweli na Serikali inatambua kwamba jengo hili lina muda mrefu tangu limeanza kujengwa, na dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba linakamilika mapema iwezekanavyo na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha Serikali itatenga kiasi cha shilingi bilioni moja na milioni mia moja kwa ajili ya jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Magu. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatenga fedha hizo na zitafikishwa ili ziweze kukamilisha jengo hilo kwa ajili ya kuboresha huduma kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nape Moses Nnauye swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mtama tulipokabidhiwa Halmashauri hii na Mheshimiwa Rais alituahidi kwamba ujenzi wa mjengo yake utaanza mapema na hivi karibuni Waziri Mkuu alifanya ziara Jimboni Mtama na kutuahidi kwamba hizi fedha za ujenzi zitakuja.

Sasa je, Serikali iko tayari kuanza kuleta hizi fedha hata kama ni kwa awamu ili ujenzi huu na ahadi ya Mheshimiwa Rais ianze kutekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imedhamiria kuhakikisha inakamilisha au inaanza ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri zile mpya ambazo miongoni mwao ni Halmashauri hii ya Mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi bilioni 80.42 zimetengwa na zitaanza kutolewa wakati wowote kuanzia sasa na taratibu zinaendelea ili zile Halmashauri ambazo kwanza zilipata fedha za kuanza ujenzi zipate fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo lakini zile ambazo zinahitaji kuanza ujenzi ziweze kupata fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili katika mwaka wa fedha ujao pia Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha shughuli hizo za ujenzi wa majengo ya utawala zinakamilika. Kwa hivyo, naomba nimhakikishie Mbunge wa Mtama, Mheshimiwa Nape kwamba Serikali inatambua uhitaji wa kuanza ujenzi wa jengo la utawala katika Halmashauri ya Nape hiyo ya Mtama na tutahakikisha fedha zinatengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Kuongezeka kwa Vitendo vya Ubakaji na Udhaliishaji wa Watoto Nchini**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusiana na ongezeko la vitendo vya ubakaji na udhallishaji wa watoto nchini?

(b) Je, kwa nini Serikali haifanyi tafiti kujua sababu za kesi nyingi kushindwa kuwatia hatiani wabakaji na kuja na mpango mpya wa kudhibiti vitendo hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum yote mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa Serikali kuwalinda wananchi wakiwemo watoto dhidi ya makosa ya ubakaji na udhallishaji. Ili kupambana na vitendo hivi Serikali imekuwa ikichukua hatua kali ikiwemo kifungo cha miaka 30 jela kwa wanaojihusisha au kusaidia kufanyika kwa vitendo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti nyingi zimefanywa na asasi mbalimbali za Serikali na zisizokuwa za Kiserikali na zimebaini kwamba kuna sababu mbalimbali ambazo zinasababisha. Sababu hizi zikiwemo sababu za muhali lakini pia kuna sababu za kumalizana nje ya Mahakam ana wahanga kuchelewa kuripoti vituo vya polisi. Kwa kipindi cha mwaka 2020 jumla ya washtakiwa 1,183 walihukumiwa vifungo jela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako tukufu naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kutoyafumbia macho matukio ya udhallishaji na ubakaji ikiwemo kutoa taarifa kwa vyombo vya dola vinavyohusika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Najma Murtaza Giga swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza niipongeze Serikali kwa jitihada inazochukua katika kupiga vita ukatili wa watoto kwa suala la ubakaji. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza litalenga kwenye majibu ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na tafiti ambyao amefanya na kututaka sisi sasa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla kuweza kusaidia katika kutatua changamoto hizi.

Swali langu liko kwamba, je, ninyi kama Serikali mmejipangaje kuhakikisha kwamba vitengo vyote vinavyoshughulikia masuala ya sheria na kutoa haki vinashirikiana kikamilifu ili kuweza kutokomeza masuala haya ambayo mmeyatafiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusiana na Sheria Namba 21 ya Mtoto ya mwaka 2009. Sheria hii imeweka wajibu na jukumu la wazazi ama walezi kuweza kuwalinda watoto dhidi ya ukatili ikiwemo hili la ubakaji.

Je, mmekwama wapi katika kutekeleza sheria hii kiasi kwamba tunaona hakuna mzazi au mlezi anayeweza kuchukuliwa hatua pale ambapo mtoto anapatikana na makosa haya tukizingatia ndoa zinavunjika kwa wingi na watoto wanatelekezwa na inasababisha kufanyiwa vitendo hivyo vya ukatili, lakini pia wale wazazi ambao wanabaki, akina baba wanaweza kufanya vitendo hivyo vya ukatili kwa watoto wao wenyewe. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na hilo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.



**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mbunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza lilikuwa linasema kwamba, je, Serikali ina mpango gani au je, kuna jitihada gani nyingine ambazo zimechukuliwa na Serikali, ili kuhakikisha kwamba, tunatokomeza vitendo hivi. Kama Serikali tumechukua jitihada nyingi na tumechukua jitihada mbalimbali, lakini bado tunaendelea kuchukua jitihada ya kwanza ikiwemo ya kuendeleza kutoa elimu kwa jamii kwa sababu, tunaamini jamii ikipata elimu ya kutosha kwenye masuala haya maana yake masuala haya yanapungua au yatamalizika moja kwa moja. kwa hiyo, kama Serikali tumeanza kutoa taaluma kwanza kupitia kwenye madawati ya kijinsia ambayo mara nyingi yapo katika Jeshi la Polisi, tunayatumia yale kutoa taaluma hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine tunao hawa *para legals*, wasaidizi wetu wa sheria ambao wako huko, wanatusaidia kuipa jamii taaluma. Pia tunavitumia vyombo vya habari kuhakikisha kwamba, taaluma inafika kwa jamii, lakini kizuri zaidi tunaenda kutengeneza mazingira ya kuipa nguvu sheria hii Namba 21 ya mwaka 2009 ili kuhakikisha kwamba, sheria inafuatwa na wananchi kwa kiasi kikubwa jamii inapungukiwa na matendo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine la pili ameuliza kwamba, sheria hii inakwama wapi? Naomba pia kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kwamba, wakati tunaipitia sheria hii tumegundua kwamba, sheria hii ipo kimadai zaidi *rather than* kijinai. Sasa ukitazama unakuta kwamba, watu wanaweza wakafanya vitendo hivi wakitegemea kwamba, wao watafunguliwa kesi zaidi za madai na kwa sababu, madai si analipa. Kwa hiyo, sasa unakuta haiko kijinai zaidi. Kwa hiyo, unakuta sheria ndio maana unafika wakati utendaji wake wa kazi unakuwa haupo vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni ugumu wa wananchi kwenda kutoa ushahidi, ugumu wa mashahidi.

Ukimchukua mtu akitoa ushahidi huko nyumbani ukikaa naye atatoa ushahidi vizuri tu, tena atatoa ushahidi maana yake ambao uko *evident*, lakini kesho twende mahakamani ndio inakuwa ngumu. Sasa na mahakama nayo ikiwa siku mbili, tatu, mara nne tano umeitwa hujaenda kutoa ushahidi maana yake mahakama inatoa uamuzi kwa upande mmoja. Kwa hiyo, upo ugumu kwenye utoaji wa ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kine sasa wanafamilia, wanamalizana tu kienyeji. Jambo limetokea kwa sababu, baba mkubwa, baba mdogo wanamalizana huko mwisho wa siku huku sheria inakuwa haipewi nguvu. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la ubakaji katika Mkoa wetu wa lringa limekithiri sana; na kwa kuwa, tunaona kwamba, wanaobaka mara nyingi wamekuwa wakiweka Mawakili tena wasomi kwa ajili ya kutetea hizo kesi, matokeo yake wanashinda; na wale wanaobakwa kwa sababu, hawana uwezo walio wengi tumeona mara nyingi hata kesi zikienda wanashindwa. Je, Serikali inasaidiaje kuhakikisha wale watu wanapata haki zao, na hasa watoto wetu wanaobakwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu maswali ya kwanza kwa ufasaha sana. Jambo kubwa ambalo Serikali tumeendelea kusisitiza ni watu wetu kutokuyamaliza haya masuala kwa namna ya kindugu ama kirafiki na kuficha ushahidi, lakini kwa kile kipengele alichosema kwa wale watu ambao hawana uwezo wa kutafuta Mawakili tumetengeneza ule utaratibu wa msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuko kwenye hatua za mwisho za kuzungumza kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ili kuweza kuanza kuwatumia Wanasheria popote pale walipo hapa nchini, wale walioko chini ya halmashauri, wale walioko chini ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, waweze kuwasaidia wananchi wale wasioweza kupata Mawakili kuwapatia msaada wa kisheria kama ambavyo viongozi wetu wakuu wamekuwa wakionesha mfano punde wanapofika katika eneo ambako kuna wananchi wana kilio, wamekuwa wakiingilia kati kuweza kuwasaidia, ili waweze kupata msaada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshajaribisha sehemu mojawapo tulipokuwa na suala moja la mwananchi mmoja ambaye hakuweza kupata suala la wakili, lakini pia hakuweza kujua masuala ya kisheria, kuweza kusaidiwa na Wanasheria waliopo Ofisi za Mkuu wa Wilaya ama Ofisi za Mkurugenzi kwa maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye Wanasheria wote Mawakili wako chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la muuliza swali ni la msingi kwa sababu kwa wakati mwingine hata mwananchi akiwa na Wakili kumekuwa na utaratibu wakati mwingine Mawakili wanazungukwa na wale watenda maovu, *I mean* wale Wanasheria, kama mlalamikaji hana fedha wanaweza wakazungukwa na wale wenye fedha ikatokea wakashindwa kupata haki yao. Kwa hiyo, tutakapokamilisha hili, tangazo rasmi litatoka ili wananchi waweze kupata haki zao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Haji, swali la nyongeza.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Zanzibar imekuwa ni muathirika mkubwa wa matukio haya ya kudhalilisha watoto. Mheshimiwa mwaka uliopita ilizuka kesi maarufu ya mlawiti maarufu anayejulikana kwa jina la Kiringo. Hii kesi ilianza kwa kishindo na ushahidi wake ulikuwa unaonekana

wazi, lakini leo kesi hii inaonekana imezima. Nataka kujua hatima ya kesi ya Kiringo imefikia wapi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Sasa Mheshimiwa Khatib Haji swali lako ni mahususi kwa kesi Fulani na kwa sababu, ni swali la nyongeza, Naibu Waziri anaweza kuwa hana hiyo kesi hapo. Kwa hiyo, kwa kuwa umempa na kwa mujibu wa taratibu zetu, nitampa nafasi ya kujibu atakapokuwa tayari na majibu ya swali hilo.

Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri na mikakati mingi ambayo wameweka kuhakikisha tunapambana na hali hii, bado kuna mianya mingi hasa kwenye sheria yetu ambayo inaenda kuchochea hii changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nitoe mfano, kuna binti lringa wa miaka 13, alibakwa na kijana wa miaka 18, akakiri kuwa amembaka binti huyu na adhabu yake ilikuwa ni viboko na akaachiwa. Huyu kijana anaruhusiwa kupiga kura, lakini sheria inapokuja kwenye kumbaka mtoto inamlinda kuwa bado ni *minor*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na mikakati hiyo inabidi waangalie upungufu mkubwa wa kisheria ambao unakwenda kuchochea changamoto hii ya watoto kubakwa na kulawitiwa katika mikoa yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, huo ulikuwa ni ushauri. Naona Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria anataka kuupokea huo ushauri, aangalie upungufu wa ile sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea na tuko kwenye hatua tunaziangalia hizo sheria, Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mtoto pamoja na Sheria za Mirathi ambazo kimsingi ni sheria zinazogusa jamii moja kwa moja ili tuone pale ambapo patakuwa na upungufu tuweze

kurekebisha, ili kuweza kulinda jamii yetu na ustawi wa jamii wa nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita, sasa aulize swali lake.

Na. 3

### **Athari za Michezo ya Kubahatisha – Maeneo ya Vijijini**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya michezo ya kubahatisha maarufu kama bonanza kulipiwa kodi ya shilingi laki moja tu kwa mwezi na kutolipa *Service Levy* kwa Halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ya kubahatisha hapa nchini inasimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania kupitia Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura Namba 41 ya mwaka 2003. Sheria hii inatambua kuainisha michezo mbalimbali ya kubahatisha ikiwemo michezo ya *slot machines* na imeainisha kodi na tozo iliyopaswa kulipwa kwa kuzingatia aina ya mchezo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya michezo ya *slot machine*, maarufu kwa jina la bonanza, inalipiwa *service levy* ya asilimia 0.03 ya mapato ya mwaka yanayotokana na michezo hiyo. Tozo hiyo hukusanywa na mamlaka ya Serikali

za mitaa. Hivyo basi michezo ya *slot machine* inalipiwa *service levy* kwa mujibu wa sheria iliyopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa sheria inawaruhusu wachezeshwa bonanza kulipa asilimia 0.03 ya mapato yao, nataka kumuuliza Waziri, je, ni nani anayejumlisha mapato yao kwa mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Wachina hawa wanaochezeshwa mabonanza wanarundika pesa zao nyumbani wala hawapeleki benki. Mfano mzuri ilitokea Morogoro, ulipofanyika msako Morogoro walikutwa na bilioni 2.5, ukafanyika msako Arusha wakakutwa na bilioni 5.0 ndani. Sasa sisi kama Halmashauri kupata ile asilimia tunayoitaka kwenye *levy* tunaipataje? Je, Serikali wako tayari kuruhusu kwamba, kule Halmashauri tuweke makufuli pamoja pale kwenye zile *slot machine*, ili wanapoenda kufungua watendaji wetu tujumuike nao ili tuweze kupata hesabu vizuri kwa ajili ya kukusanya hiyo *service levy*? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Musukuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi wanaohusika na ukusanyaji wa mapato ya *service levy* ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa wenyewe kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, naomba kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Musukuma kwamba, anajali na anajali Serikali kwa kuangalia uchumi

wa nchi unavyokwenda. Hata hivyo, Mheshimiwa Musukuma ushauri wake tumeuchukua na tutaufanyia kazi kwa mujibu wa sheria kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama ilivyo sheria. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maji. Mheshimiwa Agnesta Lambart Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 4

### **Hitaji la Maji Safi na Salama – Wilaya ya Butiama**

**MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji safi na salama Butiama ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wa Baba wa Taifa katika Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambart Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa maji safi na salama katika Wilaya ya Butiama ni 61.18%. Katika kuhakikisha wananchi wa Butiama wanapata huduma ya maji safi Serikali kupitia *RUWASA* imekamilisha miradi ya maji katika Vijiji vya Nyabanje, Magunga, Kongoto, Bukwaba, Kamgendi na Masurura, vinavyohudumia wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la kutatua tatizo la maji katika muda mrefu Butiama, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa Mugango – Kiabakari – Butiama mwezi Disemba, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi

Disemba, 2022. Kazi zilizoanza kutekelezwa ni upimaji wa maeneo ya ujenzi wa matenki, mtambo wa kusafisha maji, njia kuu ya bomba na uletaji wa vifaa katika eneo la mradi. Mradi huu unatarajiwa kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji kwa asilimia 100 katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyoko ndani ya kilometa 12 kutoka bomba kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo utatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development – SFD*) kwa gharama ya dola za Marekani milioni 30.69 sawa na takribani shilingi bilioni 70.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnesta Lambart Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa ajili ya nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri kwamba, hayaleti matumaini ya moja kwa moja kwa wakazi wa Butiama naomba nijielekeze kwenye maswali kama ifuatavyo; Swali la kwanza; kwa kuwa, miradi hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja hapa utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua sana kwa lugha nyingine umekuwa na mwendo wa kinyonga. Je, nini kauli ya Serikali basi kuhusiana na bili zinazotolewa kwa wakazi wa Butiama bila kupatiwa huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kumtua mwanamke ndoo kichwani. Swali langu ni kwamba, ni lini basi Serikali itatekeleza kauli mbiu hii kwa matendo kukamilisha miradi yote ya Serikali nchi nzima ambayo imeonekana kusuasua mpaka sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.



**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na masuala ya *bills*, maeneo mengi yalikuwa na tatizo hili, lakini tayari Wizara tunashughulikia kwa karibu kuona kwamba, mtu anakwenda kulipa bili kulingana na matumizi yake. Tunaendelea kuweka mbinu mbalimbali kama kumhusisha moja kwa moja mtumiaji maji kwa kushirikiana na msomaji mita wataangalia kwa Pamoja, watasaini kadi na hapo sasa yule mlipaji atakwenda kulipa bili kulingana na matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kumtua mwanamke ndoo kichwani; hili suala sasa hivi ni tayari linatekelezeka. Maeneo mengi ya Tanzania sasa hivi akinamama wameshakiri hawabebi tena maji vichwani na tayari Wizara tunaendelea kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha maeneo yote ya pembezoni mwa miji kwa maana ya vijijini nao wanakwenda kukamilika katika mpango huu na kazi zinaendelea. Tayari tuna ari kubwa sana kama Wizara na watendaji wetu wametuelewa mwendo wetu ni mwendo wa kasi ya mwanga. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenan, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. changamoto za maji ambazo wanakumbana nazo wananchi wa Butiama zinafanana sana na changamoto zinazowakuta wananchi wa Wilaya ya Nkasi. Natambua kwamba, Serikali imekuwa inapeleka fedha katika miradi mbalimbali katika Wilaya ya Nkasi ambayo haijaweza kumaliza changamoto za maji. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika ambacho ni chanzo cha uhakika ili kuweza kumaliza changamoto za maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji tayari tuna mikakati kabambe ya kuweza kutumia mito, maziwa na vyanzo vyote vya maji pamoja na Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, kufikia mwaka ujao wa fedha Serikali tunaendelea kuona namna bora ya kuweza kutumia Ziwa Tanganyika kutatua tatizo la maji eneo la Nkasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. pamoja na majibu mazuri na maelezo mazuri ni ukweli usiopingika kwamba, tatizo la maji katika nchi yetu ni tatizo kubwa na kama ambavyo Mheshimiwa Aida amesema kuhusiana na matumizi ya Ziwa Tanganyika. Je, sio wakati sahihi kwa Serikali kuhakikisha kwamba, Mkoa wote wa Rukwa, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Songwe unaanza kutumia chanzo cha uhakika cha Ziwa Tanganyika, ili kupata maji maeneo yote? Kwani imethibitika kabisa matumizi ya maji kutoka Ziwa Victoria yamekuwa ni ufumbuzi mkubwa katika maeneo mengi, sasa si wakati muafaka kwa hiyo mikoa niliyoitaja kutumia chanzo hicho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu awali, tayari Wizara tuna mikakati ya kuona maziwa yote ambayo yanapatikana katika nchi yetu tunakwenda kuyatumia kikamilifu katika kutatua tatizo kubwa la maji katika mikoa inayohusika. Hivyo mikoa yote ambayo inapitiwa na ziwa hili tutakwenda kuifanyia kazi na hakuna mkoa utakaorukwa,

tutagawa maji kulingana na bomba litakavyopita kadiri mradi utakavyosanifiwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taja jina lako.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Naitwa Eng. Samweli Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la maji lililopo Butiama lipo pia kwenye Mji wa Katesh kwenye Jimbo langu; na kwa kuwa Serikali imeshawekeza shilingi bilioni 2.5 kuleta maji mjini na maji yale sasa yapo tayari kutumika. Je, Wizara iko tayari kuongeza fedha kidogo ili maji yaweze kusambazwa kwa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hili.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza fedha katika miradi ambayo ipo katika hatua za utekelezaji ni jukumu la Wizara. Hivyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge fedha zitakuja kwa awamu kama ambavyo imekuwa kawaida yetu kuhakikisha mradi huu unafikia lengo la kupata maji bombani. Lengo la Wizara siyo tu kujenga hizo *structures* ambazo zipo tayari, tutaleta fedha kuhakikisha maji sasa yanafika bombani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 5

### **Mradi wa Kuhifadhi Mazingira Mufindi**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta Mradi wa Kuhifadhi Mazingira Mufindi katika chanzo cha maji cha Mto Ruaha na shamba la miti la Sao Hill?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa maji nchini. Chanzo cha maji cha mto Ruaha Mdogo ni miongoni mwa mito inayomwaga maji nchini katika kidakio cha *Great* Ruaha. Kutokana na umuhimu wa Mto Ruaha Mdogo na kwa lengo la kuhakikisha mto huo unatiririsha maji kwa muda wote, Wizara kupitia Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Rufiji tayari imekamilisha kuweka mipaka ya vyanzo vya maji na taratibu za kuvitangaza katika Gazeti la Serikali zinaendelea. Hii ni pamoja na uanzishwaji wa Jumuiya ya Watumia Maji, utunzaji wa vyanzo vya maji, upandaji wa miti rafiki na maji pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uhifadhi vyanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa shamba la miti la Sao Hill lililopo Wilaya ya Mufindi, shamba hili limehifadhiwa na Wakala wa Misitu (*TFS*) ambapo hakuna shughuli zozote za kibinadamu zinazoendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini kwa kuwa Serikali inatambua jambo hili ambalo nimesema nataka kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni lini Serikali itamaliza kero ya maji katika ukanda huu wa baridi ambapo kuna vyanzo hivyo na hivyo kufanya tatizo la maji kuwa

historia katika maeneo ya Kata za Migohole, Kasanga, Mninga, Mtwango, Idete pamoja na maeneo mengine ya Makungu, Kiyowela na Mtambula?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza, kwa kuwa suala la maji ni mtambuka na ni muhimu sana, katika eneo hilo la Mufindi Kusini kulikuwa na mradi ulikuwa unaitwa Imani, ni lini Serikali itakwenda kuufufua kwa kuboresha miundombinu ili wananchi waliokuwa wananufaika waweze kunufaika *especially* kwenye Kata za Ihoanza, Malangali, Idunda, Mbalamaziwa, Nyololo, Maduma na Itandula?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Mbunge David Kihenzile kwa namna ambavyo amekuwa mfuatiliaji mzuri sana wa matatizo ya maji katika Jimbo lake. Hii ni kawaida yake kwa sababu pia amekuwa akitoa ushirikiano mkubwa kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza tatizo la maji litakoma lini, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama Ilani ya CCM inavyotutaka Serikali kuhakikisha kufika mwaka 2025 tuweze kukamilisha maji vijijini kwa 95%, kwa maeneo ya Mufindi tutahakikisha mwaka ujao wa fedha tunakuja kuweka nguvu ya kutosha ili libaki kuwa historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la kufufua miundombinu, katika maeneo mbalimbali suala hili linaendelea kutekelezwa.

Katika eneo la Mufindi, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha tutakuwa tumeshafanya kwa sehemu kubwa kuona miundombinu chakavu tunaitoa na tunaweka miundombinu ambayo inaendana na matumizi ya sasa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Liwale unakua kwa haraka sana na mahitaji ya maji yamekuwa ni makubwa na uhaba wa maji ni mkubwa sana. Bajeti iliyopita tuliletewa fedha shilingi milioni 100 kwa ajili ya kutafuta chanzo cha pili cha maji cha Mji wa Liwale lakini mpaka leo tunaambiwa *DDCA* hawana nafasi ya kuja Liwale. Ni lini Serikali watakuja sasa kutafuta chanzo cha pili cha maji kwa ajili ya Mji wa Liwale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Liwale. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anafuatilia na amekiri tumewapatia shilingi milioni 100. Nachoweza kumwambia hawa *DDCA* nitawasimamia na nitahakikisha ndani ya mwezi huu Aprili watakuja ili waweze kuona kwamba shughuli ambayo ilipaswa kufanyika basi sasa inaenda kutekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Kilolo inafanana kabisa na Wilaya ya Mufindi; na kwa kuwa vyanzo vya mito kama Mto Mtitu na Mto Lukosi vinachangia kwa kiwango kikubwa kwenye vyanzo vikubwa vya mabwawa na pia ni vyanzo ambavyo vinasaidia katika nchi yetu. Je, ni lini Wizara itajibu kiu ya wananchi kwa kutatua tatizo la maji kwa kutoa fedha kwenye Mradi wa Mto Mtitu ambapo tayari *RUWASA* walishatoa na maji hayo yatafika hadi Iringa Mjini lakini pia yatahudumia kata zaidi ya 15 za Wilaya ya Kilolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge alivyokiri kwamba tayari shughuli zinaendelea pale kupitia Wakala wetu wa Maji Vijijini (RUWASA). Kadiri tunavyopata fedha tunahakikisha tunagawa katika maeneo yote ambayo miradi ipo kwenye utekelezaji.

Kwa hiyo, pamoja na mradi huu ambao upo katika Jimbo lake na ni Jimbo ambalo tumelitendea haki kwa sehemu kubwa sana, tutaendelea kupeleka fedha kadiri tunavyopata ili kuhakikisha mito yote ambayo mmebarikiwa watu wa Kilolo na maeneo mengine yote tunashughulikia kwa wakati. Lengo la Wizara ni kuhakikisha wananchi wanapata maji bombani na si vinginevyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 6

### **Ujenzi wa Barabara ya Mtwara hadi Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Mtwara Pachani – Nallasi – Tunduru itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*), imekamiliha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani – Lingusenguse – Nalasi Tunduru yenye urefu wa kilometa 300 kwa kiwango cha lami. Kazi hii ilitekelezwa na Mhandisi Mshauri *GEG* wa Ureno kwa gharama ya shilingi bilioni 2.559 na ilikamilika mwaka jana (2020). Kwa sasa, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ujenzi wa kiwango cha lami ukisubiri upatikanaji wa fedha, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara nchini, inaendelea kuihudumia barabara hiyo ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka huu wa fedha 2020/2021, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 2.293 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri kwa kufanikisha kufanya upembuzi yakinifu na kutengeneza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imesema inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami barabara hiyo na wananchi walio katika maeneo au waathirika wa barabara hiyo bado wanakuu ya kupata fidia yao kwa ajili ya maeneo hayo. Je, ni lini Serikali itaanza kutoa fidia kwa waathirika wa barabara hiyo kutoka Mtwara Pachani, Lingusenguse, Nalasi mpaka Tunduru mjini?



Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imetenga shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida kwenye barabara hiyo; na kwa kuwa madaraja manne kwenye barabara hiyo yamezolewa na mvua, Mto Sasawala, Lingusenguse, Mbesa pamoja na Lukumbule. Je, Serikali haioni haja ya haraka kupeleka hizo shilingi bilioni 2.2 ili kukamilisha kurekebisha madaraja hayo yaliyoharibika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fidia litaanza pale ambapo barabara itaanza kujengwa. Awamu ya kwanza ilikuwa ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi umeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa nini fedha ya matengenezo iliyotengwa kwa kuwa madaraja yameshazolewa isipelekwe huko. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru kwamba mpaka leo asubuhi madaraja yote ya kutokea Tunduru daraja la kwanza la Mbesa, Mchoteka sasa yanaweza yakapitika na hivi leo wameanza daraja kubwa la Mto Sasawala na tunaweka ndani ya muda mfupi daraja hili litaanza kupitika ili kuweza kuunganisha Tunduru na eneo la Mtwara Pachani. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo yanayowapata wananchi wa Tunduru yanafanana kabisa na matatizo ambayo yanawapata wananchi wa Kigamboni katika Mkoa wa Dar es Salaam. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga barabara ya Kibada - Kisarawe *Two* - Mwasonga - Tumbi Msongani ili kuwasaidia wananchi Wilaya ya Kigamboni waweze kupata unafuu wa usafiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam kuhusu barabara za Kigamboni. Hiki ni kipindi cha bajeti na kama tulivyoahidi barabara hizi zitajengwa ndani ya miaka mitano, kwa hiyo kwenye bajeti pengine suala la kuanza usanifu wa awali na wa kina litajitokeza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizi kama tulivyoahidi zitajengwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya Mgakolongo kwenda Kigalama mpaka Mlongo inayounganisha na nchi ya Uganda, usanifu wake umeshakamilika muda mrefu. Ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ipo kwenye Ilani na nimuombe Mheshimiwa Mbunge awe na

subira tuone bajeti ambayo tunaiandaa hiyo barabara itashughulikiwaje. Kwa sasa siwezi nikasema chochote maana ndiyo tuko kwenye kipindi cha bajeti, kwa hiyo, naomba awe na subira aone kama barabara yake itajengwa lakini tunatambua ni barabara muhimu sana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Senguruka, swali la nyongeza .

**MHE. OLIVER D. SEMGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Changamoto ya barabara iliyoko Tunduru Kusini inafanana kabisa na changamoto iliyoko wilaya ya Ngara ya barabara ya Murugalama - Lulenge - Mizani yenye urefu wa kilomita 85. Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali la nyongeza la kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hii barabara aliyoitaja ambayo inapita eneo la Mgalama - Lulenge nina hakika zitajadiliwa katika kipindi hiki cha bajeti, kwa hiyo, awe na subira.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe.

Na. 7

### **Daraja la Kisorya – Rugezi – Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, ni lini Daraja la Kisorya – Lugezi litakalounganisha Wilaya za Bunda na Ukerewe litajengwa ili kurahisisha ukuaji wa uchumi wa wananchi wa Wilaya hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa daraja litakalounganisha Wilaya ya Bunge na Ukerewe ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba – Kisorya – Nansio yenye urefu wa kilometa 121.6 ambao utekelezaji wake umeanza na uko katika hatua mbalimbali. Kazi ya upembuzi yakinifu na usaniifu wa kina wa barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba hadi Kisorya yenye urefu wa kilometa 107.1 ilikamilika Machi, 2013. Aidha, usaniifu wa kina wa sehemu ya barabara ya Kisorya – Rugezi – Nansio (Ukerewe) yenye urefu wa kilometa 14.5 pamoja na Daraja la Rugenzi – Kisorya ulikamilika Aprili, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu tatu, yaani Lots tatu, ambazo ni Nyamuswa – Bunda – Bulamba (Lot I) yenye urefu wa kilometa 56.1; Lot II bulamba – Kisorya yenye km. 51 na Lot III Kisorya – Lugezi – Nansio yenye urefu km. 14.5 inayojumuisha na daraja la Kisorya – Rugezi yaani daraja lina urefu wa mita 1000. Hadi sasa ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Bulamba – Kisorya ambao ni Lot II umekamilika. Ujenzi wa sehemu ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba Lot I kwa kiwango cha lami unaendelea na umefikia asilimia tano. Aidha, ujenzi wa sehemu ya Rugezi – Nansio Pamoja na daraja la Kiisorya – Rugezi utaanza baada ya fedha kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa sehemu ya Kisorya – Rugezi – Nansio ikiwemo ujenzi wa daraja Serikali kupitia wakala wa ufundi na umeme TEMESA inaendelea kutoa huduma ya

kuvusha wananchi wa maeneo haya kupitia kivuko cha MV Ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu la Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua jitihada za Serikali kuboresha usafiri kati ya Rugezi kwenda Kisorya. Hata hivyo, kutokamilika kwa hili eneo la Lot III na hasa barabara ile ya kilometa 14 kutoka Rugezi – Nansio inaathiri sana uchumi wa wananchi wa Ukerewe, na ndiyo maana tarehe 04 Septemba, 2021 Hayati Dkt. John Magufuli akiwa Ukerewe, kwa kutambua changamoto hizi alitoa maelekezo eneo hili lifanyiwe kazi mara moja. Mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa Ukerewe alisisitiza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwanini sasa Wizara isione umuhimu wa jambo hili ikatenga pesa kwa haraka ikaufanya kama mradi wa haraka ili Lot III, hasa wakati wanasubiri pesa za kujenga daraja basi barabara km. 14 kati ya Rugezi kwenda Nansio iweze kukamilika kwa haraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer* Kasekenya Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi Mbunge wa ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Ukerewe. Lakini Mheshimiwa Mbunge yeye pia atatambua kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa sana kuhakikisha kwamba inatengeneza barabara na ndiyo maana imegawanywa

kwenye *Lot III*. Lot ya pili imeshakamilika, lot ya kwanza mkandarasi yuko *site* na Serikali imeahidi kwamba inatafuta fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja tunaloliongelea urefu wake unafanana na daraja karibu lile linalojengwa la pale *Surrender Bridge*, ni takriban kilometa moja. Kwa hiyo Serikali lazima ihakikishe kwamba inajitahidi kupata fedha ya kutosha ili kuweza kujenga daraja hilo; na ndiyo maana tayari usanifu wa kina umeshafanyika. Tayari Serikali imeonesha jitihada za makusudi, kwamba kwanza ni ahadi ya Hayati Rais, lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo Serikali kama nilivyosema kwenye jibu la msingi inaendelea kutafuta fedha na fedha ikipatikana nina uhakika kipande hiki cha *Lot* ya tatu kitajengwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tuko katika Wizara ya Ujenzi, na Wizara hii ndiyo inayoshughulikia barabara pamoja na madaraja, sasa nilitaka kuuliza swali linalohusu barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitutembelea kule Milola na tukampa kero yetu ya barabara ambayo inatoka Ngongo inapitia Rutamba, Milola hatimaye inamalizikia Ruangwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alituahidi kwamba barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami.

Sasa, je, ni lini barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba

kujibu swali la nyongezala Mheshimiwa Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambayo iliahidiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ipo kwenye mipango, na ninaamini usanifu wa awali unaweza ukaanza kwa sababu hatujapita bado kwenye bajeti. Niombe kujiridhisha, Mheshimiwa Salma nimuombe baada ya kikao hiki pengine tuweze kukutana naye ili tuweze kuona barabara hii iko kwenye mpango kwasababu sasa hivi tuko bajeti kwa hiyo ni ngumu kusema barabara hii iko kwenye hatua gani. Kama ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kama iko kwenye ilani naamini itakuwa ni barabara ambazo ziko kwenye matazimio ya kufanyiwa kazi na hasa upembuzi yakinifu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuwa barabara inayoanzia King’ori, hadi Ngarenanyuki imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Arumeru Mashariki, na Serikali imekuwa ikiahidi mara nyingi kujenga barabara ii katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kufahamu ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi yake kwa wananchi wa Arumeru Mashariki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Magige kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba ni lini barabara ya Kilole kwenda Ngarenanyuki itajengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hizi zote ambazo zimeainishwa tuna uhakika

tutazikamilisha katika kipindi hiki cha miaka mitano. Lazima kutakuwa na mahali tutaanza na barabara chache lakini tutamaliza zote. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara zote ambazo zimeainishwa na ambazo zimeahidiwa zipo kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Kipaumbele ni zile barabara ambazo zinaunganisha mikoa na mikoa, wilaya na wilaya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Iringa Mjini kupitia Jimbo la Kalenga kwenda Kilolo kilometa 133 ambayo ina madaraja ni barabara ambayo ilikuwa ni ahadi ya hayati Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, alipofika pale akatoa ahadi hiyo, ni miaka mitano sasa imepita haijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lini Serikali itaijenga barabara hii ili angalau kumuenzi hayati kwasababu alienda akaona wananchi wa kule wanavyohangaika katika kuuza mazao yao kwenda katika sehemu mbalimbali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii yenye urefu wa km. 133 iliyoko Mkoani Iringa na ambayo ni ahadi ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Hayati, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli naomba nimhakikishie kwamba Serikali haitaacha ahadi zote ambazo zimeahidiwa na Mheshimiwa Rais. Nataka nimhakikishie kwamba barabara



zote ambazo zimeahidiwa na Mheshimiwa Rais ikiwa ni pamoja na hiyo zitajengwa kwa kiwango cha lami awamu kwa awamu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa tunaenda kwenye Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 8

### **Hitaji la Umeme wa REA kwa Mitaa 30 Ilivyosalia Handeni**

**MHE. REUBEN N. KWAGILWA** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi katika mitaa 30 isiyo na umeme Wilayani Handenni watapatiwa umeme kulipia mradi wa REA?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Reubne Nhamanilo Kwagilwa Mbunge wa Handeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vijiji, mitaa na vitongoji visivyokuwa na umeme kupitia miradi mbalimbali. Kwa sasa mkandarasi Kampuni ya M/S Sengerema Engineering Ltd. amepewa kazi ya kupeleka umeme katika vijiji 15 na mitaa vitongoji zaidi ya 30 katika Wilaya ya Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hizo zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 0.4 umbali wa km. 27.5, ufungaji wa transfoma 11 za 50 kVA na 100 kVA; pamoja na kuwaunganisha wateja wa awali 669. Mradi unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 3.36. Utekelezaji wa mradi umeanza mwezi Februari, 2020 na utakamilika ifikapo Disemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *TANESCO* inaendelea kuunganisha umeme kwa wateja ambao hawajaunganishiwa umeme katika mitaa na vitongoji vya Tanzania Bara ikiwemo Wilaya ya Handeni kupitia majukumu yake ya kila siku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, swali la nyongeza.

**MHE. REUBEN N. KWAGILWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza ili yaweze kupata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Wilaya ya Handeni ina majimbo mawili ya uchaguzi na mimi ni muwakilishi wa Jimbo la Handeni Mjini, je, Serikali haioni haja ya kuongeza wigo wa idadi ya vijiji ambavyo havijapata umeme upande wa Handeni Mjini hasa katika Kata ya Mlimani Konje, Kideleko kwa Magome, Kwenjugo, Kwadyamba, Malezi na Mabada?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kumekuwa na hali ya kukatika katika kwa umeme kila mara hali inayopelekea kuwapatia hasara wananchi kwa vyombo vyao vya umeme lakini vilevile kushindwa kufanya shughuli zao za kiuchumi za uzalishaji. Ni lini Serikali itakomesha tatizo hili wananchi wa Handeni Mjini washiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Reuben Mbunge wa Handeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya tatu, mzunguko wa pili wa *REA* unapeleka umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara ambavyo havikuwa na umeme ambavyo mpaka sasa

havizidi 1974. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji vyake vyote ambavyo havikuwa na umeme vitapata umeme katika awamu hii ya tatu, mzunguko wa pili ambayo imeanza tayari mwezi wa nne huu na itakamilika kufikia Desemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo linaenda pia kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote wa Tanzania Bara, kwamba vijiji vyote ambavyo havikuwa vimepata umeme vimeingizwa katika awamu ya tatu, mzunguko wa pili na tutahakikisha tunapeleka umeme katika maeneo yote hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili, ni kweli, Tanga kama Mkoa na Handeni ikiwemo imekuwa na matatizo ya kukatika kwa umeme ikiwemo Mikoa wa Mbeya Pamoja na Mkoa wa Kagera. Hata hivyo Wizara kwa kushirikiana na *TANESCO* imechukua juhudi mbalimbali kuhakikisha inamaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa Mkoa wa Tanga na hasa Handeni tatizo kubwa lilikuwa ni miundombinu chakavu ambayo ilikuwa inapelekea umeme katika maeneo hayo; na hivyo yamefanyika mambo mawili moja ni la sasa na lingine ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme unaokwenda Handeni unatokea katika kituo chetu cha Chalinze unakwenda kwenye substation ya Kasija, unatoka Kasija unakwenda Korogwe – Handeni – Kilindi, na njia ndefu sana ina km. zaidi ya 500. Kwa hiyo, tumebaini kuna nguzo zaidi ya 1300 ambazo zilikuwa zimeoza zimeanza kufanyiwa marekebisho na kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tunavyoongea sasa tayari nguzo zaidi ya 500 zimerekebishwa, na tumehakikisha kwamba kufikia mwishoni mwa mwezi wa nne, nguzo zote 1300 zitakuwa zimerekebishwa na kuhakikisha kwamba basi umeme haukatiki hovy.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hatua ya pili ambayo ni ya kudumu na ya muda mrefu tumeshauriana na kukubaliana na wataalam, tumekubaliana tujenge kituo kidogo cha kupoza umeme pale Handeni. Kwa hiyo tutatoa umeme Kasija kwenye kituo cha kupoza umeme cha sasa tutapeleka Handeni, km. 81 kwa gharama ya shilingi bilioni 4nne. Tukishajenga kituo hicho cha kupoza umeme pale Handeni basi tutatoa line moja ya kuhudumia Handeni, tunatoa line moja kwenda Kilindi na line nyingine moja itaenda kwenye machimbo ambayo tumeambiwa itaanzishwa siku si nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo tunahakikisha kwamba basi tatizo la kukatika umeme Wilaya yetu ya Handeni na majimbo yote mawili litakuwa limfikia ukomo na tutakuwa tuna uhakika wa umeme.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hapo umetoa maelezo marefu na mimi ninakupongeza sana. Sasa hapo umeitaja Mbeya halafu kule hujaeleza tatizo ni nini, maana huko kwingine umesema ni nguzo haya Mbeya unakatika katika kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoitaja Mbeya nikaitaja Kagera kwasababu na mimi natokea Kagera ili utakaponipa nafasi ya kuzungumzia Mbeya basi na Kagera nipitie humo humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbeya tunayo matatizo makubwa mawili, tatizo moja kubwa ni radi ambazo zimekuwa zikisumbua mifumo yetu ya umeme kwenye transfoma. Tatizo hilo pia liko Mkoa wa Kagera. Tulichokifanya katika mikoa hii miwili tumeanza kufunga vifaa vinaitwa *auto recloser circuit breaker* ambayo vinazuia radi isirudi kwenye maeneo mengine ambayo hayajaathirika hilo ni tatizo moja kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tatizo la pili lilikuwa ni uchakavu wa miundombinu kwenye maeneo hayo. Tumeunda vikosi kazi maalum katika mikoa hiyo mitatu,

Mbeya, Tanga na Kagera ya kuhakikisha kwamba kinapitia kila eneo na kubaini tatizo kubwa ni nini ili iweze kurekebisha. Vikosi kazi hivyo viko kazini, vinafanya kazi; na tunahakikisha kufikia mwezi wa sita, maeneo yote ambayo yalikuwa yana matatizo sugu yatakuwa yamefanyiwa kazi na kurekebishwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. RASHIDA A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Matatizo ya usambazaji wa umeme vijijini yaliyopo Handeni ni sawa kabisa na yaliyopo kule Lushoto katika Jimbo la Mlalo. Hivi ninavyozungumza tunapoelekea kwenye robo ya tatu ya mwaka wa fedha ambao unakaribia kwisha hakuna hata kijiji kimoja ambacho REA wamesambaza umeme. Sasa tunataka kujua, wananchi wa Lushoto hususan Jimbo la Mlalo wameikosea nini hii Serikali hii ya Awamu ya Tano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Soika, kama nilivyotangulia kujibu kwenye swali la msingi. Maendeleo ni hatua, na tulianza na vijiji vichache na tunazidi kuongeza, na katika awamu ya tatu mzunguko wa pili wa REA vijiji vyote ambavyo vilikuwa havijapata umeme vitapatiwa umeme.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi kwamba kabla ya mwaka 2022 Disemba vijiji vyote vya kwenye Jimbo lake la Lushoto viitakuwa vimepatiwa umeme kama nilivyotoa majibu kwenye swali la msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri wa Nishati alikuja Musoma, na ninamshukuru kwamba tulienda naye pale kwenye Kata ya Bweli, Mtaa wa Bukoba tukaweza kuwasha umeme, na baada ya hapo tukaenda kwenye mkutano wa hadhara akaahidi kwamba sasa maeneo yote ya Musoma Mjini wataweza kupata umeme kwa gharama ya 27,000.

Hata hivyo, kila wananchi walipojaribu kwenda kulipia wanaambiwa mpaka waraka utoke kwa sababu haujapatikana. Sasa napenda kujua ni lini Mheshimiwa Waziri wa Nishati atatoa waraka ili wale wananchi wangu wa Jimbo la Musoma waweze kupata umeme kwa gharama nafuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Manyinyi, Mbunge wa Musoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kabisa kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Waziri yaliyotolewa yanatakiwa kuzingatia na kusimamiwa kama ilivyo na kwa kuwa tumesikia kuna lalamiko la namna hiyo, naomba tulichukue na tutahakikisha kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Waziri yanafanyiwa kazi kama ilivyoelekezwa, hakuna kupindisha maelekezo yaliyotolewa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa changamoto ya umeme wa Jimbo la Handeni inafanana kabisa na Jimbo la Arusha Mjini, napenda kuuliza maswali ya nyongeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Jiji la Arusha ni jiji la kitalii, lakini bado kuna kata ambazo zinachangamoto kubwa sana ya umeme Kata kama za Telati, Kata ya Olasiti, Olmoti, Moshono, Mulieta kule maeneo ya Losoito, Sokoni 1 na Sinoni. Ningependa kufahamu, je, Wizara ina mpango gani kupitia Mradi wa *Peri-urban* ili kuhakikisha kwamba wananchi hawa ambao wapo kwenye Jiji la Kimataifa, Jiji la Utalii wanaondokana na changamoto ya umeme katika jimbo letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa moja tu, hilo ni la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ukiwa nayo mengi unapeleka swali la msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gambo, Mbunge wa Arusha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inapeleka umeme katika maeneo mbalimbali kwa *programmes* tofauti. Ziko awamu za *REA* ambazo zimeendelea, ziko *programme* ya *densification*, lakini ipo programu *peri-urban* ambayo inapeleka umeme kwenye maeneo ambayo yana asili ya ukijiji lakini yako mjini. Mkoa wa Arusha tayari umeshanufaika na awamu ya kwanza ya *densification*, *peri-urban* kupeleka umeme katika baadhi ya maeneo na iko awamu ya pili ya *peri-urban* ambayo itakuja, inaanza mwezi wa Saba.

Katika maeneo ambayo hayajapata Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Tanga yatapelekewa umeme katika Mradi huo wa pili wa *peri-urban*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba awamu hiyo ya pili ikianza basi na yeye maeneo yake yatapatiwa umeme katika awamu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mbunge wa Butiama, sasa aulize swali lake.

Na. 9

### **Hitaji la Umeme katika Vitongoji – Butiama**

**MHE. JUMANNE A. SAGINI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itazipatia umeme kaya na vitongoji ambavyo havijapatiwa umeme Wilayani Butiama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mbunge wa Butiama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika mitaa na vitongoji ambavyo havijapata umeme ikiwemo Wilaya ya Butiama. Serikali imeanza maandalizi ya kutekeleza mradi unaohusishwa ujenzi wa miundombinu ya umeme ya njia ya msongo wa kilovoti 0.4 zenye urefu wa kilometa 1,620, ufungwaji transformu 648 na kuunganisha wateja wa awali 48,600 katika vitongoji 648 nchini ikiwa ni pamoja na kaya na vitongoji vya Wilaya ya Butiama ambavyo havijapata umeme. Gharama ya mradi huuni shilingi bilioni 75. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza julai, 2021 na kukamilika mwezi Desemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huu kutatimiza azma ya Serikali ya kufikisha huduma ya umeme katika vitongoji vyote vya Wilaya ya Butiama.



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, swali la nyongeza.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Jimbo la Butiama lina vitongoji 370, katika awamu zote mbili nilizopita za *REA* ni vitongoji 147 tu vilipata umeme sawa na asilimia 40. Sasa Naibu Waziri ananihakikishiaje kwamba pia kama njia ya kumwenzi baba wa Taifa, vitongoji 223 vilivyosalia vitapata umeme katika awamu ijayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; sera ya Wizara ni kwamba unapopita umeme taasisi za elimu au afya zilizoko katika maeneo hayo zinapaswa pia kuhakikisha kwamba zinafungiwa umeme, lakini ninazo taarifa katika Jimbo la Butiama zipo shule za sekondari, vituo vya afya na zahanati ambavyo havijapata umeme. Je, Waziri atanihakikishiaje kwamba vituo hivyo vinapata umeme, orodha ninayo ndefu lakini atuhakikishie kwamba *TANESCO* walioko kule wanaweza wakashusha umeme kabla ya utekelezaji ya awamu ijayo anayosema inayoanza mwezi Julai?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Sagini, Mbunge wa Butiama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Butiama ni mojawapo ya Wilaya ambayo tayari zimepata umeme katika vijiji vyote vilivyoko na kweli kuna baadhi ya vitongoji ambavyo havijapata umeme. Upelekaji wa umeme kwenye vitongoji ni zoezi endelevu na ni kwa awamu na tunapeleka umeme katika maeneo haya kupitia *TANESCO* kufanya kazi zao za

kila siku lakini pia kupitia katika miradi tuliyokuwa nayo ambayo ilikuwepo *densification I, densification IIA, IIB* na sasa mwezi wa Saba tutaanza *densification IIC* ambapo kama tulivyosema tutapeleka vitongoji 648.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vitongoji vyote vilivyoko katika Wilaya ya Butiama, awamu kwa awamu vitapelekewa umeme na vyote vitapatiwa umeme vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, nipende kusema kwamba ni kweli zipo baadhi ya taasisi ambazo zimekuwa zikiachwa bila kupelekewa umeme, lakini wakati wa kuzindua mradi wa *REA*, awamu ya tatu, mzunguko wa pili, maelekezo ya Wizara ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati, yalisema kwamba katika kupeleka umeme katika awamu hii ya tatu, kisiachwe kijiji au eneo lolote ambalo lina taasisi ya umma ambayo haitapelekewa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, uniruhusu nirudie maelekezo yake kwamba wakandarasi wote wanaopeleka umeme katika awamu ya tatu, mzunguko wa pili, wasiache kupeleka umeme katika taasisi zote za umma ambazo ziko katika maeneo yetu. Vile vile, uniruhusu nisisitize maelekezo mengine mawili ambayo Mheshimiwa Waziri aliyatoa, mojawapo ikiwa ni kwamba watakapokwenda Wakandarasi kupeleka umeme katika maeneo yetu, pamoja na watu wengine na taasisi nyingine watakazoenda, wahakikishe wanapiga hodi kwa Waheshimiwa Wabunge ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwaonyesha maeneo ambayo yana changamoto zikiwa ni pamoja na hizo ambazo ni taasisi zetu za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo la mwisho, alilolitoa ni kwamba ni lazima upelekaji wa umeme ukamilike ndani ya muda ambayo ni kufikia Disemba, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fletei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI I. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Jimbo la Butiama ni majimbo ya zamani kama ilivyo Mbulu Vijijini na changamoto ya umeme karibu zinafanana. Zipo Kata za Masieda, Eda Chini, Eshkesh ambazo Mheshimiwa Waziri naye alikuja akazona. Je, ni lini sasa maeneo hayo niliyoyataja yatapata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awamu ya tatu, mzunguko wa pili wa *REA*, unapeleka umeme katika vijiji vyote vilivyokuwa vimebakia katika awamu zilizotangulia bila kupelekewa umeme.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba katika awamu hii inayoanza ambayo pengine imeshaanza kwenye maeneo mengine na kufikia Disemba, 2022 vijiji vyote vilivyo katika eneo lake vitapata umeme na vitongoji vitapata umeme kupitia utaratibu huo huo kwa sababu mkandarasi anapopeleka umeme kwenye Kijiji kimsingi anaunganisha wateja kwenye vitongoji na kuunganisha wateja kwenye kaya na mteja mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwa ujumla kwamba vijiji vyote Tanzania Bara vilivyokuwa havina umeme, vitapelekewa umeme katika awamu ya tatu, mzunguko wa pili wa *REA* bila kukosa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itatusaidia kupeleka umeme katika Kata ya Kasokola na Mwamkulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sebastian, Mbunge wa Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote vilivyokuwa havijapelekewa umeme katika awamu zilizotangulia zitapelekewa umeme katika awamu hii ya tatu, mzunguko wa pili na vijiji kwa kuwa viko kwenye kata, kata hizo pia zitakuwa ni sehemu ya kupata umeme huo ambao Serikali imejipanga vyema kabisa kuhakikisha kwamba umeme unawafikia wananchi katika kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Aprili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Matatizo yaliyopo katika Wilaya ya Butiama Mkoa wa Mara yanaonyesha uhalisia wa Wilaya zote ndani ya Mkoa wa Mara kwenye kadhia ya umeme na kwa sababu umeme unaweza kuimarisha usalama na kuweza kukuza uchumi kwa maana kupitia uanzishwaji wa viwanda na vitu vingine. Ningependa kujua ni lini sasa Serikali itahakikisha umeme unapatikana katika wilaya zote ndani ya Mkoa wa Mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wilaya zote Tanzania Bara zina umeme, maeneo machache katika wilaya hizo ndiyo hayajafikiwa na umeme, kwa hiyo nimhakikishie kwamba maeneo hayo machache ambayo bado hayajafikiwa na umeme kwa maana ya vijiji yatakuwa yamepatiwa umeme

katika miezi 18 ijayo. Kama ni umeme wa uhakika kama nilivyotangulia kujibu maswali yaliyotangulia ya msingi, Serikali inaendelea kuwa na jitihada za kuhakikisha inatenga bajeti kuhakikisha inawawezesha *TANESCO* kuendelea kurekebisha miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pamoja na hayo, pia Serikali inatekeleza miradi mikubwa sana ya ufuaji wa umeme Tanzania bara ikiwemo ya Mwalimu Nyerere itakayozalisha *megawatt* 2,115, Rusumo *megawatt* 80, Kagati *megawatt* 14, Ruhudji *megawatt* 358 na Rumakali *megawatt* 222. Miradi yote hiyo ikikamilika tutaweka umeme mwingi sana kwenye *grid* yetu ya Taifa na kuweza kumpatia kila mmoja umeme wa kutosha. Kwa hiyo tunawahakikishieni Wabunge wote kwamba umeme upo na utaendelea kuongezwa, tutarekebisha miundombinu yetu ili kila moja aweze kufikiwa na umeme ili Tanzania ya viwanda iweze kuwa ya kweli.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo la Manyoni Magharibi ambako mimi natoka kwa maana ya Halmashauri ya Itigi kuna vijiji 15 na vitongoji kadhaa bado havijafikiwa umeme. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje juu ya vijiji vyangu ni lini vitapata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali hilo kutoka kwa Mheshimiwa Massare, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Massare, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida ni kati ya mikoa ambayo imejengewa kituo kikubwa kabisa cha kupoza umeme na kipo kingine kinachoongezwa kikubwa pia kwa ajili ya kupitisha umeme kutoka Iringa kupita Singida kwenda

Arusha kwa ajili ya kwenda nje ya nchi ambapo ni Arusha kwenda Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida ni mkoa ambao hauna matatizo ya umeme na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo machache ambayo kwake bado hayajapata umeme, yataendelea kupelekewa umeme kwa kupitia taasisi yetu ya *TANESCO*, lakini kwa kupitia awamu mbalimbali ikiwemo *REA* awamu ya tatu, mzunguko wa pili, ambao kwa sasa unaendelea kwa sababu umeme tunao wa kutosha na tunao uwezo wa kupeleka lakini ni kwa awamu kwa awamu kama nilivyotangulia kusema.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Meatu liko nyuma katika utekelezaji wa umeme wa *REA*, kwa kuwa ni asilimia 46 tu ndiyo iliyotekelezwa. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka kwanza kwenye kata saba ambazo hazijafikiwa kabisa ambazo ni Kata ya Mwamalole, Mwamanongu, Mwabuzo, Imalaseko, Kimali na Mbushi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika maswali mengine yaliyotangulia, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na *TANESCO* na *REA* tunapeleka umeme na tumejipanga kupeleka umeme katika maeneo ya vitongoji na vitongoji hivyo ndimo kata zinapopatikana, ndimo vijiji vinapopatikana na wilaya inahudumia maeneo hayo hayo. Kwa hiyo katika awamu ya tatu, mzunguko wa pili, hatujabaguwa nani aanze na nani afuate tutakwenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme katika awamu hii ya tatu, mzunguko wa pili, tumefanya mambo mawili ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na uhakika wa kupeleka umeme katika maeneo yote kwa wakati mmoja. Jambo la kwanza tulilolifanya tumegawa kazi kidogo kwa wakandarasi wachache wachache kuhakikisha kwamba basi mkandarasi anakuwa hana kazi kubwa za kufanya na hivyo kushindwa kumaliza kazi yake kwa wakati katika eneo alilopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili tulilolifanya, tumehakikisha kwamba tunapeleka wasimamizi katika maeneo hayo ya kanda na kwenye mikoja ambayo yatakuwa yanatokea *REA* kwenda kuhakikisha kwamba wale wakandarasi tuliowapeleka wanafanya kazi.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Leah kwamba katika kipindi hiki cha *REA* awamu ya tatu, mzunguko wa pili, ataona matunda makubwa na mafanikio makubwa ya upelekaji wa umeme katika maeneo yote ya vijiji na vitongoji tuliyokuwa nayo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tumalizie swali la mwisho, Mheshimiwa Assa Nelson Mekanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 10

### **Serikali kuweka Katika zao la Mchikichi**

**MHE. ASSA N. MAKANIKA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwekeza yenyewe katika zao la Mchikichi badala ya kuziachia Halmashauri ili kukabiliana na upungufu wa mafuta nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Makanika, Mbunge wa Jimbo Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 hadi mwaka 2020/2021, Serikali imewekeza Jumla ya Sh.5,820,361,798 kwa ajili ya kuendeleza zao la mchikichi ambapo hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2021 jumla ya miche bora ya michikichi 2,244,935 imezalishwa na jumla ya miche 1,456,111 imesambazwa kwa wakulima katika Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Kigoma na miche 788,824 inatarajiwa kusambazwa kwa wakulima katika msimu wa 2020/2021. Aidha, katika mwaka 2021/2022, Serikali imetenga jumla ya Sh.3,158,200,000 kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza mbegu na miche ya zao la michikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mafuta ya kula yanakadiriwa kuwa tani 570,000 kwa mwaka. Hata hivyo, uzalishaji wa mafuta ya kula nchini unakadiriwa kufikiwa wastani wa tani 205,000 na kufanya upungufu wa wastani wa tani 365,000 kwa mwaka ambapo hupelekea kama nchi kutumia wastani wa kiasi cha shilingi bilioni 474 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa mazao mengine, Serikali hwekeza katika utafiti, uzalishaji na upatikanaji wa pembejeo za kilimo, huduma za ugani, udhibiti wa visumbufu vya mazao na utafutaji wa masoko. Aidha, katika utekelezaji wa mikakati hiyo Serikali imekuwa ikishirikiana wdau mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sehemu ya mkakati wa kujitosheleza kwa mafuta ya kula, mwaka 2018, Serikali iliamua kuanzisha Kituo Maalum cha Utafiti wa Zao la Michikichi cha *TARI* Kihinga, Mkoani Kigoma ili kuendeleza zao hili kwa ufanisi zaidi. *TARI* Kihinga ikishirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (*ASA*), halmashauri na sekta binafsi katika utafiti, uzalishaji wa miche bora ya michikichi na kuisambaza kwa wakulima.



Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya umma na binafsi kuendeleza zao la mchikichi na mazao mengine ya mbegu za ili kuwezesha nchi kujitosheleza kwa mafuta ya kula. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuwekeza katika mazao ya kilimo kutokana na mapato yanayotokana na ushuru wa mazao (*produce cess*) likiwemo zao la michikichi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Assa Nelson Mekanika, swali la nyongeza.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na niipongeze Serikali kwa hatua ambazo imezichukua juu ya zao hili la michikichi, lakini vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameonsha jitihada za kipekee sana katika kusaidia zao hili la mchikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungufu wa mafuta katika nchi yetu, niipongeze Serikali tu kwamba ni kweli imewekeza jitihada kwenye kuzalisha mbegu lakini napenda kujua Serikali imejiandaaje katika kuokoa mafuta yanayopotea kwenye Mkoa wetu Kigoma katika kuwekeza kwenye teknolojia? Kwa sababu kuna mafuta mengi sana yanapotea, hata hii miche iliyopo inapoteza mafuta mengi sana kabla ya kuwekeza kwenye miche mipya hii ambayo ameisema Naibu Waziri. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mekanika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali tumeanza maongezi na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, *TIRDO* na *SIDO* kwa ajili ya kuja na teknolojia rahisi. Kwa sababu tume-*invest* katika miche baada ya miaka mitatu itaanza kutoa matokeo. Sasa itakapotoa matokeo tunakuja na mfumo wa ku-*develop* teknolojia ndogondogo ambazo

katika *household level*, wananchi wataanza kukamua mafuta na kuyafanya kuwa *crude* ili yaweze kuzalishwa na kupunguza upotevu unaoongelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amerudia jambo hili mara ya pili, katika Kamati vilevile aliraise concern hii, nataka nimhakikishie kwamba tunajadlliana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuja na teknolojia ya kupunguza hasara na upotevu.

Vilevile kuja na teknolojia rahisi ya ku-process mafuta katika *primary level*, katika *level* ya *crude*, pale ambapo miche hii itakuwa ime-mature na kuwafanya wakulima badala ya kuuza matunda wauze mafuta *crude* kwa processor wa *secondary level*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Sasa nitamkaribisha Mheshimiwa Spika kuendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

*Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *Asalaam aleykum*.

**WABUNGE FULANI:** *Waaleykum Salaam*.

**SPIKA:** Bwana Yesu Asifiwe.

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**SPIKA:** Tumsifu Yesu Kristo.

**WABUNGE FULANI:** Milele amina.

**SPIKA:** Kumekucha. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, mauti yalimfikia aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, tarehe 17 Machi, 2021 na kufanya Kiti cha Rais kuwa wazi na hivyo aliyekuwa

Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kushika nafasi ya Rais kwa mujibu wa Ibara ya 37(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ili kujaza nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara hiyohiyo ya 37(5) ya Katiba inaweka masharti kwamba baada ya kushauriana na Chama cha Siasa anachotoka Rais, Mheshimiwa Rais atapendekeza jina la mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura zisizopungua asilimia hamsini ya Wabunge wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hivyo basi, kwa mujibu wa Ibara hiyo ya 37(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, tayari amependekeza jina la mtu atakayekuwa Makamu wa Rais kupitia chama chake, kwa maana hiyo zoezi limekamilika na mimi jina hilo sina. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima, naomba nimualike ADC wa Rais aweze kuingia hapa ukumbini kuniletea jina hilo. *Serjeant-At-Arms! (Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Mpambe wa Rais - Kanali Nyambuli E. Mashauri aliingia Ukumbini kukabidhi jina linalopendekezwa la Makamu wa Rais)*

**KANALI NYAMBULI E. MASHAURI – MPAMBE WA RAIS:**

Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimeelekezwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Tanzania kuwasilisha nyaraka kwako. Kwa heshima na taadhima, naomba niwasilishe nyaraka hii. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hajaondoka, huyu ni ADC wa kwanza mwanamke tangu nchi hii ipate uhuru. *(Makofi/Vigelegele)*

Ahsante sana, nimepokea nyaraka hii toka kwa Mheshimiwa Rais, mpelekee salamu zetu za upendo. Tutaifanyia kazi kwa taratibu za Kibunge, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Subiri kidogo ADC, naweza kutakiwa nisaini kwamba nimepokea hapa. Jamani bahasha ya kwanza ni hii, bahasha ya pili ni hii nyeupe. Basi ADC nakuruhusu uweze kwenda, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa Mpambe wa Rais - Kanali Nyambuli E. Mashauri alitoka nje ya Ukumbi wa Bunge)*

**MBUNGE FULANI:** Wanawake oyee!

**WABUNGE FULANI:** Oyee!

**SPIKA:** Hiyo ya mwisho nimeipenda hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza awali, hapa tusikilizane vizuri, Mheshimiwa Rais kwa mamlaka aliyopewa na Katiba chini ya Ibara ya 37(5), amempendekeza afuataye kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aliyependekezwa, nitasoma karatasi hii kama ilivyo. *(Kicheko)*

Kwa hiyo nanukuu, imeandikwa hivi; Mheshimiwa Spika, nawasilisha Bungeni jina la Mheshimiwa, narudia tena. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbona unatupa *pressure*?

**SPIKA:** Makatibu, naomba maji ya kunywa. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mko tayari?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rais anasema, Mheshimiwa Spika, nawasilisha Bungeni jina la Mheshimiwa Philip Isdor Mpango kwa nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais amewasilisha jina la Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama na kushangilia)*

**SPIKA:** Ahsante sana, naomba mkae.

**WABUNGE FULANI:** CCM! CCM! CCM! CCM! *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa naomba mkae, maana Mheshimiwa Dkt. Mpango simuoni hapa; naomba Mheshimiwa Jenista anitafutie, Mheshimiwa Dkt. Mpango yuko wapi?

Aah jamani, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, sasa nimemuona. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Makamu wa Rais Mteule - Mhe. Dkt. Philip Mpango Alisimama)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, naomba ukae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu za Bunge hazijatoa mwongozo wa namna ya kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais. Hivyo, kwa mamlaka niliyopewa na Kanuni ya 5, natumia uzoefu wa jambo kama hili lililofanyika tarehe 13 Julai, 2001 kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais – mtakumbuka 2001 baada ya Mheshimiwa Omari Ali Juma kuwa amefariki wakati tunamthibitisha Mheshimiwa Dkt. Shein, tutafuata utaratibu huo wa wakati huo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nitamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe hoja fupi tu ya kulitaka Bunge lithibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais halafu tutaona kama

hoja hiyo itaungwa mkono. Ikishaungwa mkono basi Katibu wa Bunge atapewa fursa ya kutoa maelezo ya utaratibu wa kuthibitisha uteuzi huo na baadaye nitaeleza kitakachofuata.

Waheshimiwa Wabunge, moja kwa moja nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe neno fupi la kuweka hoja ya kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

## **HOJA YA KUTHIBITISHA UTEUZI WA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwa Bunge lako tukufu kufuatia mapendekezo ya jina la Makamu wa Rais lililoletwa mbele ya Bunge lako tukufu, jina ambalo tayari umelisoma na kwa mujibu wa taratibu na maelekezo yote ambayo umeyatoa, jina hili ambalo limeletwa na Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, linahitajika kuingia ndani ya Bunge lako, zoezi ambalo tayari limekamiliika na uweze kulitangaza, zoezi ambalo limekamiliika.

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata kwa mujibu wa maelezo yaliyoko kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jina hilo lazima lipitishwe na Bunge lako kwa zaidi ya asilimia 50. Sasa utaratibu ambao tunaweza kuutumia, kama ambavyo umedokeza kwa uzoefu ambao ulijitokeza wakati wa kifo cha Makamu wa Rais, Mheshimiwa Omari Juma, tunaweza kuufuata utaratibu uleule ambao unao juu ya Meza yako.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kutoa hoja ili utaratibu uweze kufuatwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nawashukuru sana kwa uungwaji mkono huu mkubwa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa muda si mrefu Katibu wa Bunge atatoa maelezo ya utaratibu wa jinsi upigaji kura utakavyokwenda, lakini napenda tuwe na uchangiaji kidogo ili kutoa nafasi kwa Maafisa wa Bunge kupata cv fupi ya Mheshimiwa Dkt. Mpango ambayo itasomwa baadaye hapa ndani, siyo muda mrefu ujao, baada ya uchangiaji huu mfupi na baada ya hapo ndiyo zoezi la upigaji kura litaendelea, tayari tunaendelea kuandaa karatasi za kupiga kura.

Kwa jinsi hiyo basi nitatoa dakika tano tano, lakini nadhani busara inasema nianze na Mheshimiwa Dkt. Mpango mwenyewe kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kifupi tu tunakupa nafasi ya kusema chochote kufuatia heshima hii kubwa. Baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Jenista na wachangiaji wengine. Mheshimiwa Dkt. Mpango, karibu sana. *(Makofi)*

#### **MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO - MAKAMU WA RAIS**

**MTEULE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa namna ya pekee kabisa kwa kutupatia uhai na kutuwezesha kukutana hapa ili kuendelea na shughuli zetu za Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kupendekeza jina langu na kuridhiwa na Chama chetu, Chama cha Mapinduzi, ili liweze kuletwa hapa kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge kama tulivyoelezwa kwa nafasi muhimu sana na nyeti katika taifa letu ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni heshima kubwa sana, sikuwahi kuota. Wakati Naibu wangu hapa anajibu swali nilikuwa nahangaika na mambo mengine ikiwemo na mishahara ya baadhi ya Wabunge ambayo ilikuwa haijalipwa mpaka leo asubuhi. Nimetoka nje mara kadhaa kujaribu kuhangaikia hilo pamoja na malipo mengine, kwa hiyo, nimepigwa na butwaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, labda niseme tu kwa kifupi kwamba nilizaliwa katika Wilaya ya Buhigwe katika Mkoa wa Kigoma mwaka 1957 tarehe 14 Julai, ilikuwa siku ya Jumapili. Nimesoma kule Shule ya Msingi lakini nilianza kule darasa la pili kwa sababu darasa la kwanza na nusu ya la pili nilisoma Shule ya Msingi ya Kipalapala katika Mkoa wa Tabora. Baadaye nilirudi nyumbani kijijini nikaendelea na Shule ya Msingi na nilihitimu elimu ya msingi katika Shule ya Msingi ya Muyama huko kwetu Buhigwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadaye nilikwenda Seminari ya Ujji nikasoma mpaka kidato cha pili, ndiyo ilikuwa utaratibu, ile shule ilikuwa inaishia kidato cha pili; na baadaye nilikwenda Seminari ya Itaga, Tabora ambapo nilisoma kidato cha tatu na cha nne. Baadaye Upadre ulinishinda, naamini Mwenyezi Mungu hakunipangia wito huo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikwenda high school, Shule ya Sekondari ya Ihungo kule Bukoba ambapo nilihitimu mwaka 1977. Baada ya pale nilikwenda Jeshi la Kujenga Taifa kama ilivyo ada kujifunza juu ya ukakamavu na ulinzi wa nchi yetu, lakini pia ilikuwa muhimu sana kwa uzalendo wa Taifa letu. Nilikwenda Jeshi la Kujenga Taifa Bulombola, Kigoma na baadaye nilikwenda JKT Mlale kule kwa watani zangu Songea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya pale nilifanya kazi kabla ya masomo ya Chuo Kikuu na nilifanya kazi iliyokuwa inaitwa *NPF* kwa muda mfupi na baadaye nilifanya kazi Shirika la Umma linaitwa *Elimu Supplies*. Nilitoka pale nikaenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo nilifanya Shahada ya Uchumi na nilihitimu shahada ya kwanza mwaka



1984. Baada ya pale nilifanya kazi Wizara ya Kazi, tulikuwa na Idara inaitwa Nguvu Kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilifanya kazi toka mwaka huo wa 1985 mpaka mwaka 1986 niliporejea Chuo Kikuu kwa ajili ya Shahada yangu ya pili katika Uchumi. Hivyo mwaka 1988 nilipomaliza Shahada ya pili ya Uchumi niliajiriwa kama Mkufunzi (*Tutorial Assistant*) kwanza halafu baadaye nikawa *Assistant Lecturer* huo mwaka 1988. Mwaka uliofuata nilikwenda masomoni kwa ajili ya Shahada ya Uzamivu. Nilikwenda Chuo Kikuu cha Lund kule Sweden, tulikuwa na programu ambayo ni *sandwich*, unafanya *coursework* kule halafu unarudi kufanya utafiti nyumbani.

Mheshimiwa Spika, nilirejea mwaka 1992 nikaendelea na utafiti na kuendelea kufundisha. Mwaka 1996 nilihitimu Shahada ya Uzamivu katika Uchumi na niliendelea kufanya kazi yangu ya ualimu pale Chuo Kikuu, Idara ya Uchumi na Utafiti. Nilifanya kazi hiyo mpaka mwaka 2002 ambapo niliomba *sabbatical leave* nikaenda kufanya kazi Benki ya Dunia kama Mchumi Mwandamizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haukuwa uamuzi mwepesi sana, labda niwaambie kwamba niliamua kwenda kule ili nijifunze taasisi hizi kubwa ambazo zinasukuma sera na kadhalika kwa nchi zetu zinafanyaje fanyaje? Kuna nini kule ndani? (*Makofi*)

Kwa hiyo, nilifanya kazi pale na niliaminiwa kusimamia baadhi ya miradi hasa upande wa matumizi ya Serikali. Wakati ule kulikuwa kuna kitu kinaitwa *public expenditure review* na mimi nilikuwa Katibu wa ile timu ya Benki ya Dunia na Serikali ambayo ilikuwa inaratibu zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliniteua kuwa msaidizi wake katika masuala ya uchumi kutoka Benki ya Dunia. Nilianza kazi ile mwezi Januari mwaka 2007 baada ya utumishi wa miaka mitano pale Benki ya Dunia Ofisi ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, nilitumikia katika nafasi hiyo mpaka mwaka

2010 ambapo aliniteua kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha wakati ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitumikia pale na baada ya hapo alinihamisha na kunipeleka kuwa Mkuu wa Tume ya Mipango nchini hususan kwa kazi kubwa ya kuandaa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano. basi nilitumikia pale kwa takribani miaka mitano na kidogo. Kwa hiyo, Mpango wa Pili wa Miaka Mitano uliandaliwa nikiwa Mkuu wa Tume ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliniteua nikiwa pale kama Mkuu wa Tume ya Mipango akanipeleka kuwa Kaimu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Nilifanya kazi ile kwa mshangao kama leo kwa muda wa takribani mwezi mmoja. Ilikuwa kazi ngumu sana, ngumu kweli, kwa sababu tulipewa kazi ya kusema lazima tuongeze mapato ya Serikali. Kwa hiyo, wakati bado nadhani nimezoea zoea sasa kukusanya mapato na changamoto zake, saa mbili usiku, nafikiri ilikuwa tarehe 23 nikiwa ofisini ndiyo rafiki zangu wakaniambia Mheshimiwa Rais amekuteua kuwa Mbunge na Waziri wa Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sauti yangu siku ile ilikuwa; "Mungu wangu nisaidie, Mungu wangu nisaidie," kwa sababu niliona sasa mzigo ni mkubwa zaidi kama ambavyo imekuwa hivi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi yaliyobaki walio wengi mnayafahamu, nimekuwa mmoja wenu kama Mbunge wa Kuteuliwa kwa miaka mitano, lakini kama Waziri wa Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimewasilisha Bajeti za Wizara yangu hapa, nimewasilisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa miaka mitano mfululizo. Naam, labda niwaambie tu kwamba mimi huwa ninaamini kwamba kazi zote njema ni kazi za Mungu. Kwa hiyo, kazi njema tunawajibika kuzifanya kwa uwezo wetu wote na akili yetu yote kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa jina langu limeletwa mbele yenu kwa pendekezo la Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kazi hiyo ngumu. Kazi ya kumsaidia yeje kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kabla ya kukaa chini kwamba alipofariki Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, nililia sana hadharani, lakini pia hata binafsi huko nyumbani. Baadaye machozi yangu yalika kwa sababu Tanzania lazima iendelee kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima Taifa letu liendelee kuongozwa na Watanzania na kazi yetu kubwa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ni moja tu; jambo muhimu sana tunaloweza kumtenda haki Marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ni kuishi ndoto yake. Lazima tuibadilishe Tanzania, lazima tusimamie rasilimali za nchi yetu, lazima tuhakikishe viongozi wote wa umma wanaishi maadili ya kazi waliyotumwa na Watanzania. Mjomba alikuwa zamani, lazima tuyasimamie. Rasilimali za nchi, jicho lote hapo na nafasi ya Bunge katika hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, endapo Bunge hili litanithibitisha katika nafasi ambayo nimependekezwa, ahadi yangu ni hiyo. Ni lazima tumuenzi Hayati Rais wetu, lazima tutende wajibu wetu kwa Taifa hili. Nimesema mara kadhaa humu ndani, ningependa sana tutoke sasa kuwa *low middle income country*, twende kuwa *high income country* katika kipindi kifupi na inawezekana tukiamua kwa pamoja kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile bado nasubiri kama ndugu zangu hawa itawapendeza, naomba uniruhusu nikae. Nadhani nimejieleza, mimi mwenyewe huko nitokako, mimi ni mtoto wa maskini kabisa. Kwa hiyo, kama ni kiatu cha umaskini, najua kinavyouma. Kama mtanithibitisha, hilo nawaahidi kuendelea kusimamia haki za wanyonge wa Tanzania. Nitafanya kazi na viongozi wengine wa nchi yetu kwa uwezo wangu wote ambao Mwenyezi Mungu alinjalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango. Umenisaidia sana, maana sasa sitakuwa na sababu ya kusoma wasifu. Maana ulivyoeleza, umeeleza vizuri ambavyo msoma wasifu asingeweza kufikia viwango hivyo. Kwa hiyo, nakushukuru sana. Baadaye mwishoni tutakutaka tena useme kidogo, huko mbele kidogo baada ya zoezi hili kukaribia mwisho.

Mheshimiwa Makamu wa Rais kule kwenye chama alitamka...

Mh! Mheshimiwa Rais, mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais alitamka kwamba mtu ambaye naweza kufanya naye kazi kama msaidizi wangu bila mashaka ya aina yoyote ni Philip Isidor Mpango. Kwa hiyo, sisi Bunge kazi yetu kwa kweli ni rahisi na tutaifanya baada ya muda siyo mrefu kwa kuthibitisha kwenye karatasi ya kupiga kura.

Kwa hiyo, tutakuwa na wachangiaji kidogo, nami nitawa-pick kwa random. Tuanze na maprofesa wawili; wa kwanza Mheshimiwa Prof. Ndalichako na wa pili awe Profesa Palamagamba Kabudi. Dakika tano tano kuunga mkono hii hoja. Wengine mtafuata.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuunga mkono hoja ya pendekezo la kumpitisha Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa maono yake. Hakika Mheshimiwa Rais wetu ana maono. Ametazama katika Watanzania na ametuletea jina ambalo ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina bahati ya kumfahamu Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa sababu tumefanya naye kazi Chuo Kikuu kama alivyoeleza na alikuwa ni mchapakazi, alikuwa anasimamia maadili ya taaluma na wanafunzi wake walikuwa wanamfahamu. Mheshimiwa Dkt. Mpango alikuwa anaipenda sana kazi yake na alikuwa kama mlezi anajisikia faraja anapole ana kuleta wataalam wachumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Dkt. Mpango namfahamu kama Mcha Mungu. Mmemsikia hata katika mazungumzo yake, anasema, “kazi njema ni kazi ya Mungu.” Katika maisha yake yote Mheshimiwa Dkt. Mpango amekuwa anamtanguliza Mwenyezi Mungu na nina hakika ndiyo siri ya mafanikio yake. Ni mchapakazi, ni mtu ambaye anajituma, ni mtu ambaye ni mzalendo wa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango anaipenda sana nchi yake ya Tanzania. Katika kila nafasi ambayo amekuwa anapata, anaitumikia kwa dhati. Ni mtu ambaye ana uchungu na Taifa hili, ni mtu ambaye anatamani kuona Taifa hili linasonga mbele. Ndiyo maana tumemwona katika nafasi yake kama Waziri wa Fedha na Mipango namna ambavyo amefanya kazi hiyo kwa uadilifu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi ni watu wachache sana ambao wanadumu katika nafasi ya Waziri wa Fedha kwa miaka mitano na alikuwa amepewa mitano tena. Ni kutokana na uchapakazi wake, ni kutokana na uadilifu wake. Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye masuala ambayo mtu anataka kuchezea chezea raslimali za nchi hii, hana urafiki hata kidogo na huwa hacheki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nirudie kusema kwamba Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, hakika ana maono. Mimi sina mashaka kabisa kwamba Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango atakuwa msaidizi mzuri wa Mheshimiwa Rais wetu kutokana na sifa na hasa zaidi uzalendo wake na mapenzi ya dhati kwa Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu kwa kumpitishia msaidizi wake ambaye hakika ana vigezo vyote, anatosha, ana uwezo, ana utayari na ataenda kuwa kiungo kizuri katika kuhakikisha kwamba anasimamia raslimali za nchi hii na analinda maslahi ya Watanzania ambao ni wanyonge; anaendelea kukuza uchumi, kazi ambayo ameifanya kwa uadilifu katika kipindi chote ambacho amekuwa Waziri, ili nchi yetu iendelee kusonga mbele kwa sababu uchumi na mapato ya Serikali ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha kwamba mipango ambayo Serikali yetu imepanga inaweza ikatekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba sote tumtie nguvu mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kumpa Dkt. Phillip Mpango kura zote za ndiyo. Nitashangaa kama kuna kura itakayoharibika au kura yoyote ambayo itapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumsema Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango ambaye anatosha kabisa kwenye nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Profesa Ndalichako. Nakushukuru sana kwa maneno yako mazuri. Nami nithibitisha kwamba japo sijafanya utafiti wa ndani, lakini katika Afrika yetu hii *turnover* yaani mabadiliko ya Mawaziri wa Wizara ya Fedha huwa ni miaka miwili au mitatu, yaani lazima pawe pamebadilika, katika nchi karibu zote za Afrika, lakini Mheshimiwa Mpango huu ni mwaka wa sita. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Kabudi, atafuatiwa na Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, nami kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu kwa kuturuzuku

uhai na kutuwezesha leo kukutana katika Bunge hili Tukufu. Leo ndiyo siku aliyoifanya Bwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo katika kipindi hiki toka tupate msiba ameliongoza Taifa letu kwa umakini, utulivu wa hali ya juu sana na kuweza kutuvusha katika kipindi ambacho wengi walikuwa na wasiwasi na hofu. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumpongeze sana na kumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea jina la mtu anayestahili kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Phillip Isdor Mpango. Mimi binafsi leo ameacha kuwa pacha wangu, yeye sasa ni Makamu wa Rais. Kwa kauli hii, mimi na yeye watoto wa Salome sasa ukuta umewekwa, kimo chake kimepanda. Kimo chake kimepanda kama alivyosema yeye mwenyewe, mambo haya hupanga Mungu na Mungu akiyapanga hutimia. Kwa hiyo nimpongeze sana na nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua yeye kuwa msaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Phillip Isdor Mpango, anazo sifa zote. Alifiwa na baba yake akiwa mtoto mdogo, akatunzwa na mama yake na watoto waliotunzwa na mama zao, baba zao wakiwa hawapo, Mungu huwapandisha hapo! Mungu huwaona mayatima na wadhaifu na kuwapandisha katika viti vya wafalme; Zaburi ya 113; Mungu huwatoa watu jaani na kuwapandisha na kuwaketisha katika viti vya wafalme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo sala ya Hannah katika Biblia na hiyo ndiyo ilikuwa sala ya mama yake aliyemtunza yeye peke yake wakati baba yake alipokufa. Ndiyo maana naamini Mungu amemwangaza mama mwingine, Samia Suluhu Hassan kumteua yeye kuwa Makamu wa Rais. Hata hivyo, niwaambie Watanzania wenzangu, Mheshimiwa Phillip

Mpango amejaaliwa unyenyekevu usiokuwa wa kawaida, amejaaliwa upole lakini uthabiti. Mheshimiwa Phillip Mpango amejaaliwa kauli ambayo haibadiliki na kama kuna mtu ameyaishi maisha ya Zaburi ya 15 ya rafiki wa Mungu ni Mheshimiwa Phillip Isdor Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Taifa hili limemwandaa vizuro toka wakati wa Rais Mstaafu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na sasa. Kwa hiyo tuna Makamu wa Rais ambaye tukimpitisha na tumpitisha sote tayari ana uzoefu wa nafasi mbalimbali katika uongozi wa nchi yetu ikiwa ni pamoja na Wizara ngumu ya Fedha na Mipango katika kipindi hiki ambacho mmefanya mambo makubwa na sio kufanya mambo makubwa tu, kuingia katika uchumi wa kati. Watanzania tuna bahati sana kuwa na Taifa lenye umoja na kuwa na Katiba iliyotayarishwa na waasisi wa Taifa hili ambalo linaweza kutuvusha wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema tumpigie Mheshimiwa Phillip Isdor Mpango ambaye mimi namfahamu toka tukiwa Chuo Kikuu, tumpe kura zote. Kwa kufanya hivyo, moja tutakuwa tunampa nguvu yeye Mheshimiwa Phillip Isdor Mpango; pili, tutakuwa tunamheshimu Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan; na tatu, tutakuwa tunamuenzi Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Ni Mataifa machache sana ya Afrika yanaweza kupata msukosuko, dhoruba na yakavuka hivi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Katiba nzuri, madhubuti lakini pia imeonesha nchi hii ina watu wengi wenye uwezo na mmoja ni Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango. Furaha yang una shangwe yangu ni kubwa sana. Phillip na natumia neno Phillip kwa mara ya mwisho. Phillip, Mungu atembe naye. Mungu amlinde na amkamate na Mungu amwangazie nuru ya uso wake katika siku zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tumpe Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango kura zetu zote na kumthibitisha kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kwa sababu tunaelekea kwenye kupiga kura, naomba wanaofuata waende kifupi zaidi. Tuanze na Mheshimiwa Lukuvi, halafu tupate maneno ya Mungu kidogo kutoka kwa Askofu Gwajima. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, naanzia hapa kwa sababu nauona msingi wa hili zoezi tunalolianza leo, tunalolifanya leo. Nadhani kama sio malezi na kuaminiwa na Marehemu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli uaminifu aliouonesha Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi na uteuzi aliompa, pengine naamini haya leo yasingetokea.

Kwa hiyo ndiyo maana nasema naanzia hapo kwamba tuendeleo kumwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, mahali pema peponi. Hii inaonesha kwamba japo ametutoka lakini huko alipo na malaika wake bado anaiombea nchi hii ili iendeleo kuwa nzuri kama alivyoiacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya sio maajabu kwetu tu, lakini ni maajabu hata kwake. Alipofika hapa Mheshimiwa Dkt. Mpango tulikuwa tunazungumza naye, anazungumza mambo mengine tu hakuwa hata anajua. Bila shaka hata sisi wote tunajua kwamba hili hakuna mtu aliyelijua, lakini Mungu ana matumaini kwake. Ametuletea mtu mzuri ambaye kwa kweli wengi wetu na lazima tuseme ukweli, wengi wetu hatukutarajia. Ni Mwenyezi Mungu ametuletea mja wake ambaye wote sasa mioyo yetu inasema la! Kumbe Mheshimiwa Dkt. Mpango yupo na anatosha vizuri. Kwa hiyo tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuletea Mheshimiwa Dkt. Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema namfahamu Mheshimiwa Dkt. Mpango. Alipokuja kweli Awamu ya Nne, mimi nilikuwa *Chief Whip*, nilikuwa Waziri nahudumu kama Mheshimiwa Jenista, wakati ule ilikuwa Fedha na Mipango ni tofauti. Alikuwa ndiyo Katibu Mtendaji wa Tume, lakini kwa mamlaka aliyonayo alikuwa anaingia mpaka kwenye Baraza la Mawaziri, alikuwa mtu mzito! Hizi pilikapilika za kupanga kwamba sijui bajeti iende wapi zilikuwa zinaanza kwake. Hazikuwa zinaanzia Wizara ya Fedha, zilikuwa zinaanzia huku maana yake ndiye aliyetayarisha Mpango na ndiye anajua kumega sungura gani aende mahali gani. Kwa hiyo nami nikamfahamu hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mwenyewe na walivyosema wenzangu wengine kwa kweli kama binadamu umelelewa vizuri na una mapenzi mema, kugombana na Mheshimiwa Dkt. Mpango unataka mwenyewe. Yaani kugombana kwa maneno au kwa vitendo unataka mwenyewe kwa sababu mzee huyu Mheshimiwa Dkt. Mpango hutamwona namna alivyokasirika, amechukia sana hutamjua, hawezi kukufokea, hawezi kukutukana na mara zote nilikuwa natoka pale Magogoni kwenda kwake huyu utamkuta hata saa mbili usiku yuko ofisini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimesimama hapa kwa kweli kuunga mkono sana jina hili la Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi hii ambayo Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama Samia ameamua kumpa leo. Ni mtu anayefaa, anayestahili na ana uwezo wa kufanya haya ambayo anapewa leo kwa sifa ambazo mmezisikia lakini kwa namna alivyo Mheshimiwa Dkt. Mpango. Ni kweli Dkt Mpango ni mcha Mungu sana, mkitaka kujua hayo mtembeleeni kwake Chanika kule ndiyo mtajua, nyumbani kwake. Ukiingia tu hata ishara ya nyumba yake utajua hii ni nyumba ya mcha Mungu; maana nyumba za wacha Mungu unazona. Hata kabla hujaingia kumsalimia ukifika nyumba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango, alama zilizopo utajua huyu ni mcha Mungu. Ni mcha Mungu sio wa kuigiza, ni kweli na ndiyo maana mmemsikia hata alipopata matatizo juzi, hata alivyokuwa anasema, alikuwa anamtanguliza Mungu zaidi.

Kila mara Mheshimiwa Dkt. Mpango amekuwa akimtanguliza Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono na utashi wa kumwona Dkt. Mpango na kumpa kazi hii. Nasema hakukosea, Mungu amemjaalia, amempata mtu shujaa, mtu sahihi kabisa kwa kazi hii na nadhani kwa niaba ya wenzangu wote tuliomo kwenye jumba hili tumhakikishie kwamba tutampa ushirikiano wa kutosha huyu Makamu wa Rais ambaye anakwenda kupata kura zote leo. Ni mwenzetu kwa miaka sita, ametufanyia mengi kama binafsi, lakini ameshiriki vizuri sana katika kutafuta ushindi wa nchi hii kwa kusimamia fedha ambayo ndiyo ilikuwa nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Ametafuta, amezipanga na amezisimamia na utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, tulikuwa tunataniana hapa sana, lakini kwa sababu hatutamwona, maana hatutamwona, Makamu wa Rais unamwona wapi? Hatutamwona. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ambariki, tunajua ataendelea kuwa hivyo hivyo, sisi wenzake tupo, tunamwomba na tunamtakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu amjaalie aendeleo kuwa Mheshimiwa Dkt.Mpango huyo tunayemjua sisi. Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima atafuatiwa na Mheshimiwa Maalim Musa Hassan Musa.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa dakika hizi chache za kusema maneno machache kuhusiana na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mteule. Mimi tu niseme kwamba, jicho lililomuona Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mteule ni kubwa kuliko aliyeteuliwa.

Jicho lililofanikiwa kupita kati ya Watanzania zaidi ya milioni 60 na kumpata mtu mmoja anayeitwa Phillip Mpango, hilo jicho la mama Samia Hassan Suluhu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kubwa kuliko jicho lolote lile. Tumezoea kuwanukuu watu wengine, tunanukuu wanafalsafa wa karne mbalimbali duniani lakini leo nataka nimnukuu Mtanzania mmoja anaitwa Piere *Liquid* aliyesema, niseme mama Samia Hassan Suluhu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni *konki fire*. Tena niongezee mama Samia Hassan Suluhu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yuko mwinguni, yuko juu sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya yeye kuwa *konki fire* na yuko juu sana ndiyo maana kwa jicho lake amefanikiwa kumpata Phillip Mpango kati ya Watanzania wote zaidi ya milioni 50 mpaka 60 ili awe Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mteule. Kwa habari ya Phillip Mpango mwenyewe, mimi wakati naingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara ya kwanza kwenye Mkutano wa kwanza nilikuwa na tatizo kubwa sana kwenye Jimbo langu kule Kawe. Kulikuwa na Bandari moja ya majahazi yanayotoka Zanzibar kuja Mbweni ilikuwa imeshindwa kufunguliwa kwa miaka mingi. Wananchi wa Kawe walikuwa wanaumizwa, wanapata matatizo, Masheikh wangu, Maustadh wangu wa Mbweni pamoja na maeneo yote walikuwa wanashindwa kuleta mafuta kutoka Zanzibar. Nilipofika hapa nilizungumza na Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango kama Waziri wa Fedha, akaniambia Mheshimiwa Gwajima, ndani ya wiki mbili itafunguliwa na leo imefunguliwa na wananchi wangu wanaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango ni Mpango kweli kweli. Kwa maneno machache, nimwambie tu Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango, Biblia inasema maneno haya:

*Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala hakukaa katika Baraza la wenye mizaha, bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo na sheria hiyo huitafakari*

*mchana na usiku. Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya mto unaozaa matunda yake hata wakati wa joto na kila alitendalo litafanikiwa. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimtakie mafanikio, yeye atakuwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kwanza mwenye mafanikio kuliko wote waliomtangulia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Gwajima. Mheshimiwa Musa atafuatiwa na Fakharia Shomari halafu tuendelee na zoezi linalofuata.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, *Asalaam Aleykum Warahmatullah Wabarakatuh.*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nikazungumza na kuunga mkono Azimio ambalo limeletwa mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wa Taala* kwa kutufaraji baada ya msiba mkubwa ambao umetufika. *Inshallah* Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho yake Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna huzuni, lakini nataka niwatoe Wabunge huzuni kwani Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wa Taala* anasema: "*Kullu nafsin zaikatul maut*", kwamba kila nafsi, kila mmoja wetu sisi ataonja tu mauti kwani mauti ni mlango kila mmoja wetu atapita. Baada ya kusema hivyo nawaombeni turudi kwa Mwenyezi Mungu na tumshukuru anapoondosha moja huleta lingine.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Mimi namfahamu sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan nilifanya naye kazi kwa ukaribu sana na kauli yake aliyoitoa kwamba aliyesimama hapa ni Rais mwenye maumbile ya kike haikuwa mara ya kwanza. Kuna mfanyakazi mmoja akifanya kazi chini yake aliwahi kugeuka baada ya kuona sura na umbile lake lakini alimwambia papo hapo kwamba

kama mwanamke watoto wangu nitanyonyesha siyo mwanamke kwa wewe, kwa hiyo, ile Wizara ilikuwa na heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwa ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango. Mheshimiwa Mpango ni muumini na nikisema muumini hapa sitaki kusema kwamba ni *Christian* ama ni Muislamu. Yeye ni muumini kwa maana ya kwamba anaamini Mwenyezi Mungu kwamba ndiye mwongofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitabu vyetu vimesema: *“Yafa-Allahu ladhi amalu minkum waladh uta-al-maddarajjat”*. Hupatwi na mshangao, atamuinua Mwenyezi Mungu yule aliyemuamini kisha atampandisha daraja, hii ni haki yake. Hii ni haki yake ya msingi na mtu anafanywa hivi kwa sababu kwanza, muumini, ana uwezo na anajua anachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mipango ni matumizi kwamba tusingefika hatua hii leo kama hatuna kiungo cha mpango. Nawaombeni Waheshimiwa Wabunge tuthibitishie maneno aliyosema Musa na aliyoyasema Mwenyezi Mungu kwa kumthibitisha Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kura zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, kuna kazi inafuata mimi nimalize tu kwa kumuomba dua, Mwenyezi Mungu amuwezeshe afanye kazi yake kwa uadilifu kama Taifa ambavyo linamtegemea. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maalim Mussa. Mheshimiwa Kamishna Fakharia. *(Makofi)*

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu maana Mwenyezi Mungu ndiyo muweza wa yote. Leo nampongeza Mheshimiwa Mama Samia kwa jina alilotuletea na *inshallah* litapita kwa uwezo wake *Allah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mpango namfahamu miaka sita iliyopita. Mheshimiwa Dkt. Mpango ni Waziri wa Fedha na Mipango. Wakati yuko Waziri wa Fedha anapowasilisha kwenye Bunge anapata maelezo ya kila aina kutoka kwa Wabunge, lakini anatulia, anakuwa mwangalifu, anasikiliza, kisha mwisho anatoa suluhisho na sote Wabunge tunalikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namjua Mheshimiwa Dkt. Mpango ni mtulivu, msikivu na ni mpole, sasa hii nafasi aliyoipata najua ataitendea kheri na tutapata mafanikio kutokana na jina lake la mipango. Nafasi anayoiendea inataka shughuli za kutumikia mipango na yeye ni Mchumi na pale anapokwenda atatusaidia wanyonge kama ilivyokuwa mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kwetu tuna usemi tunasema mpewa hapokonyeki aliyepewa kapewa. Mheshimiwa Dkt. Mpango hili ni mwenyewe *Allah*, mama katia mkono wake, lakini mwenyewe *Allah* alikuwa tayari amekwisha kuteua. Kwa uwezo wa *Allah* utafanya kazi zako vizuri na *inshallah* utaivusha Tanzania na utamsaidia Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuivusha Tanzania, kuwasaidia wanyonge na miradi yote iliyokuwa imeanzishwa kumalizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua wenzangu wamezungumza mengi na yameshasemwa mengi ya kumsifu lakini nawaomba Wabunge wenzangu kutoka Zanzibar na Tanzania Bara, sote ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa umoja wetu tuunge mkono na Mwenyezi Mungu atamuwezesha Mheshimiwa Dkt. Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kabla sijamkaribisha Katibu ili tuendelee kwa sababu yale Maazimio yanayokuja watakaopata nafasi ya kuchangia bado wanaweza wakalichangia hili pia, naangalia makundi mbalimbali, kundi

gani nimelisahau? Nafikiri kundi la darasa la saba sijalipa nafasi, Mheshimiwa Musukuma tafadhali. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kukumbuka kundi hili muhimu ambalo mimi ni kiongozi wake humu Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutuletea jina la Dkt. Mpango. Naomba niseme ni kweli Mheshimiwa Mama Samia atatuvusha na tuna imani naye kubwa sana na dalili ya mvua ni mawingu. Nimekaa humu Bungeni, ukiondoa huko nje wakati nikiwa Mwenyekiti na vyeo vingine leo mwaka wa sita, jina lililoko mbele yetu kusema na ukweli kabisa Mungu shahidi ni Waziri ambaye hana makundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sio makundi na huu ni mfano kwa Mawaziri wengine, ni Waziri ambaye anamsikiliza kila mtu na anamchukulia kama Waziri mwenzie. Mimi binafsi Mheshimiwa Dkt. Mpango, kaka yangu, ni Mawaziri wachache sana ukimuomba lifti anakupa; nilimsimamisha Dar-es-Salaam na akanipa lifti. Kuna Mawaziri wengine humu mnakuwa kama hamjuani akishaingia kwenye V8. Nadhani huu ni mfano mzuri kwa wale mnaotaka kuendelea mbele, igeni mfano wa Mheshimiwa Dkt. Mpango. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mpango hakuna mtu atakayemnyima kura. Mimi binafsi kama Mbunge kuna kauli nimezisikia, leo nimeisikia hapa ni mara ya tatu, mara ya kwanza aliwahi kuzungumza kwenye hotuba yake kwamba yeye ni mtoto wa masikini. Mara ya pili alipokuwa anaapishwa juzi kule Chamwino alisema wewe umegombea jimbo ameona masikini wanavyoishi na leo mara ya tatu amezungumza ametoka familia masikini. Sisi humu ndani tunaongoza familia masikini asilimia 95. Kwa hiyo, nina imani unaenda kuwa mshauri namba moja wa Mheshimiwa Rais, mueleze shida zilizoko vijijini. Mueleze umasikini wa Watanzania ulivyo muendeleo kushauriana ili muweze kutubadilishia maisha yetu huko Usukumani na sehemu nyingine. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, lakini lingine Mheshimiwa Dkt. Mpango, leo tunakuita hili jina samahani kama alivyosema Mjumbe kwa mara ya mwisho, acha tukuite kabisa ili tumalize hamu. Mheshimiwa Mpango amekuwa humu ndani ametusaidia kama Taifa, tumepanda kutoka uchumi wa chini mpaka uchumi wa kati, lakini kumekuwa na kero mbalimbali mfano ni madini. Tullilia na Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na Mheshimiwa Rais mkatuita, mkatusikiliza, mkarekebisha sheria, sasa hivi mnakusanya kodi vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mpango najua alikuwa *TRA* sasa amepewa rungu kubwa, matatizo ya *TRA* na wafanyabiashara anayafahamu.

Mheshimiwa Dkt. Mpango hakuna Mtanzania anayewaomba wewe Makamu wa Rais na Rais mkwame, lakini kuna vitu ambavyo vinafanya wafanyabiashara na Serikali kuwa maadui, Mheshimiwa Mpango ameanzia huku chini na leo anaenda kuwa juu, namwomba na nilimwomba Mheshimiwa Rais, Hayati Magufuli, akakae na Mheshimiwa Rais awaite wafanyabiashara kwa makundi wamueleze wapi wanakwamishwa na *TRA*. Hakuna mtu anataka kukwepa kodi, tutakulipa pesa Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Mama Samia mara tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tupigeni kura zote za ndiyo, hata ukituhoji kwa mdomo tupo tayari. Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, Makamu wa Rais mtarajiwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani Mwenyekiti wa *PAC* angeweza kusema kidogo pia, tunakaribia kuhitimisha.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nikianza kumsifia Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango sitamaliza leo, lakini kwa kifupi kwa vile tunajua muda umesogea niseme, hata mimi mwenyewe nilimwambia na anajua hilo kwamba sijaona Waziri aliyekuwa mnyenyekevu kama yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza tukimuita hata kwenye Kamati ya PAC anashuka kuliko unavyotegemea. Hata wakati nikipata utata nikienda ofisini kwake kumuuliza hili likoje, hasa wakati tulipopata shida ya ile 1.5 trillion alinieleza ukweli akasema kuna matatizo ya mfumo tunafanyia kazi na tutaufanyia kazi tuurekebishe. Kwa hiyo, mimi niseme ni mtu muaminifu, mwenye upendo na anajua kushuka, hapendi makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sikujua ni yatima, yatima ni wale ambao hawana baba si ndio, lakini aliyelelewa na mwanamke mnaona alivyo shujaa, wanawake wanajua kulelea watoto wao. Kwa hiyo, nasema hata huyo mama aliyemzaa aliyemfikisha hapo Mungu azidi kumbariki. Tunazidi kumuomba akaangalie yeye anajua tangu akiwa Hazina na akiwa na Kamati yetu yale matatizo tuliyokuwa tunayapata na zile areas ambazo tukipeleka Serikalini zilikuwa hazifanyiwi kazi, tunaomba amsaidie Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ili waweze kutatua matatizo ambayo fedha ya umma ilikuwa inapotea bila kujulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana maana najua kuna mahali ambapo tutapeleka kilio chetu cha PAC kisikike. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. kwa sababu ya muda nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kidogo, kama nilivyosema tutaendelea kulisema hili kwenye session inayofuata. Katibu wa Bunge, tafadhali.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe utaratibu wa kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais. Kwanza, tunaanza na hatua ya kuhesabu idadi ya Wabunge walioko ndani ya ukumbi. Bahati nzuri hilo limeshafanyika, tunayo idadi ya Wabunge 356.

Mheshimiwa Spika, lakini kinachofuatia ni kugawa karatasi za kupigia kura kwa Wabunge wote. Endapo utaruhusu zoezi hilo linaweza likaanza kuendelea, maana ni zoezi la pili. Hatua ya tatu itakuwa ni ya kupiga kura, Wabunge

wakishapiga kura karatasi zitakusanywa na zitawekwa kwenye masanduku ya kura.

Mheshimiwa Spika, baada ya pale unaweza kuteuwa wawakilishi wa kusimamia zoezi la kuhesabu kura. Mwisho matokeo yatatangazwa, ikiwa mgombea atakuwa amepata zaidi ya asilimia 50 atakuwa amethibitishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu. Sasa Waheshimiwa Wabunge muanze kupokea karatasi za kupiga kura, tufanye chap-chap ili tuokoe muda na wale wa ma-*box* na wenyewe wajiandae kuanza kukusanya kura zilizopigwa ni Ndiyo au Hapana. Tunaomba busara kubwa katika jambo hili.

*(Hapa karatasi za kura ziligawiwa kwa Wabunge)*

*(Hapa Wabunge walipiga kura kuthibitisha jina la Makamu wa Rais)*

**SPIKA:** Wale wa ma-*box* waanze kupita pia.

Naomba wafuatao wafike hapa mbele; Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mwenyekiti wa Katiba na Sheria, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Mwenyekiti wa LAAC.

**WABUNGE FULANI:** Mwenyekiti wa LAAC hayupo.

**SPIKA:** LAAC hayupo. Wenyeviti hawa nawaomba, PIC, Kilimo, Ardhi na Katiba tusimame hapo mbele. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma simuoni?

Tufanye haraka na tuwe na utulivu Waheshimiwa Wabunge, tusitoke-toke zoezi hili ni muhimu sana. Wakusanyaji fanyeni haraka. Tufanye haraka Waheshimiwa Wabunge, tuokoe muda. Tunaomba utulivu na ukimya. Kila mtu akae mahali pake kwenye kiti chake. Anzeni kusogeza masanduku

mbele. Naomba mnaotembea-tembea kila mtu akae kwa utulivu mahali pake.

Ahsante sana masanduku ya kura ndiyo hayo. Nimewateuwa Wenyeviti wetu hawa wa Kamati watakuwa wasimamizi wakishirikiana na Katibu wa Bunge. Sasa nawaomba mwende, lakini tunaomba mrudi hapa haraka sana, zihesabiwe kwa *speed* kubwa sana, ili tuokoe muda. Pelekeni masanduku tafadhali, hizo kura zihesabiwe haraka sana, naomba timu ya kuhesabu ihesabu haraka sana.

Naomba kila mtu akae kwa utulivu mahali pake, mnaotembea tembea, eee dakika moja tu! dakika moja tu! unaenda kuhesabia nje.

Ahsante sana, masanduku ya kura ndiyo hayo, nimewateuwa wenyeviti wetu wa Kamati, hawa watatu watakuwa wasimamizi wakishirikiana na makatibu wa Bunge. Sasa naomba muende, lakini tunaomba mrudi hapa haraka sana, zihesabiwe kwa *speed* kubwa sana ili tuokoe muda. Haya ingizeni, rudini nyuma, pelekeni masanduku, hizo kura zihesabiwe haraka sana sana, naomba timu ya kuhesabu ihesabu haraka sana.

Tafadhali peaneni hizo karatasi haraka zikahesabiwe. Ahsante sana! Kwa mara nyingine naomba kila mtu akae mahali pake, yeyote yule aliyesimama naomba akae. Nitaanza kuwataja majina wale wanaomangamanga. Kule nyuma kabisa nawaona mliosimama, naomba mkae mahali penu kwa utulivu.

Sasa Waheshimiwa Wabunge muda si mrefu nitatoa taarifa ya Spika ambayo itaendana na kutoa matangazo, tangazo la jinsi ambavyo kura zimeenda baada ya kuwa zoezi la kuhesabu kura limekamilika, na matokeo haya yatatuonyesha basi kama tumepata zaidi ya kura kwa asilimia hamsini ya Wabunge wote basi itakuwa tumetekeleza wajibu wetu kikatiba. Sasa wakati Katibu wa Bunge na timu yake wanahesabu hizi kura nitumie nafasi hii kumpa tena Dkt. Mpango nafasi ya kuzungumza nasi na kuwaaga wapiga

kura wake wa Buhigwe. Ni vizuri ikawa baada ya matokeo, lakini, maana baada ya matokeo anakuwa Makamu, akishakuwa Makamu *automatically* sio Mbunge, sasa ataongeeje na Bunge, ndipo napatafuta hapo, nafikiri tupo pamoja ee! Hapo ndipo ninapotatafuta, ndiyo maana nikishatangaza tu basi hawezi kuongea tena, ndo maana nikafikiri wakati huu ni mzuri, akazungumza nasi, nadhani ni sawa si ndiyo Waheshimiwa naam! niko tayari kupokea ushauri. Mheshimiwa *Chief Weep!*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, tunadhani nakuamini kwamba, fursa aliyoipata Mheshimiwa Makamu wa Rais mtarajiwa, kwa sababu ndio tunaendelea na zoezi lenyewe aliyoipata, ya kusema ameipata pia katika mazingira haya haya ambayo unayazungumza.

Sasa, kwa kuwa tunapomaliza kumthibitisha bado taratibu za kikatiba ndipo zitakuja tena huko mbele, ingependeza sana ule umoja wetu humu ndani na zile kura zote tutakazozimwaga hapa leo zikishakuwa zimewekwa hapa hadharani, basi ndipo ingekuwa ni nafasi nzuri kwa Mheshimiwa Mpango sasa kusimama na kuyasema yale yote na kupata fursa sasa ya wale wana Buhigwe kuona kwamba walichagua chombo kwelikweli hawakufanya makosa na wameungwa mkono na Watanzania wote kwa sababu hapa Wabunge wote wanawawakilisha Watanzania wote kupitia kwenye majimbo yao ya uchaguzi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwahiyo nilikuwa natoa ushauri huo, kwamba ikikupendeza aseme baada ya yale matokeo yakiwa yameshatolewa hapa hadharani.

**SPIKA:** Ngoja niangalie vitabu vyangu tena unajua Katiba iko *very tricky* kidogo. Ni Ibara ile ya 71, haya mnisikilize sasa, twende pamoja, tunajaribu kutumia huu muda, wakati wanahesabu na sisi tunajifunza kidogo Katiba yetu, natumaini wale wenye *tabulate* mme-download, hii kitu huwa mnayo kwenye *tabulate* zenu, na wale wenye vitabu hebu twende pamoja. Ibara ya 71,

71.-(1) Mbunge atakoma kuwa Mbunge na ataacha kiti chake katika Bunge litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo: –

Sasa yale (a), (b), (c) usijali, kinachotuhusu hapa ni (e);

(e) Ikiwa Mbunge atachaguliwa au anateuliwa kuwa Makamu wa Rais.

Nikitaja matokeo tu hapa atakuwa tayari ni Makamu wa Rais mteule na akishakuwa Makamu wa Rais Mteule hataweza kuongea hapa kwa sababu *automatically* anafutika kuwa Mbunge. *Chief Weep* ndiyo maana nikawa nahangaika kwamba ni kipindi kipi hasa, maana si unajua mambo ya Katiba wako wajuaji huko wataanza Spika amevunja Katiba!. Nitengue Katiba eee! (*Kicheko*).

Kwa vile sina mashaka yeyote sasa, kama meza kuhusu matokeo yetu, ambacho bado ni kutaja tu takwimu lakini sina mashaka yeyote, nitazitaja baada ya muda si mrefu kwa kweli nimpe nafasi Mheshimiwa Dkt. Mpango aseme chochote, halafu nitataja matokeo, halafu tutaendelea, lakini matokeo yangu hayana mashaka yeyote, naomba Mheshimiwa Mpango utumie fursa hii. Ni vizuri ukaja hapa karibu sana. (*vigelegele/makofi*).

Ahsante, naomba mkae, Mheshimiwa Mpango karibu sana.

**MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO - MAKAMU WA RAIS MTEULE:** Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kwa ruhusa yako niseme walau kwa mara ya mwisho. Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wote kwa mara nyingine tena; naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Siku ya leo sina maelezo nayo lakini naomba tu muendeleo kunisaidia kumshukuru Mungu pamoja nami. (*Makofi*)

Kwa miaka mingi nimekuwa katika nyadhifa mbalimbali ambazo nimetumikia katika nchi yetu. Nimekuwa nasumbuka sana na umaskini, na kwa sababu ile ile niliyowaambieni, kwamba nimevaa kiatu cha umasikini tangu utoto wangu, na kwa hiyo hata nilipokuwa shuleni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nilijielekeza zaidi kwenye Uchumi wa Maendeleo (*Development Economics*). Hii ni kwa sababu nilitaka nione ni namna gani tunaweza tukaondoka kwenye huu umaskini. Kwa hiyo inapofika siku hii ambayo Waheshimiwa Wabunge mtanithibitisha katika nafasi ambayo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amependekeza ninaamini kabisa kwamba kazi yangu ya kwanza ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu ni kuhakikisha kwamba ndoto ya Watanzania inatimia. (*Makofi*).

Wote ni mashahidi, kwanza nataka kuwakumbusha matukio mawili wakati tunamuombeza Rais wetu Kipenzi Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, pale uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam wote tuliwashuhudia wananchi wanyonge kabisa wakiruka *fence* kwenda kumsindikiza kipenzi chao wakati mwili wake unakaribia kupakiwa kwenye ndege ili kuja hapa Dodoma.

Tukio la pili, mliliona hapa Dodoma jinsi ambavyo bodaboda waliamua kuchukua kazi ya polisi wa barabarani, wakamsindikiza kipenzi chao. Kwangu mimi matukio hayo mawili ni ishara wazi ya wanyonge kutuambia kwamba kazi zote alizoacha kiongozi wetu, zisipokwenda vizuri hatuna namna. Sijui kama mliwasikia walivyokuwa wanaimba; walikuwa wanaimba jeshi! jeshi! jeshi! Kwa hiyo tunaowajibu wa kuhakikisha kwamba, ndoto za wanyonge hawa watanzania, miradi wanataka *SGR* yao ikamilike, wanataka bwawa la Mwalimu Nyerere likamilike, wanataka barabara na hususani za vijijini zikamilike, wanataka huduma za Afya ziwe bora zaidi, wanataka maji, wanataka usalama ili waendeleo kufanya shughuli zao. (*makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawataki rushwa. Ninachotaka kusema ni kwamba kama Bunge la Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania litanithibisha katika nafasi iliyopendekezwa na Mheshimiwa Rais wetu, haya ndiyo mambo nitakayokwenda kumsaidia ili nchi yetu isonge mbele wananchi hawa kiu yao ya maendeleo iweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, Bunge ni chombo muhimu sana. Katika hii miaka mitano na kidogo nimejifunza sana.

Mheshimiwa Spika na nataka nikushukuru wewe mwenyewe binafsi, mtangulizi wako yule kabla ya huyu alikuwa Spika wa viwango, sasa sijui wewe nikuiteje, nadhani wewe ni Spika wa Kidijitali, umekuwa ni kiongozi mahiri sana wa Bunge hili na nimejifunza mengi kutoka kwako. Ikifika msimamo ni msimamo na hilo nimejifunza sana. Kwa mambo ya msingi ni lazima kuyasimamia. Vilevile umeendesha Bunge hili likiwa na pande zote mbili, kwa kweli umetulea wengi tumejifunza sana kwako. Uongozi maana yake ni nini? Mungu akubariki sana sana. *(Makofi)*

Lakini pia Mheshimiwa Naibu Spika, naye amekuwa mahiri sana na mwanamama shupavu. Nadhani baada ya Mheshimiwa Rais wetu ambaye ni mwanamama Shupavu sasa ameongezeka na Tulia; kuna watu wana wasiwasi juu ya uwezo wa akinamama?

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nitumie nafasi hii kumshukuru kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina namna nyingi za kukueleza. Katika Hotuba ya Bajeti mojawapo nilisema sikutarajia kwamba Waziri Mkuu Kiongozi wangu kila tulipokuwa tukikaa kwenye vikao vyetu anatuita sisi Mawaziri anasema Mawaziri wenzangu. *(Makofi)*,

Ahsante sana kwa unyenyekevu huo, na mimi Waheshimiwa Wabunge hawa wakinithibitisha nitajitahidi kadiri ninavyoweza kujifunza unyenyekevu kutoka kwako, lakini usimamizi mahiri wa shughuli za umma ambazo tunaopewa. Najua umekuwa hulali, sisi wasaidizi wako tulikuwa tunafahamu unavyohangaika kumsaidia Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais wakati ule, pia kufanya kazi zile ambazo wakubwa hawa walikuwa wameelemewa



na wanakutuma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana umekuwa ni darasa kubwa sana kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema niseme pia, maana pengine sitapata kweli hii fursa, *Chief Whip* amefanya kazi nzuri sana, Uratibu wa Mawaziri Bungeni kwa kweli ulipata mtu sahihi na kama vile ni ajabu tena ni mwanamama mwingine. Ahsante sana amekuwa msaada mkubwa kwangu, kuratibu kazi zangu pale Wizara ya Fedha na shughuli zote za Bunge na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niatumie nafasi hii, kuwashukuru sana viongozi wote wa Kamati za Bunge, yaani hata katika kipindi kifupi cha Bunge hili, nimeshuhudia uhusiano mzuri sana kati ya Wizara yangu na mimi binafsi, lakini na shughuli za Kamati zote. Ahsanteni sana kwa sababu hiyo ndio inavyopasa, maslahi ya Tanzania kwanza, kwa hiyo nawashukuru sana na hususani Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran lakini pia Makamu wake, Mheshimiwa Omari Kibua na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti bila kubagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jana tu tulikuwa tunaendelea na shughuli na hata mchana huu najua bado tuna kazi, sasa sijui itakuwaje mkinithibitisha, lakini hakuna litakalokwama kazi ya nchi yetu itaendelea kufanyika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena, Bunge hili ni chombo muhimu sana, kwanza kuleta mawazo ya wananchi wetu na hasa hao walio wanyonge hapa, kwenye mhimili huu ili yaweze kufanyiwa kazi. Bunge hili lina kazi kubwa ya kuishauri Serikali, naendelea kuwasihahi Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kutunga sheria, wazisimamie ambazo ziko kwenye Katiba lakini hizi ni kazi wamepewa na Mwenyezi Mungu, wazifanye kwa uaminifu kabisa. Mkinithibitisha katika nafasi hiyo mpya na Mwenyezi Mungu anisaidie niishi maneno yangu, yale ambayo yatakuwa yameshauriwa na Bunge kuja Serikalini, nitamsaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba yanasimamiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaomba jambo moja tu, mimi ni binadamu, pamoja na kuwa mmesema maneno mengi mazuri juu yangu mengine hamkusema. Nataka nitumie nafasi hii, pale ambapo nilimkwaza mtu yeyote, Mheshimiwa Mbunge yeyote, humu ndani au nje katika nafasi yangu ya Uwaziri wa Fedha na Mipango, nawaomba mnisamehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitatoka kabisa na lalamiko lolote juu ya Mbunge yeyote. Najua wamesema mimi ni mpole, mcha Mungu, najitahidi, najitahidi kumcha Mwenyezi Mungu, kwa sababu bila hiyo najua si chochote, lakini kuna maeneo naomba muwe mnasema ukweli, mimi sio mpole kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mambo ya hovyohovyoyo ya matumizi ya fedha za umma, hapana mimi sio mpole. Kwa watu wanaokula rushwa, mimi sio mpole na kwa hilo naomba mnisamehe. Pale ambapo itabidi kusimamia kazi za umma kwa ajili maendeleo ya Tanzania, nawaambieni ukweli nitamsaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba tunakwenda sawasawa. Mniombe kwa Mwenyezi Mungu. Naomba sana, kila mtu kwa dini yake. Dhamana hii ni kubwa, umaskini katika nchi yetu ni mkubwa sana bado tuna zaidi ya watu karibu milioni 14 ambao wanaishi chini ya kiwango cha umaskini, ni kiwango hakikubaliki. Kwa hiyo, wale ambao tutakuwa sijui wanadokoa rasilimali za umma hao ni halali yangu, nitamsaidia Mheshimiwa Rais. Kwa niaba ya Watanzania wanyonge. Nisaidie sana Mwenyezi Mungu aniongoze, nisiwe na chuki na mtu yeyote na wala nisionee mtu yeyote katika dhamana hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napata ugumu kidogo unaponiambia kwamba sasa pengine wakinithibitisha sitarudi tena hapa na nilizoea, nina marafiki wengi, nina kaka zangu, nina pacha wangu, sasa anataka kuukana leo, nina shemeji zangu, nina dada zangu, napata tabu kidogo, lakini kwa faida ya nchi yetu na kama ndio utaratibu, basi itakuwa hivyo lakini nitabaki kuwa mwaminifu na karibu sana na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kuzungumza na wananchi ambao wako mbali kidogo na hapa tulipo. Ni ndugu zangu, ni wananchi wa Buhigwe ambao walinichagua kwa kura 77% ili niwe mwakilishi wao hapa Bungeni. Kwanza naendelea kuwashukuru kwa heshima waliyonipa, kabla ya hapo nilikuwa nimeamua kwamba nikafanye kazi nyingine na nilisema hivyo kwa kiasi fulani lakini niliwaruhusu kwamba bado nina nguvu ya kufanya kazi. Nawashukuru na bado Buhigwe ndio kwetu nitaendelea kuwa karibu nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaombea na naamini kabisa, watapata mwakilishi mwingine mahiri kwa ajili ya kusemea, matakwa yao, shida zao katika Bunge hili. Hata hivyo, pia, Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma walioko humu, naamini kabisa kwamba bado wataendelea nao kuwa sauti ya wananchi wale wa Buhigwe na Kigoma kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu awabariki sana nitakapopata nafasi nitarudi nyumbani, nyumbani ni nyumbani, nitarudi kuwasalimia na tutaona tunavyoendelea kwenda kutetea maslahi ya wananchi wale na Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa nimekosa fadhila, nitakuwa nimekosa fadhila kabisa, mwanzoni nimemshukuru mama yetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kufikiria kwamba Philip Mpango anaweza kumsaidia kubeba jukumu hili la Taifa letu.

Pia niliwashukuru chama changu ndivyo nilivyosema, kwa hiyo, kwa naomba kwa namna ya pekee ni ushukuru sana uongozi wa chama chetu ambao umethibitisha pendekezo la Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwamba niweze kumsaidia kazi na wakaridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaendelea kuwa mwanachama mwaminifu wa Chama cha Mapinduzi mpaka nitakapokufa sio kwa sababu tu ya nafasi ambayo nimependekezwa, mpaka nitakapokufa nitaendelea kutetea na kuishi nidhamu,

maadili na ahadi za mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niondoke hapa lakini *I will miss the House*. Mjadala mahiri, mjadala ambao unalenga kusukuma maendeleo ya Mama Tanzania. Hata wale wachache ambao hawako, hawana imani ya chama chetu najua wengine walichopoka tu kama mdogo wangu mmoja naona ananiangalia pale, nitapenda sana mkirudi tukawa pamoja. Hata hivyo, kukaa kwenu upande mwingine mjielekeze zaidi nawasihi sana, mjielekeze kwenye *priorities* za Mama Tanzania, kile ambacho ni maslahi ya Mama Tanzania, mkitetee bila woga bila kuangalia kwamba basi hiki kwasababu kimetoka upande mwingine basi mnakikataa. Katika vitu vilinimumiza sana ni pale ambapo mlikuwa mnaikataa Bajeti ya Serikali, bajeti ambayo inakwenda kuhangaika na maisha ya hayo watanzania. Mliangalie sana hilo sitawasukuma sana, lakini mliangalie sana, maslahi ya Mama Tanzania kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu akubariki sana, Katibu wa Bunge, bado nitaendelea kukuita mdogo wangu na watendaji wenzako wa Bunge, walioko hapa na ambao wako huko wakiendelea kulihudumia Bunge. Ahsanteni sana, ahsanteni sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wote ahsanteni, ahsanteni, ahsanteni. Mungu libariki Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mungu ibariki nchi yetu nzuri ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya upendeleo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nakuomba Mheshimiwa Dkt. Mpango uendelee kusimama hapo hapo.

Ahsante sana kwa hotuba nzuri sana. Tunakushukuru sana, umesema maneno makubwa na mazuri kwetu sote na

kwa nchi yetu. Nasi tunakutakia kila la kheri pia, tutakupa kila aina ya ushirikiano Mungu akipenda.

### **MATOKEO YA KURA ZA KUTHIBITISHA JINA LA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SPIKA:** Matokeo ya kura za kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, jumla ya kura zilizopigwa ziliongezeka kwa sababu Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiingia, mwisho wakawa Wabunge tuko humu ndani ni 363. Hakuna kura iliyoharibika hata moja. Kwa hiyo, idadi ya kura halali ni 363. Naomba kutangazia Bunge hili na nchi yetu kwa ujumla, kwamba kura za hapana hakuna hata moja. *(Makofi/Vigelegele)*

Kura zote 363 ni kura za ndio kwa hiyo amepata asilimia mia moja ya kura zote. *(Makofi/Vigelegele)*

### **WABUNGE FULANI: CCM, CCM!**

**SPIKA:** Ahsanteni sana, naomba mkae, Mheshimiwa Dkt. Mpango aendelee kuwa hapo, naomba mkae.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na Ibara ya 49, Makamu wa Rais kabla ya kushika madaraka yake ataapishwa mbele ya Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, kiapo cha uaminifu pia kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji kazi yake. Kwa hiyo, kwa tarehe itakayopangwa tutakayojulishwa, Mheshimiwa Makamu wa Rais Mteule, ataapishwa na Jaji Mkuu. Kwa ajili ya kupeana elimu ya kilichoko humu ndani. Lakini kabla hajaondoka hapa, nitoe taarifa ifuatayo:-

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa maelekezo kuhusu muda wa Wabunge kushika madaraka yao. Ibara ya 71 inaoorodhesha mambo ambayo kwayo Mbunge atakoma kuwa Mbunge na ataacha kiti chake cha ubunge. Miongoni mwa mambo hayo ni iwapo Mbunge anachaguliwa au anateuliwa kuwa Makamu wa Rais. Muda si mrefu Bunge hili limethibitisha uteuzi wa Mheshimiwa Dkt.

Philip Isdor Mpango, Mbunge wa Buhigwe kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Uthibitisho huu unamwondolea sifa Mheshimiwa Dkt. Mpango kuendelea kuwa Mbunge wa Jimbo la Buhigwe. Hivyo kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, nawajibika kuitaaruifu Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwamba kiti cha Ubunge wa Jimbo la Buhigwe sasa kiko wazi. (Makofi)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango ahsante sana, ubarikiwe sana na sasa tunakuruhusu ndugu yetu uweze kutoka na wakati akitoka basi tumpigie makofi ya kumtakia kila la heri Mheshimiwa Makamu wa Rais. Ahsante sana. (Makofi)

*(Hapa Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango - Mkamu wa Rais Mteule alitoka nje ya ukumbi wa Bunge na Wabunge waliimba wimbo wa tuna imani na Mhe. Dkt. Philip Mpango)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, nina matangazo mawili, tangzo moja linatoka kwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza Katibu wa Wabunge wa CCM, anasema kwamba leo Wabunge wote kutoka Zanzibar wa CCM watakuwa na kikao hapo ukumbi wa Msekwa, Wabunge wote kutoka Zanzibar wa Chama Cha Mapinduzi, mnaombwa by saa saba muwe pale Msekwa ambapo mtakutana na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu pia atakuwepo na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar atakuwepo. Mtakuwa na kikao kifupi pale, Wabunge wote wa CCM kutoka Zanzibar.

Tangazo la pili, ni la ibada kutoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe, kwamba Wabunge wote na wafanyakazi wa Wabunge mlioko maeneo ya Bunge mnakaribishwa katika *Chapelya* Bunge iliyoko maeneo ya jengo la Msekwa kwa ajili ya Ibada leo tarehe 30 Machi, 2021 kuanzia saa saba mchana mara baada ya kusitisha shughuli.

Mwisho kabisa, kwa kweli niwashukuruni sana kwa zoezi hili muhimu sana kwa nchi yetu ambalo tumelikamilisha kwa uaminifu mkubwa kwa umoja wetu Wabunge wote kabisa vizuri kabisa nasema ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge naamini kwa pamoja namna hii tutazidi kwenda vizuri na kwa *speed* kubwa zaidi. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni unajua katika kipindi hiki tunahitaji sana Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, kwa hali yetu ilivyo, basi mtaangalia angaalia huko, tunahitaji sana *a substantive* Waziri wa Fedha ili mambo yaweze kwenda kwa hiyo, ili lingine tutaangalia hali ilivyo.

Basi kwa hatua hii kwa sababu muda uliobaki ni mdogo sana kwa kweli yale mambo yetu ya Azimio inabidi tuyafanye jioni kuanzia saa kumi na moja kamili jioni. Hivyo, naomba tuwahi kurudi hapa tuweze kuendelea na yale maazimio yetu mawili. Kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni ya leo.

*(Saa 6.39 Mchana Bunge lllisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

### **MAAZIMIO YA BUNGE**

**Azimio la Bunge la Kutambua na Kuenzi Mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Utumishi wake Uliotukuka; na Azimio la Bunge la Kump ongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa ajili ya Azimio la kwanza.

**Azimio la Bunge la Kutambua na Kuenzi Mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utumishi wake uliotukuka**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii adhimu kabisa. Kwa mujibu wa Kanuni ya 61(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Hoja kwamba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha Azimio la Kutambua na kuenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utumishi wake uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kuwapa pole tena Watanzania na Waafrika kwa ujumla kwa kifo cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021 jijini Dar es Salaam. Hakika huu ni msiba mkubwa, kwani tumempoteza kiongozi mchapa kazi na mzalendo wa kweli aliyesimamia na kujenga umoja wa kitaifa, uzalendo na uadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alishika rasmi madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 5 Novemba, 2015. Katika kipindi chote cha uongozi wake alifanya kazi kwa bidii, umahiri, maarifa na kujitoa maisha yake kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alikuwa mzalendo wa kweli kwa nchi yake, mambo aliyoyafanya ni mengi kiasi kwamba kuyaorodhesha kwa hakika itachukua miezi kadhaa kukamilika.

Hata hivyo, katika kutambua na kuenzi mchango wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, naomba nikumbushe machache ambayo aliyasimamia wakati wa uhai wake akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliimarisha utumishi wa umma na mifumo ya taasisi za umma. Katika hili alirejesha nidhamu na uwajibikaji katika miongoni mwa watumishi wa umma hali ambayo imewezesha wananchi kupata huduma bora na kwa wakati. Vilevile, aliimarisha maadili kwa viongozi wa umma kwa kuanzisha utaratibu wa Kiapo cha Uadilifu kwa kiongozi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kiasi kikubwa alifanikiwa kuboresha huduma za jamii hususani kuboresha elimu, afya, maji na umeme vijijini. Kwa upande wa elimu alianzisha utaratibu wa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne katika mpango wa elimu msingi sambamba na kuongeza idadi ya shule za msingi kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka 2020 na shule za sekondari kutoka 4,708 mwaka 2015 hadi shule 5,330 mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya, alifanikiwa kuwezesha kuongezwa kwa bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa kutoka shilingi bilioni 31 hadi kufikia zaidi ya shilingi bilioni 300 na kuimarisha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Hospitali za Rufaa kama vile Moi, Mloganzila na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. Aidha, aliongeza zahanati kutoka 6,044 hadi 7,242; vituo vya afya kutoka 718 hadi 1,205 na kuajiri watumishi kwa ajili ya kutoa huduma katika sekta hiyo na kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali, vituo vya afya na zahanati kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta ya maji, pamoja na mambo mengine alifanikiwa kuanzisha na kukamilisha miradi mbalimbali ya maji na hivyo kutimiza azma yake ya kumtua mama ndoo kichwani. Aidha, alianzisha Taasisi ya *RUWASA* ambayo imekuwa kichocheo cha usambazaji na upatikanaji wa huduma za maji vijijini na mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa umeme alifanikiwa kuimarisha hali ya uzalishaji na usambazaji wa umeme hususani maeneo ya vijijini kupitia Wakala wa Umeme

Vijijini (*REA*) kwa kuongeza vijiji vilivyounganishwa na mpango wa umeme vijijini kutoka vijiji 2,018 mwaka 2016 hadi vijiji 10,312 Februari 2021 sawa na asilimia 84 ya idadi ya vijiji vyote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameteteleza kwa vitendo uamuzi wa miaka mingi wa kuhamishia makao makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma ambayo ilikuwa ni ndoto ya Rais wa kwanza na muasisi wa Taifa hili, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tangu mwanzo miaka ya 1970 sambamba na ujenzi wa ofisi za Serikali na taasisi za umma. Jambo hili limerahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi nchi nzima na kuchochea ukuaji na ustawi wa mikoa ya Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu, Serikali chini ya uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, imefanikiwa kuimarisha miundombinu katika nyanja zote ikiwemo ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kama vile barabara ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha. Aidha, aliwezesha ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za juu, yaani *fly over* na *interchange* na barabara za *by pass* Arusha na Mwanza, ujenzi wa reli ya kisasa yaani *standard gauge* kutoka Dar es Salaam – Morogoro ambayo imekamiliika na Morogoro – Dodoma ambayo ujenzi wake umefikia takribani asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo alifufua Shirika la Meli nchini kwa kununua meli mpya Mwanza, kukarabati Meli ya MV. Victoria na kujenga na kukarabati vivuko. Vilevile, amefanikiwa kufufua Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) kutoka kuwa na ndege moja (1) ndogo mbovu hadi kuwa na ndege kumi na moja hadi sasa. Aidha, alifanikiwa kuimarisha Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alifanikiwa kutujenga Watanzania katika kujiamini na kujinenea mema hadi tukaweza kuamini kuwa Tanzania sio nchi masikini bali ni tajiri na inaweza kuwa miongoni mwa nchi wahisani yaani *donor country*. Katika

sekta ya viwanda, uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, uliweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha viwanda. Kutokana na mazingira hayo jumla ya viwanda vipya 8,477 vimeanzishwa nchini kati ya mwaka 2015 – 2019. Kati ya viwanda hivyo 201 ni viwanda vikubwa, 460 viwanda vya kati, 3,406 viwanda vidogo na 4,410 viwanda vidogo sana. Katika juhudi za kuendeleza uchumi wa viwanda nchini aliweza bila kuyumba kusimamia uamuzi wa kujenga Bwawa la Nyerere, ujenzi unaogharimu zaidi ya trilioni 6 na utakaowezesha uzalishaji umeme wa megawati 2,115.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi 2020, ulipoibuka ugonjwa wa corona, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alifanikiwa kutoondoa hofu Watanzania na kutujengea matumaini kwamba tukimtanguliza Mungu mbele, tutashinda mapambano dhidi ya ugonjwa huo. Aidha, alisisitiza kwamba pamoja na kuwapo kwa ugonjwa wa corona ni lazima maisha yaendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, alihimiza wananchi kutumia mbinu mbalimbali za kisayansi na kiasili katika kukabiliana na ugonjwa wa corona. Alikataa kabisa kuiga mtindo wa kufunga mipaka ya nchi au kuwafungia wananchi wake wasitoke nje tofauti na viongozi wa mataifa mengine waliofunga mipaka ya nchi zao na kuzuia watu wao kutoka nje yaani *lock down*. Msimamo huo una mchango mkubwa kwa Tanzania kupiga hatua kiuchumi kiasi cha kupiga hatua za uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alikuwa kinara wa kuikuza na kuitangaza lugha ya Kiswahili nje ya mipaka ya Tanzania. Kwa juhudi zake, lugha ya Kiswahili imeweza kuingizwa miongoni mwa lugha rasmi za *SADC* na pia nchi mbalimbali zimeingiza lugha ya Kiswahili katika mitaala ya mataifa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo aliyofanya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ilikuwa ni kwa faida ya wanyonge nchini ambao kwa kiasi kikubwa walikuwa

hawanufaiki na rasilimali za nchi yao. Alikuwa mtetezi mkubwa wa makundi ya wananchi wa hali ya chini, kama vile, machinga na mama lishe. Naamini kila Mtanzania, anajivunia namna Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alivopigania na kujitolea maisha yake kwa faida ya nchi kama ambavyo yeye mwenyewe siku za karibia na mwisho wa uhai wake alisema, naomba ninukuu: "Lakini najua Watanzania wananipenda, ninajua ninayofanya ni kwa maslahi ya mapana ya Watanzania masikini. Kwa hiyo ndugu zangu, tuendeleo kuchapa kazi, tuendeleo kumtambuliza Mungu mbele kila mmoja kwa imani yake, lakini tujenge Tanzania yetu. Mimi ni mtumishi wenu na ninataka niwaambie ndugu zangu, siku moja mtanikumbuka na ninajua mtanikumbuka kwa mazuri si kwa mabaya, kwa sababu nime-sacrifice maisha yangu kwa ajili ya Tanzania masikini. Kwa hiyo, tusimame pamoja tusibaguane kwa vyama, tusibaguane kwa dini zetu, tusibaguane kwa makabila yetu, sisi tujenge Tanzania".

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo naomba sasa niwasilishe Azimio la Bunge la kutambua na kuenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa utumishi wake uliotukuka, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA kurejesha nidhamu, kuimarisha uwajibikaji miongoni mwa watumishi wa umma na kuimarisha maadili miongoni mwa viongozi wa umma, kuliiongezea ufanisi, tija na usawa katika kutoa huduma kwa wananchi;

KWA KUWA uboreshaji na uimarishaji wa huduma za elimu, afya, maji na umeme vijijini, kuliimarisha ustawi wa maisha ya wananchi kutokana na ongezeko la wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne kutoka 1,644,359 mwaka 2015 hadi kufikia zaidi ya 2,000,200 hivi sasa, ongezeko la bajeti ya sekta ya afya kutoka shilingi bilioni 31 hadi kufikia zaidi ya shilingi 300, pamoja na usambazaji umeme vijijini kutoka vijiji 2,018 mwaka 2016 hadi vijiji 10,312 kati ya vijiji 12,668 vya Tanzania kufikia Februari, 2021;

KWA KUWA utekelezaji wa uamuzi wa kuhamisha makao makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma umerahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi nchi nzima na vilevile umechochea ukuaji wa ustawi wa Mikoa ya Kanda ya Kati;

NA KWA KUWA ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara na ujenzi wa reli na madaraja, ununuzi wa meli na uboreshaji wa viwanja vya ndege, kufufua Shirika la ATCL na ununuzi wa ndege mpya umesaidia sana kukuza sekta ya uchukuzi, utalii na kurejesha heshima ya nchi ya kuwa na ndege zake na kukua kwa biashara kutokana na miundombinu kutumika kusafirisha bidhaa mbalimbali ikiwemo mazao ya kilimo.

KWA KUWA kujiamini na kujinenea mema kiasi cha Watanzania kujitambua kama Taifa lao si masikini bali linaweza kuwa miongoni mwa wahisani kumeiwezesha Taifa kuwa na hali ya kujitegemea katika ngazi ya maisha ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

KWA KUWA mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha viwanda, yalichangia kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na kuingia katika nchi yenye uchumi wa kati.

KWA KUWA kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la Nyerere katika Mto Rufiji, kwa ajili ya uzalishaji umeme wa megawati 2,115, kutaimarisha upatikanaji wa uhakika wa umeme na kwa bei nafuu na hivyo kwenda sambamba na Tanzania ya viwanda, jambo linaloendelea kukuza uchumi wa Taifa.

KWA KUWA kitendo cha kuwatoa hofu na kuwapa matumaini wananchi katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona, kwa kuwahimiza kumtanguliza Mungu, kutumia mbinu za kisayansi na za kiasili katika kukabiliana na ugonjwa huo na kukataa kuiga mtindo wa kufunga mipaka na kuwafungia wananchi wake wasitoke nje kulizingatia hali halisi ya uwezo wa kiuchumi kwa wananchi walio wengi

ambao kipato chao ni cha chini, kimeifanya nchi yetu isiyumbe kiuchumi na kuchangia kuingia kwenye uchumi wa kati.

NA KWA KUWA juhudi za Rais wa Tano Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kuikuza na kuitangaza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi kwa kutumia uhusiano wa kidiplomasia kumeiwezesha lugha hiyo kuingizwa kwenye lugha rasmi za *SADC* na mitaala ya mataifa mbalimbali jambo linalowezesha hata upatikanaji wa ajira.

KWA HIVYO BASI Bunge hili katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha Kwanza, leo tarehe 30 Machi, 2021, linaazimia kwa dhati na kauli moja kwamba tunautambua na tutauenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa utendaji wake uliotukuka ambao umefanikisha upunguzaji wa umasikini kwa wananchi, kuliwezesha Taifa letu kufikia uchumi wa kati na kupandisha hadhi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**AZIMIO LA BUNGE LA KUUTAMBUA NA KUENZI MCHANGO  
WA RAIS WA TANO WA JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA, DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI  
KWA UTUMISHI WAKE ULIOTUKUKA KAMA  
LILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(*Kanuni ya 61 (1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Juni, 2020*)

---

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 61 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha **Hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Azimio la Kuutambua na Kuenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Utumishi wake uliotukuka;**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nichukue fursa hii kuwapa pole tena Watanzania na Waafrika kwa ujumla kwa kifo cha Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021 Jijini Dar es Salaam. Hakika huu ni msiba mkubwa kwani tumempoteza kiongozi mchapakazi na mzalendo wa kweli aliyesimamia na kujenga Umoja wa Kitaifa, Uzalendo na Uadilifu;

**Mheshimiwa Spika**, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alishika rasmi madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 05 Novemba, 2015. Katika kipindi chote cha uongozi wake alifanya kazi kwa bidii, umahiri, maarifa na kujitoa maisha yake kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Taifa hili;

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi kwamba Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikuwa mzalendo wa kweli kwa nchi yake. Mambo aliyoyafanya ni mengi kiasi kwamba kuyaorodhesha, kwa hakika itachukua miezi kadhaa kukamilika. Hata hivyo, katika kuutambua na kuenzi mchango wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, naomba nikumbushe machache ambayo aliyasimamia wakati wa uhai wake akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

**Mheshimiwa Spika**, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliimarisha Utumishi wa Umma na Mifumo ya Taasisi za Umma. Katika hili alirejesha nidhamu na uwajibikaji miongoni mwa Watumishi wa Umma, hali ambayo imewezesha Wananchi kupata huduma bora na kwa wakati. Vilevile, aliimarisha maadili kwa viongozi wa umma kwa kuanzisha utaratibu wa Kiapo cha Uadilifu kwa Kiongozi wa Umma;

**Mheshimiwa Spika**, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kiasi kikubwa alifanikiwa kuboresha huduma za jamii hususan kuboresha Elimu, Afya, Maji na Umeme Vijijini;

Kwa upande wa elimu, alianzisha utaratibu wa elimu bila malipo kuanzia Elimu ya Awali hadi Kidato cha Nne katika Mpango wa Elimu Msingi sambamba na kuongeza idadi ya Shule za Msingi kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka

2020 na Shule za Sekondari kutoka 4,708 mwaka 2015 hadi shule 5,330 mwaka 2020;

Kwa upande wa Afya, alifanikiwa kuwezesha kuongezwa kwa Bajeti ya kwa ajili ya ununuzi wa dawa kutoka Shilingi Bilioni 31 hadi kufikia zaidi ya Shilingi Bilioni 300, kuimarishwa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali za Rufaa kama vile MOI, Mloganzila na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. Kuongeza Zahanati kutoka 6,044 hadi 7,242, Vituo vya Afya kutoka 718 hadi 1,205, kuajiri Watumishi kwa ajili ya kutoa huduma katika sekta hiyo na kuongeza upatikanaji wa dawa na Vifaa Tiba katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati kote nchini;

Kwa upande wa sekta ya maji, pamoja na mambo mengine, alifanikiwa kuanzisha na kukamilisha miradi mbalimbali ya maji na hivyo kutimiza azma yake ya kumtua Mama ndoo kichwani. Aidha, alianzisha Taasisi ya RUWASA ambayo imekuwa kichocheo cha usambazaji na upatikanaji wa huduma za maji Vijijini na Mijini.

Kwa upande wa umeme, alifanikiwa kuimarisha hali ya uzalishaji na usambazaji wa umeme hususan maeneo ya vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwa kuongeza vijiji vilivyounganishwa na mpango wa umeme vijijini kutoka vijiji 2,018 mwaka 2016 hadi vijiji 10,312 Februari, 2021 sawa na asilimia 84 ya idadi ya vijiji vyote nchini;

**Mheshimiwa Spika**, ameteteleza kwa vitendo uamuzi wa miaka mingi wa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, ambayo ilikuwa ni ndoto ya Rais wa Kwanza na Muasisi wa Taifa hili, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tangu mwanzoni mwa miaka ya 1970 sambamba na ujenzi wa Ofisi za Serikali na Taasisi za Umma. Jambo hili limerahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi nchi nzima na kuchochea ukuaji na ustawi wa Mikoa ya Kanda ya Kati;

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa miundombinu, Serikali chini ya uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imefanikiwa kuimarisha miundombinu katika nyanja zote



ikiwemo ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kama vile barabara ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha. Aidha, aliwezesha ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za juu (*flyover na interchange*), ujenzi wa barabara za By Pass Arusha na Mwanza, ujenzi wa Reli ya Kisasa (*Standard Gauge*) kutoka Dar es Salaam – Morogoro ambayo imekamilika na Morogoro – Dodoma ambayo ujenzi wake umefikia takriban asilimia 50. Pamoja na hayo alifufua Shirika la Meli nchini kwa kununua Meli mpya Mwanza, kukarabati Meli ya MV Victoria, kujenga na kukarabati vivuko;

Vilevile, amefanikiwa kufufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kutoka kuwa na ndege moja ndogo mbovu hadi kuwa na ndege kubwa kumi na moja hadi sasa. Aidha, alifanikiwa kuimarisha bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara;

**Mheshimiwa Spika**, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alifanikiwa kutujenga Watanzania katika kujiamini na kujinenea mema hadi tukaweza kuamini kuwa Tanzania sio nchi maskini bali ni tajiri na inaweza kuwa miongoni mwa nchi wahisani (*donor country*);

**Mheshimiwa Spika**, katika sekta ya Viwanda, Uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli uliweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha viwanda. Kutokana na mazingira hayo jumla ya viwanda vipya 8,477 vimeanzishwa nchini kati ya mwaka 2015 na 2019. Kati ya viwanda hivyo 201 ni viwanda vikubwa, 460 viwanda vya kati, 3,406 viwanda vidogo na 4,410 viwanda vidogo sana.

Katika juhudi za kuendeleza uchumi wa viwanda nchini aliweza, bila kuyumba, kusimamia uamuzi wa kujenga Bwawa la Nyerere ujenzi unaogharimu zaidi ya Trilioni 6 na utakaowezesha uzalishaji umeme wa Megawati 2,115;

**Mheshimiwa Spika**, Mwezi Machi, 2020 ulipoibuka ugonjwa wa Corona, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alifanikiwa kutuondoa hofu Watanzania na kutujengea matumaini kwamba, tukimtanguliza Mungu mbele tutashinda

mapambano dhidi ugonjwa huo. Aidha, alisisitiza kwamba pamoja na kuwapo kwa ugonjwa wa Corona ni lazima maisha yaendelee;

Vilevile alihimiza wananchi kutumia mbinu mbalimbali za kisayansi na za kiasili katika kukabiliana na ugonjwa wa Corona, na alikataa kabisa kuiga mtindo wa kufunga mipaka ya nchi au kuwafungia wananchi wake wasitoke nje tofauti na viongozi wa mataifa mengine waliofunga mipaka ya nchi zao na kuzuia watu wao kutoka nje (*lockdown*). Msimamo huu una mchango mkubwa kwa Tanzania kupiga hatua kiuchumi kiasi cha kuingia uchumi wa kati;

**Mheshimiwa Spika**, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikuwa kinara wa kuikua na kuitangaza Lugha ya Kiswahili nje ya mipaka ya Tanzania. Kwa juhudi zake, Lugha ya Kiswahili imeweza kuingizwa miongoni mwa Lugha rasmi za SADC na pia nchi mbalimbali zimeingiza Lugha ya Kiswahili katika Mitaala ya Mataifa yao;

**Mheshimiwa Spika**, mambo aliyofanya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ilikuwa ni kwa faida ya wanyonge nchini ambao kwa kiasi kikubwa walikuwa hawanufaiki na rasilimali za nchi yao. Alikuwa mtetezi mkubwa wa makundi ya wananchi wa hali ya chini kama vile Machinga na Mamalishe. Naamini kila Mtanzania anajivunia namna Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alivyopigania na kujitolea maisha yake kwa faida ya nchi, kama ambavyo yeye mwenyewe siku za karibia na mwisho wa uhai wake alisema:

*...lakini ninajua Watanzania wananipenda, ninajua ninayoyafanya ni kwa maslahi mapana ya Watanzania maskini, kwa hiyo ndugu zangu tuendeleo kuchapa kazi, tuendeleo kumtanguliza Mungu mbele kila mmoja kwa imani yake lakini tujenge Tanzania yetu. Mimi ni mtumishi wenu; na ninataka niwaambie ndugu zangu siku moja mtanikumbuka, na ninajua mtanikumbuka kwa mazuri si kwa mabaya, kwa sababu nime-sacrifice maisha yangu kwa ajili ya Watanzania masikini. Kwa hiyo, tusimame pamoja, tusibaguane kwa*

*vyama, tusibaguane kwa dini zetu, tusibaguane kwa makabila yetu. Sisi tujenge Tanzania.”*

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo naomba sasa niwasilishe Azimio la Bunge la Kuutambua na Kuenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Utumishi wake uliotukuka kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA**, Kurejesha nidhamu, kuimarisha uwajibikaji miongoni mwa Watumishi wa Umma na kuimarisha Maadili miongoni mwa Viongozi wa umma kulingeza ufanisi, tija na usawa katika kutoa huduma kwa wananchi;

**KWA KUWA**, uboreshaji na uimarishaji wa huduma za Elimu, Afya, Maji na Umeme Vijijini kuliimarisha ustawi wa maisha ya wananchi kutokana na ongezeko la Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza hadi cha nne kutoka 1,648,359 mwaka 2015 hadi kufikia zaidi ya 2,200,000 hivi sasa, ongezeko la bajeti ya sekta ya afya kutoka shilingi bilioni 31 hadi kufikia zaidi ya shilingi bilioni 300 pamoja na usambazaji wa umeme Vijijini kutoka Vijiji 2,018 mwaka 2016 hadi Vijiji 10,312 kati ya Vijiji 12,268 vya Tanzania kufikia Februari, 2021;

**KWA KUWA**, Utekelezaji wa uamuzi wa kuhamisha Makao makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma umerahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi nchi nzima na vilevile, umechochea ukuaji na ustawi wa Mikoa ya Kanda ya Kati;

**KWA KUWA**, ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara, ujenzi wa reli na madaraja, ununuzi wa meli na uboreshaji wa viwanja vya ndege, kufufua Shirika la ATCL na ununuzi wa ndege mpya umesaidia sana kukuza Sekta ya Uchukuzi, Utalii na kurejesha heshima ya nchi ya kuwa na ndege zake na kukua kwa biashara kutokana na Miundombinu kutumika kusafirisha bidhaa mbalimbali ikiwemo mazao ya kilimo;

**KWA KUWA**, kujiamini na kujinenea mema kiasi cha Watanzania kujitambua kama Taifa lao si maskini bali

linaweza kuwa miongoni mwa nchi wahisani kumwezesha Taifa kuwa na ari ya kujitegemea katika ngazi ya maisha ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla;

**KWA KUWA**, mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha viwanda yalichangia kuifanya Tanzania kuwa nchi ya Viwanda na kuingia katika nchi zenye uchumi wa kati;

**KWA KUWA**, kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la Nyerere katika Mto Rufiji kwa ajili ya uzalishaji umeme wa Megawati 2,115 kutaimarisha upatikanaji wa uhakika wa umeme na kwa bei nafuu na hivyo kwenda sambamba na Tanzania ya Viwanda jambo linaloendelea kukuza uchumi wa Taifa;

**KWA KUWA**, kitendo cha kuwatoa hofu na kuwapa matumaini wananchi katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona kwa kuwahimiza kumtanguliza Mungu, kutumia mbinu za kisayansi na kiasili katika kukabiliana na ugonjwa huo na kukataa kuiga mtindo wa kufunga mipaka na kuwafungia wananchi wake wasitoke nje, kilizingatia hali halisi ya uwezo wa kiuchumi wa wananchi walio wengi ambao kipato chao ni cha chini kimeifanya nchi yetu isiyumbe kiuchumi na kuchangia kuingia kwenye uchumi wa kati;

**NA KWA KUWA**, juhudi za Rais wa Tano, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, katika kuikuza na kuitangaza Lugha ya Kiswahili nje na ndani na nje ya nchi kwa kutumia uhusiano wa kidiplomasia kumwezesha Lugha hiyo kuingizwa kwenye Lugha rasmi za SADC na katika mitaala ya mataifa mbalimbali jambo litakalowezesha hata upatikanaji wa ajira;

**KWA HIYO BASI**, Bunge hili katika Mkutano wake wa Tatu, Kikao cha Kwanza, tarehe 30 Machi, 2021, linaazimia kwa dhati na kauli moja kwamba tunautambua na tutauenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utendaji wake uliotukuka ambao umefanikisha kupunguza umasikini kwa wananchi, kuliwezesha Taifa kufikia uchumi wa kati na kupandisha hadhi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb.

**MBUNGE WA VITI MAALUM**

30 Machi, 2021

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu wa kawaida, lakini kwa sababu siku ya leo kama mnavyooona kwenye ratiba yetu tunayo Maazimio mawili, yatawasilishwa yote kwa pamoja, halafu wakati wa kuwahoji baadaye tutawahoji kwa kila Azimio moja.

Kwa hivyo, nimuite sasa Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama kwa ajili ya Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 61(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha Azimio hili. Naomba pia kutumia nafasi hii, kumpa pole Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kifo cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021 jijini Dar es Salaam. Hakika huu ni msiba mkubwa kwetu sote Watanzania ila kwake yeye ni msiba mzito zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 47 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Makamu wa Rais ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano wa kwa ujumla. Ni wazi kwamba mafanikio ya Serikali chini ya uongozi wa Rais yeyote yanatokana na ushirikiano wa Rais huyo na Makamu wake. Kwa mantiki hii, mafanikio ya uongozi wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yana mkono wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa walifanya kazi bega kwa bega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuapishwa kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunawezesha muendelezo wa mafanikio yaliyopatikana. Aidha, uzoefu wake katika nafasi za uongozi, utumishi wa umma na taasisi za kimataifa unatoa matumaini kwamba Tanzania itaendelea kufanikiwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameitumikia nchi hii katika nafasi mbalimbali za uongozi. Miongoni mwa nafasi hizo ni pamoja na zifuatazo:

(i) Mwaka 2015 – 2021 alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

(ii) Mwaka 2014 alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

(iii) Mwaka 2010 – 2015 alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

(iv) Mwaka 2010 – 2015 alikuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jimbo la Makunduchi. *(Makofi)*

(v) Mwaka 2000 – 2005 alikuwa Waziri wa Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto na baadaye Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

(vi) Mwaka 2000 – 2005 alikuwa Mwakilishi wa Viti Maalum katika Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

(vii) Mwaka 2011 mpaka sasa amekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoa nafasi hizi alizowahi kushika kitaifa na kimataifa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kipindi chote alichohudumu kama Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akimwakilisha Rais katika mikutano na matukio mbalimbali katika taasisi za kimataifa na za nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo haya, ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ana uzoefu wa kutosha, weledi, na uwezo wa kuendeleza kazi nzuri za Rais wa Tano, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niwasilishe Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan sasa ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

KWA KUWA Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameshika nafasi mbalimbali za uongozi katika nyanja tofauti nchini, hivyo kuwa na uzoefu, uhodari, uthubutu na uwezo wa kuendeleza kazi nzuri za Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,

KWA HIYO BASI katika Mkutano wake wa Tatu, Kikao cha Kwanza, tarehe 30, Machi, 2021 Bunge linaazimia kwa dhati na kwa kauli moja kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kumuunga mkono katika majukumu yake ya kazi

ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumuomba afya njema, baraka na ulinzi wa Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(Makofi)

**AZIMIO LA BUNGE LA KUMPONGEZA MHE. SAMIA SULUHU  
HASSAN KUWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA - KAMA LILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Kanuni ya 61 (1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Juni, 2020)*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 61 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha **Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu Ijadili na kupitisha Azimio la Kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha Hoja ya Azimio hili;

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kutumia nafasi hii kumpa pole Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kifo cha Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021 Jijini Dar es Salaam. Hakika huu ni msiba mkubwa kwetu sote Watanzania, ila kwake yeye ni msiba mzito zaidi;

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 47 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Makamu wa Rais ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano kwa jumla. **Ni wazi kwamba mafanikio ya Serikali chini ya uongozi wa Rais yeyote yanatokana na ushirikiano wa Rais huyo na Makamu wake. Kwa mantiki hii, mafanikio ya uongozi wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yana mkono wa Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa walifanya kazi bega kwa bega.**



**Mheshimiwa Spika**, kuapishwa kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunawezesha muendelezo wa mafanikio yaliyopatikana. Aidha, uzoefu wake katika nafasi za uongozi, Utumishi wa Umma na Taasisi za Kimataifa unatoa matumaini kwamba Tanzania itaendelea kufanikiwa zaidi;

**Mheshimiwa Spika**, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameitumikia nchi hii katika nafasi mbalimbali za uongozi, miongoni mwa nafasi hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- Mwaka 2015 – 2021 alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
  - Mwaka 2014 alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
  - Mwaka 2010 – 2015 alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
  - Mwaka 2010 – 2015 alikuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jimbo la Makunduchi;
  - Mwaka 2000 – 2005 alikuwa Waziri wa Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto na baadaye Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;
  - Mwaka 2000 – 2005 alikuwa Mwakilishi wa Viti Maalum katika Baraza la Wawakilishi; na
  - Mwaka 2011 mpaka sasa amekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi.
- Mheshimiwa Spika**, ukiondoa nafasi hizi alizowahi kushika Kitaifa na Kimataifa, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kipindi chote alichohudumu kama Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akimuwakilisha Rais katika Mikutano na Matukio mbalimbali katika Taasisi za Kimataifa na nchi za nje.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo haya ni dhahiri kwamba Mhe. Samia Suluhu Hassan ana uzoefu wa kutosha, weledi na uwezo wa kuendeleza kazi nzuri za Rais wa Tano Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba sasa niwasilishe Azimio la Kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA**, Mhe. Samia Suluhu Hassan sasa ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

**KWA KUWA**, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameshika nafasi mbalimbali za uongozi katika nyanja tofauti nchini hivyo kuwa na uzoefu, uhodari, uthubutu na uwezo wa kuendeleza kazi nzuri za Rais wa Tano Dkt. John Pombe Joseph Magufuli;

**KWA HIYO BASI**, Bunge hili katika Mkutano wake wa Tatu, Kikao cha Kwanza, tarehe 30 Machi, 2021, linaazimia kwa dhati na kauli moja:

(a) Kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(b) Kumuunga mkono katika majukumu yake ya kazi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumuomba afya njema, baraka na ulinzi wa Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Joseph Kizito Mhagama, Mb.

**MBUNGE WA MADABA**

30 Machi, 2021

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea sasa na utaratibu wetu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza kuchangia lakini Waheshimiwa mtakuwa huru kuchangia azimio moja wapo au maazimio yote katika muda ambao mtakuwa mmepewa.

Sasa leo pia tuna changamoto kidogo ya muda kwa sababu ilikuwa tuanze kuchangia haya maazimio asubuhi lakini tukapata neema ya kupata Makamu wa Rais siku ya leo kwa hiyo hilo jambo likatuchukulia muda. Hata hivyo, yote ni mema. Naamini wale watakaotuwakilisha katika kuchangia leo tutaridhika na hayo ambayo watatuwakilisha nayo.

Hatutaweza kuchangia kwa ile idadi iliyokuwa imekusudiwa kuanzia asubuhi kwa sababu muda wetu hautaweza kutosha kuchangia kila mmoja aliyekuwa anahitaji kufanya hivyo. Kwa hiyo nadhani turidhike na wale wachache watakaopata fursa.

Ninayo orodha hapa ya vyama vyenye uwakilishi Bungeni, nimeletewa. Kwa hiyo tutaanza na hao wachangiaji ambao watapata fursa siku ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kukushukuru wewe, kulishukuru Bunge lako, na kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ameendelea kutupa nafasi ya kuwepo hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze kwa uamuzi mzuri wa kuamua kuleta maazimio haya mawili ndani ya Bunge kwa sababu kubwa mbili. Moja ni kumuenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumpongeza

mama yetu Samia Suluhu Hassan ambaye leo ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna maneno mazuri sana ya kusema leo, lakini ukweli ni kwamba inawezekana kulingana na vitabu vitakatifu yako mambo yameandikwa kwenye vitabu hivi vitakatifu, na sisi kama wanadamu tunaishi tusiojua leo wala kesho na mipango yote kama ambavyo Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye leo jina lake limeletwa mbele yetu na ametuambia mambo yote mazuri yanatoka kwa Mungu, hatuna shaka ya kwamba kipindi alichohudumu Dkt. John Pombe Magufuli ndio wakati wake aliopewa na Bwana kutenda yale aliyoyatenda na sisi kama Watanzania tuyaone na ikiwezekana tufate dira hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia tamko hapa, Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais, mama yetu Samia. Hakika ni kwamba huwezi kutenganisha shughuli iliyofanywa na Dkt. John Pombe Magufuli na mama yetu Samia Suluhu ambaye alikuwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Kwa msingi huo, hatuna shaka mama aliyepokea kijiti hiki amekipokea kutoka kwa mtu sahihi, na kwa sababu ya maandiko amekipokea wakati sahihi na hatuna shaka atalivusha taifa hili kama ambavyo wengi tunayo matumaini makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sisi kama Watanzania na sisi kama Wabunge tunafahamu lindi kubwa ambalo tunapita sasa. Lakini mimi niombe kutumia nafasi hii, nafasi ambayo leo tumepata mabadiliko ya uongozi bila kutegemea, ni wakati ambao sisi kama taifa na watu tuliopewa dhamana, ni wakati sasa wa kutenda sambamba na yale tunayoamini kwamba yatakwenda kuwasaidia Watanzania walio wengi na maskini.

Tumejionea mfano amesema hata Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa asubuhi namna ambavyo umati tuliouona kwenye kila mkoa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alikopita, ni ishara ya kwamba watu wanatamani kuona changamoto zao zinasemewa na kutatuliwa kwa kina na kwa vitendo.

Hatuna shaka mama ambaye naamanini sana. Na tumpe heshima hii ya kumuita mama, tuiseme tu mwanamke kwa sababu tunaamini ni wakati wa wanawake lakini tukimpa mama tunakuwa tunamtengenezea heshima na uzito mama huyu ambaye kwa mara ya kwanza katika taifa letu amepata nafasi hii na ninaamini anakwenda kutengeneza historia ambayo itajengwa na itakaa kwenye vizazi na vizazi kwa sababu inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia siku moja akihojiwa na *TBC*, ni namna gani anawaza na kufikiria kama ipo siku nchi hii itapata Rais mwanamke. Mama huyu kwa hekima akasema kama imetokea leo kwa mara ya kwanza Makamu wa Rais ni mwanamke, kwa nini huko mbele isiwezekane? Jambo lolote chini ya jua linawezekana kama tu Mungu amekupangia safari hiyo.

Kwa hiyo inawezekana hakujifikiria yeye akafikiria watu wengine kwenye vizazi vinavyokuja; lakini hakika kumbe Mungu alimpangia yeye na hakika amempa. Tumuombe dua, tumuombe mapenzi makubwa, lakini kikubwa zaidi tuendeleo kumuomba hekima, busara na uchapaji kazi ambao utatupa dira na kutuonesha Watanzania. Safari iliyoanzishwa na Dkt. John Magufuli ndiyo kwanza sasa imeanza kwa sababu imepokelewa na mama, na wote tunaamini mama akiachiwa familia watoto hawawezi kufa njaa, na vivyo hivyo, Tanzania haiwezi kubaki kama ilivyokuwa, tutakwenda kwenye wakati ambao tutavuka salama, na tena salama kuliko wakati wowote.

Bwana ambariki sana Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan na aendeleo kumpa mapumziko mema huko aliko Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono maazimio yote mawili. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabla sijaongea ninapenda kutoa pole kwa Kiti cha Spika pamoja na wewe pamoja na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi walioondokewa na kiongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa kwanza mwanamke, mama Samia Suluhu Hassan akituwakilisha wanawake ambao tunaona maono mbele ya kutetea Taifa hili la Tanzania na kwenda mbele kupambania haki za wanawake, wanaume na watoto wa nchi hii; ninampa pongezi. Yeye alipoapishwa tarehe 19 aliongea maneno ya matumaini kwa Watanzania; alisema tuache yaliyopita sasa tujenge Tanzania mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimuombe mama Samia Suluhu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi yetu ni moja na sisi sote tumezaliwa Tanzania kwa kusudi la Mungu. Tunamuomba asimame kama Rais wa watu wote, Rais wa vyama vyote.

Ninamuomba Mheshimiwa Rais pamoja na pongezi tunazompatia, tunaomba agange majeraha yaliyowapata Watanzania hasa wakati wa uchaguzi. Aweze kuwaachilia wafungwa wa kisiasa ambao bado wapo magerezani, hasa wale waliokuwa wamesingiziwa. Waliokosea, sheria ichukue mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais tunayempongeza leo alikuwa Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Tunaomba sana Mheshimiwa Rais uanzie pale ulipoishia, Katiba ya Warioba tunaomba uanzie hapo kulisogeza mbele Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba tangu ameapa kuwa Rais nchi imetulia, imeanza kupoa, watu wameanza kupata amani. Tunaomba amani hiyo yeye kama mama aisimamie, ahakikishe anasimama kama Amiri Jeshi Mkuu anayetetea pande zote bila kubagua. Tumeona viongozi baadhi ya vyama wameanza kuomba msamaha; hiyo ni dalili njema ya kujua kwamba kiongozi aliyepo sasa anasimamia haki, atasimamia Katiba na ataijenga na kuisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, ninasisitiza tena; ninakupa pongezi Mheshimiwa Rais, kwamba utasimamia haki na Katiba ya Watanzania kuhakikisha tunakwenda mbele maana safari bado ni ndefu, Tanzania bado ni imara, wewe ndiwe tunakutegeme kujenga na kuisogeza mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nasema ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nipate fursa ya kuchangia maazimio haya mawili yaliyoletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nami niungane na wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kwa msiba mzito ambao ulitufika kama taifa wa kuondokewa na mpendwa wetu Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio haya yamekuja kwa wakati sahihi na ni jambo sahihi na ni jambo muhimu na kubwa sana kufanywa na Bunge lako Tukufu. Katika miaka sita ambayo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amehudumu kama Rais wa nchi hii amefanya mambo

makubwa, amefanya mabadiliko makubwa sana kwenye taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema tuanze kueleza kazi nzuri na njema alizofanya Dkt. Magufuli, hata muda huu haunitoshi kusema yote mazuri aliyoyafanya. Lakini kama Mbunge na kama Mbunge kijana, nianze kabisa kwa kutambua mchango na thamani kubwa ambayo Dkt. Magufuli aliitoa kwa vijana wa taifa hili kwa kuwateua kwenye nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya nchi yetu. Mheshimiwa Dkt. Magufuli aliwaamini sana vijana, aliwapa nafasi za kufanya kazi na kuitumikia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana yako maeneo tumemuangusha kidogo lakini kwa sehemu kubwa vijana aliowateua walifanya kazi nzuri ya kumsaidia na kuleta uongozi kwenye taifa letu. Sisi kama vijana tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa imani hiyo kubwa kwa vijana. Amewatengeneza watu wengi kuwa viongozi na kuweza kutoa mchango kwenye taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kubwa zaidi alilofanya Dkt. Magufuli ni kutusaidia kukamilisha ndoto kubwa tulizokuwa nazo kama taifa kwa miaka mingi. Kwa muda mrefu tumekuwa na ndoto ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi yetu lakini tulikuwa tukisuasua kwenye utekelezaji wa jambo hili. Dkt. Magufuli kwenye kipindi chake amesimama imara jambo hili limefanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuishia kuhamishia tu makao makuu, alihakikisha kwamba Wizara za Serikali zinapata majengo mazuri na ya kudumu kwenye eneo la Dodoma ili Serikali iweze kufanya shughuli zake vizuri hapa Dodoma. Ni muhimu sana kuendelea kuenzi mchango huu.

Pia amefanya kazi kubwa kwenye kusimamia rasilimali za taifa letu. Tulibadilisha sheria kwenye usimamizi wa madini na nchi yetu imeongeza thamani na imeongeza mapato kutoka kwenye rasilimali tulizokuwa nazo kama taifa.



Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri alizofanya Dkt. Magufuli, lakini kwa mara ya kwanza kama kijana wa Kitanzania nimeona na kusahudia kitu cha tofauti. Nimeona na kusahudia baadhi ya watu wakifurahia kifo na kusema maneno yasiyokuwa mazuri. Kwa umri wangu mdogo, kwa nilivyolelewa kwa utamaduni wetu si jambo zuri sana kufurahia kifo cha mtu mwingine. Lakini pia si jambo zuri kukosoakosoa mtu akiwa ameshatangulia mbele ya haki.

Ninawaomba Watanzania, Dkt. Magufuli ameifanya kazi yake vizuri, ameimaliza safari yake, amefunga kitabu chake. Tumpe heshima anayostahili, tuendeleo kumuomba Mwenyezi Mungu amhifadhi mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuondoka kwa Dkt. Magufuli tumempata mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kipekee kabla ya kumpongeza Mheshimiwa Samia ni lazima Watanzania tujipongeze kama taifa. Tumepita kwenye kipindi ambacho pengine kuna watu walikuwa wanatuangalia kama tutavuka salama au hatutavuka salama. Lakini leo tunapozungumza kwa uimara wa Katiba iliyotengenezwa na waasisi wa taifa letu, kwa uimara wa sisi Watanzania na kupendana kwetu, kwa uimara wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, kama taifa tunavuka salama na tunavuka vizuri.

Tunayo sababu ya kujipongeza na kujivunia Watanzania, ni jambo kubwa ambalo tunaweza tukaliona kama ni jambo la kawaida, lakini ni jambo kubwa sana kuvuka kwenye kipindi kama hiki tukiwa salama na tukiwa tumeendelea kushikamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Samia kwa kupata nafasi ya kuwa Rais wa Nchi yetu. Mheshimiwa Samia ana uzoefu mkubwa kama ilivyosemwa na aliyewasilisha hoja ya Azimio la Kumpongeza. Ana uzoefu mkubwa kwenye kuongoza Serikali ya nchi yetu, ana uzoefu mkubwa kwa uongozi wa Serikali kwa pande zote mbili za Muungano, na hili ni jambo la kipekee na muhimu sana. Tunampongeza kwa kupata

nafasi ya Urais. Tuna matumaini kwamba ataifanya kazi hii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samia ni mchapakazi. Kama wako watu ambao wanafikiri baada ya kuondoka kwa Dkt. Magufuli mambo yatalegalega, wanafikiri watapata nafasi ya kuja kuiibia na kuifisadi nchi yetu, kwa mama Samia nafasi hiyo haipo. Ni mama mwadilifu anayependa taifa lake, mama mzalendo anayeichukua rushwa na mchapakazi wa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 ya mwezi Februari tulikuwa Korogwe kwenye ziara na Mheshimiwa mama Samia akiwa Makamu wa Rais. Tulikuwa na daraja linasumbua akiwa mama kwa muda mrefu, tulipomueleza akatoka palepale akafanya mawasiliano na Wizara na *TARURA* wakasema hawana fedha. Akawaambia hata kama hakuna fedha jengeni kivuko ambacho akina mama wanaokwenda kupata huduma za afya hawatateseka. Leo ninapozungumza mkandarasi yuko *site* ameshashusha vifaa na kazi inafanyika; ni ufuatiliaji wa mama Samia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba mama Samia Suluhu Hassan si mtenda miujiza. Kama ambavyo tumetoa ushirikiano kwa Dkt. Magufuli, nawaomba Watanzania tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, nawaomba tumuombee, nawaomba tushirikiane naye ili mama huyu aweze kuifanya kazi vizuri aende mbali zaidi kuanzia pale alipotuacha Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono maazimio yote mawili. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajiandae.

**MHE. SAASHISA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pia kabla ya kusema chochote, nitoe pole sana kwako wewe, kwa Mama

Samia Suluhu kwa kuondokewa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, familia ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye aliyetuletea mwenyewe Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Hii kwangu naitafsiri kama ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuja kwa Watanzania. Leo nasimama hapa kushukuru na kurudisha sifa na utukufu kwa Mwenyezi Mungu kwa zawadi hii ambayo alitupa ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoa hoja ameeleza mambo makubwa ambayo yamefanywa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, lakini Watanzania kwa hakika wanajua mambo haya makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Ukiangalia kipindi cha maombolezo, ukianza safari ya kuaga pale Dar es Salaam, hii ni dhahiri kwamba Watanzania wanajua haya mambo makubwa ambayo Hayati Dkt. Magufuli aliyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawakujali ukubwa wa uzito wa uzio ulipo pale Uwanja wa Ndege. Wakatafsiri, ndege ni zetu wenyewe, Rais ni wetu wenyewe na sasa tunaingia wenyewe kwenye uwanja wetu. Waliingia kuonyesha mapenzi yao kwa Rais wao mpendwa wanayempenda. Vile vile kila mahali msafara ulipopita, wananchi walijitokeza kwa wingi. Hii ni ishara kubwa kwamba wananchi walimwelewa, walimpenda na hili ni zao la Watanzania kwa hakika. Naomba nishauri, haya mambo makubwa yaliyofanya tuyaweke kwenye kumbukumbu, niishauri Serikali ikiona inafaa itenge siku maalum iitwe *Magufuli Day* kwa ajili ya kumuenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, Serikali ione namna ya kufanya hapa Dodoma, jiji ambalo mwenzangu aliyepita ameshaeleza namna ambavyo alipambana kuhakikisha linakuwa Makao Makuu ya Nchi; kijengwe kituo maalum kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake. Hii itakuwa

ni sehemu kubwa ya kuendelea kuenzi hayo mambo mazuri aliyoyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tayari alikuwa ameshaelekeza namna Wizara ya Elimu itakavyotengeneza mtaala wa kutengeneza historia yetu, basi kwenye mtaala wetu tuweke pamoja na viongozi wengine historia yake ili Watanzania waweze kuisoma vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, tunalo jambo la kujivunia kwa haya mambo makubwa ambayo wenzangu wameeleza. Leo tunazungumza uwepo wa reli, treni ya umeme; haya ni mapinduzi makubwa ya kihistoria ambayo yamefanyika wakiwa pamoja na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda moja kwa moja kwenye Azimio la pili. Haya mambo tunayoyataja leo, haya mambo tunayoyaona leo na kuyafurahia, barabara za chini na za juu zimejengwa, Vituo vya Afya vimejengwa, Mahakama wamejengewa ofisi nzuri. Kama wamejengewa Ofisi nzuri, watoto wanasoma kupitia Mfumo wa Elimu Bure, yamefanyika sambamba kwa kushirikiana na aliyekuwa Makamu wa Rais wakati huo ambaye leo ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sina mashaka hata kidogo kwamba miradi ile yote ambayo ilikuwa imepangwa itaendelea vizuri kabisa bila wasiwasi wowote. Tumeona katika kipindi cha muda mfupi, ndani ya siku tano, cha uongozi baada ya yeye kuapishwa kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya mambo makubwa ndani ya siku hizo tano. Kule Bandarini tumeona kilichotokea, hii ni ishara kwamba kiatu kilipotoka kimeingia kiatu kingine chenye *size* ile ile kwa *speed* nyingine kubwa. Kwa hiyo, tunayo matazamio makubwa sana. Hili lililotokea leo, nadhani wale ambao wanafuatilia kwenye mitandao, hapa kuna watu wamepigwa chenga ya mwili. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, walichokuwa wanadhani kwamba sasa tunafika mahali tunaenda kuyumba kama nchi, wamepigwa chenga ya mwili mzima. Leo tumeletewa tena Mtumishi mwingine wa Mungu, mtu ambaye ni mzalendo, amechukua nafasi ya Makamu wa Rais. Nasi hapa bila tashwishi tumempitisha kwa asilimia mia. Nawapongeza sana ndugu zangu upande ule kule kwa namna ambavyo tumeungana kwenye jambo hili. Huu ndiyo msingi wa kuanzia leo, tuendeleo kuungana kwenye mambo ambayo ni ya Kitaifa ili hata wale wengine walioko huko, ambao wamebaki na kazi ya kujifungia ndani, kazi yao ni *WhatsApp*, *Twitter*, kukashifu, kutukana nchi yetu, wajifunze kuanzia leo kwamba sisi ni Watanzania, tunaenda kusimama kuhakikisha Rais wetu anaenda kutekeleza yale yaliyopo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na vile vile yale yote ambayo waliandika katika hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka hapa, Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli alituletea hotuba hapa Bungeni inayoonyesha mwelekeo wa Serikali. Hotuba ile kwa hakika waliandaa pamoja na Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu. Kwa hiyo, haya yote yanaenda kutekelezwa kwa *speed* ile ile. Kwa hiyo, niwatumie salamu pia wale waliodhani kwamba tunaenda kukwama, Mungu ameshusha tena baraka nyingine na leo tumeshuhudia hapa namna ambavyo tunaenda kukimbia kwa *speed*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono na nawaomba sana Watanzania, tumwombe sana Mheshimiwa Rais wetu ili ayafanye yale ambayo ni matarajio yetu. Nasi kama Wabunge tusimame imara kuisaidia Serikali na kumshauri ili yale matarajio ya Watanzania yapate kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja zote. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, atafuatiwa na

Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa Jaqueline Msongozi ajiandae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja ya kumpongeza Rais wa Tano aliyepita kwa njia ya kifo na Rais mpya wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwape pole wafiwa wote wa Tanzania na hasa wenzetu wa Chama cha Mapinduzi ambao wamempoteza kiongozi wao wa Chama. Naungana na Watanzania wote wanawake kwamba wanawake wamefurahi sana kwamba wamepata kiongozi mwanamke ambaye atapandisha hadhi ya wanawake; kunyanyaswa kwa wanawake tunajua sasa basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upole, kwa hekima aliyonayo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na kwa CV ambayo tumeiona, tunaamini kwamba atasimama katika nafasi yake kuifanya Tanzania iheshimike katika Taifa hili na nje ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Watanzania wengi wanaamini kwamba kwa hekima yake atarudisha demokrasia kwenye vyama vyote vya kisiasa vipate nafasi kama ambavyo Muasisi wa Taifa hili Mwalimu Nyerere alitaka kwamba viwe na uhuru ambao ni kikatiba pia, kufanya mikutano yao bila kubughudhiwa na vyombo vya dola. Pia Watanzania wengi wanajua kuwa kupitia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan uhuru wa Vyombo vya Habari na uhuru wa wananchi kujieleza utapatikana yeye akiwa ni mama mwenye busara na hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hata Angela Merkel wa Ujerumani jinsi alivyopeleka ile nchi mpaka ikaheshimika mpaka leo. Tunajua kwamba nchi yetu ili iwe na upendo wa kweli na amani ya kweli ni lazima haki itendeke. Haki ndiyo inayoweza kuzaa amani ya kweli na kuleta upendo na umoja katika nchi yetu. Kwa hiyo,

tunaamini kwamba kupitia mama kama ambavyo mmesifu, akinamama ni watu ambao hawana ubaguzi; hatujasikia hata siku moja mama akisema mwanawe akafanye DNA, maana watoto wote ni wake. Kwa hiyo, tunajua kwamba vyama vyote ni vyake, wananchi wote ni wake, wenye vyama na wasio na vyama ni wake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, atasimama katika nafasi yake kuonyesha akinamama ambavyo tunaweza kuendesha nchi na isiingie kwenye mitafaruku wala vita. Kwa hiyo, tunashukuru na tunaamini kwamba Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan atalitendea Taifa hili kazi kubwa na ataonekana mwanamke wa kwanza siyo Barani Afrika tu na duniani kwamba nchi yetu hii ameipaisha kwa kurudisha demokrasia ya kweli, kurudisha vyama vyote viwe na nafasi sawa na kwamba akinamama wa Tanzania hawanyanyaswi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwombea Mwenyezi Mungu ambariki aweze kufanya kazi yake hii akiongozwa na Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Jaqueline Msongozi na Mheshimiwa Khatib Said Haji ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia maazimio yaliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Watanzania wote nami kutoa masikitiko yangu makubwa kwa kuondokewa na Kiongozi wetu. Pia niungane na wenzangu waliotangulia kusema kwamba Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe. Hatuna jinsi zaidi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu. Leo Mheshimiwa Dkt. Mpango amesema ni lazima Taifa liendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa demokrasia ile ile iliyopo kwenye nchi ya Tanzania ambayo wenzetu wengine hawaioni, tumeweza kufuata Katiba na kumchukua Makamu wa Rais na kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napata shida sana kusikia mtu anasema Serikali iliyopita ilikuwa haina demokrasia. Nasema demokrasia ipo na ndiyo maana baadhi ya Wabunge wenzetu vyama vyao viliwakataa, lakini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikasema ni haki yao kuwa Wabunge. Walikuja hapa wakaapishwa wakati hakuna Bunge. Kwa hiyo, naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano, lakini tuko na tunaipongeza na kuiombea kila la heri Serikali yetu ya Mama yetu, Rais wetu, Mama Samia Suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilianza kumfahamu Mheshimiwa Rais wetu wa sasa wakati wa Bunge la Katiba, alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Mama huyu alikuwa Mwenyekiti mahiri. Nakumbuka Mzee Samuel Sitta alikuwa ana-*dea*/sana na mambo ya kiutawala. Mama alikaa kwenye mijadala mizito, aliweza kuiamua, Bunge la Katiba lilikuwa liko *hot*, lakini mama alienda nalo vizuri na hatimaye tulivuka tukamaliza Bunge la Katiba salama salimini. Nina hakika na ninayo kila sababu ya kuwaambia Watanzania, tutaenda kuvuka na kazi itaenda kupigwa na tutafikia malengo yaliyowekwa katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani sana na Mheshimiwa Rais. Mfano juzi au jana wakati anapokea taarifa ya CAG, maamuzi aliyoyachukua, Watanzania wamempokea kwa mikono miwili. Wameona tuko kule kule kwa mzalendo, ana uchungu na fedha za Watanzania, ana uchungu na wezi na anachukua hatua kama alivyokuwa anachukua mtangulizi wake. Sipati shida kusema Mheshimiwa Mama Samia na Marehemu Rais wetu walikuwa ni Kurwa na Doto, walikuwa wanafanya kazi zao kwa pamoja. Kwa hiyo, niwaambie Watanzania, wawe na imani kubwa kwamba tunakwenda kutekeleza mambo yote tuliyoyaahidi kwa Watanzania. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia mwenzetu mmoja hapa anaongea kwamba Mheshimiwa Rais ahakikishe Katiba mpya inapatikana. Niwaambie tu, wakati Mheshimiwa Rais aliyepo sasa hivi madarakani na aliyekuwa amefariki, walitembea Tanzania nzima kuomba kura kwa Watanzania wakiahidi maendeleo, zahanati, maji, shule, elimu bure na kadhalika. Hawakuweza kuwaahidi Katiba mpya. Msitake kumtoa Rais wetu kwenye reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwenye mitandao, kuna raia mmoja wa Ubelgiji alianza kuandika kwamba tunataka Katiba mpya kwa Rais mpya. Mimi nimweleze tu, hawawezi wao kutupangia, tutajipangia wenyewe na tutakwenda kama tulivyojipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimwambie Mheshimiwa Rais, aliwaahidi Watanzania maendeleo, tunataka achape kazi alete maendeleo ili mwaka 2025 tutoke kifua mbele kwenda kuomba kura na hatimaye CCM iibuke kidedea kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Wabunge wenzangu kusema kwamba Mungu anaipenda Tanzania. Tendo la leo lililotokea la kumchagua Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mpango, niseme Mungu anaipenda Tanzania. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda kupata Makamu wa Rais mchapakazi atakayemsaidia Rais wetu kufanya kazi, mzalendo anayechukia rushwa, amekaa Wizara ya Fedha. Nani ambaye hajui Wizara ya Fedha? Leo angekuwa amejilimbikizia mali za kila aina, lakini siyo Mheshimiwa Dkt. Mpango. Ni mchumi aliyebobea. Tuna imani tutakwenda kupandisha uchumi wetu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Jaqueline, lakini nimepewa taarifa, nafasi yake atachangia Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Charles Mwijage ajandae.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa zawadi ya maisha ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye kupitia uongozi wake ametuachia mbegu ya ujasiri, mbegu ya kuipenda nchi yetu, mbegu ya uzalendo, mbegu ya kujiamini na mbegu ya kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, nchi yetu imeshuhudia maendeleo makubwa na miradi mingi mikubwa ikitekelezwa ambayo tunaamini kabisa kwamba itakwenda kuleta tija kwa Mtanzania na kulfanya Taifa letu liendee kusonga mbele. Mheshimiwa Hayati Rais Dkt. Magufuli alifanya kazi yake kwa kumtanguliza Mungu na ametuachia hilo kama funzo sisi viongozi katika kazi zote ambazo tunazifanya, tumweke Mungu mbele ili tuweze kufikia malengo na mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamkumbuka sana Hayati Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika nchi yetu ya Tanzania na kwa sisi hapa Dodoma kama ambavyo ilikuwa ada ya Azimio la mwaka 1973 la Makao Makuu, Hayati Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli alitekeleza kwa vitendo. Katika viongozi wote waliopita kila mmoja alifanya kwa sehemu yake, lakini tumeshuhudia chini ya uongozi wake, Makao Makuu ya Serikali yakiwa hapa Dodoma na Dodoma imebadilika hivi sasa, maendeleo yanakuja kwa kasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashuhudia miundombinu mingi sana ikikamilika ndani ya Dodoma na kuifanya Dodoma kuendelea kuwa kati ya sehemu ambazo zinakua kwa kasi

sana hapa nchini. Hii ni kazi kubwa na alama ambayo Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli ametuachia na tutaendelea kumkumbuka katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kazi ambayo ameifanya katika nchi yetu ya Tanzania na hasa katika kuwaamini vijana, ametujengea heshima kubwa sana vijana wengi wa Kitanzania kuamini kwamba wana uwezo wa kufanya kazi na kazi ambayo inaweza kuonekana na watu ambayo inaweza kuonekana na watu kuithamini. Ni kiongozi ambaye aliamini katika vijana akawapa nafasi na kwa asilimia kubwa vijana hao wamelitendea vyema Taifa hili, hivyo tunamshukuru sana kwa heshima hiyo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kazi hii kubwa yote iliyofanywa na Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tumempata mama yetu ambaye anakwenda kuiendeleza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye tunaamini kabisa atakwenda kuyasimamia yale ambayo Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli aliyaanzisha na kuyaendeleza kwa kasi kubwa zaidi. Imani yetu ni kwamba nchi yetu iko katika mikono salama. Wale wote waliokuwa wanadhani kwamba sasa mpira umerudi kwa *goal keeper*, hivi sasa kazi inaendelea pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kazi ambayo ameianza siku chache zilizopita, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan inaonyesha ni namna gani Tanzania ile ile ambayo kila mmoja alikuwa anaiota inaendelea. Nitoe rai kwa Watanzania nasi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika kazi hii ngumu kabisa na tunaamini kabisa Mwenyezi Mungu atamsimamia ili tuipeleke Tanzania kule ambako kila mmoja anataka Tanzania yetu iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mmoja anaamini katika uadilifu na uchapaji kazi wa mama yetu Mheshimiwa Suluhu Hassan. Ni Imani yetu kwamba nchi yetu ya Tanzania kupitia uongozi wake itaendelea kung'ara na basi yale yote ambayo

yalifanywa akiwa na Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli, huu ndiyo mwendelezo wake mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani kubwa sana ambayo tunayo kwa akina mama naye akiwa Makamu wa Rais ambaye alipita kwenye kipindi kilichopita, tunaamini ataifanya kazi hii vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naunga mkono maazimio yote mawili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Charles Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai wake ambao leo umewezesha kukutana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imepita katika mtihani mkubwa sana katika kipindi hiki. Umauti uliowakuta viongozi wetu wakuu wawili katika nchi hii, kwakweli ni pigo kubwa sana. Kuondokewa na Dkt. John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Seif Sharif Hamad, Makamu wa Rais wa Zanzibar. Kwa kweli ni msiba mkubwa ambao katika historia ya nchi hii haujawahi kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba naungana na Watanzania wote na Wabunge wenzangu kuyasifu, kuyaadhimisha na kuyapongeza mema yote waliyoyatenda viongozi wetu. Nataka niseme kwamba kwa imani yangu tunapaswa kumsema Marehemu kwa mema yake na sisi tunatimiza ibada kwa kuyasema mema ya Dkt. Pombe Magufuli kwa yale aliyoyafanya katika uhai wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Dkt. Pombe Magufuli ni binadamu na hakuwa mkamilifu lakini hatupaswi kuyasema

sasa kwani nafasi ya kujitetea hana tena. Kwa hivyo, nijielekeze katika kumpongeza kwa yale mema ambayo ametuachia na sisi tuko tayari kushirikiana na uongozi mpya uliopo kuyatekeleza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata Rais wetu mpya mama Samia Suluhu Hassan. Binafsi niseme nina imani na mama Samia Suluhu Hassan kama walivyo na Imani Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mola wetu Mtukufu alipoiumba dunia alimuumba Adam, kwa mujibu wa vitabu vitakatifu vinyosema lakini akaiona dunia siyo mpaka alipomtoa mama Hawa ubavuni kwa Adam. Kwa hivyo, Hawa ana nafasi kubwa sana na ndiyo maana leo akina mama tunawapa nafasi kubwa hata kama sisi tumewatangulia katika uumbaji wake Mola wetu Mtukufu. Hebu leo tujiulize bila akina mama hii dunia ingekalikaje? Ingekuwa ni mtihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mama Samia ameshika madaraka ya nchi hii ilianza kuonesha jinsi ambavyo atayadumisha yale mema ya mtangulizi wake. Pia tunaridhika na alivyotunesha kwamba ni mama anayejamini kweli kweli. Kwa hiyo, hatuna shaka hata kidogo na uongozi wa mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niseme kwamba tumepata pia Makamu wa Rais miongoni mwetu kwa maana ametoka hapa ndani. Nimevutiwa sana na aliyoyaongea hapa, ameongea mambo mengi jinsi watakavyosimamia yale maendeleo waliyoyaanzisha pamoja na mtangulizi aliyekuwepo. Amezungumzia habari ya kuimarisha barabara, reli, maji, elimu na afya. Hayo ni mambo mema ambayo kila Mtanzania anatakiwa ayapongeze yalivyofanyika na walivyopanga kuendelea kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nataka nimuombe Mheshimiwa Makamu wa Rais huko aliko kama

anasisikia, katika hotuba yake amegusia maendeleo ambayo wanatarajia kuyafanya. Nataka aweke *highlight* katika dondoo chache ambazo nitampa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeingia katika uchumi wa kati kwa jitihada zao na zetu. Sasa nataka kuiona Tanzania chini ya uongozi wao ikiingia katika demokrasia ya kati. Tutoke demokrasia tuliyonayo twende demokrasia ya kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namaanisha nini? Tunataka kuona uhuru wa vyama vya siasa unatekelezwa kwa vitendo. Tunataka kuona vyama vya siasa vinafanya kazi zake pasipo kubughudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Makamu wa Rais aweke *highlight* Katiba mpya ni mahitaji ya Watanzania, sisi na wenzetu wa CCM. Siyo mahitaji ya wapinzani kama inavyodhaniwa na baadhi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo, sisi waja tunapozungumza, waungwana onesheni vitendo. Katiba mpya haikuwa mahitaji ya Upinzani, Katiba mpya kwa mujibu wa ilipofikia tayari ilipitishwa, kilichobakia ni umaliziaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona fedheha sana kama mimi nilikuwa Mjumbe wa Bunge la Katiba na tulipiga kura kuipitisha leo akitokea mwingine akisema kwamba si kipaumbele cha nchi hii, ni ahadi na zilitumika pesa za Watanzania ili ipatikane Katiba mpya kwenye nchi hii. Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa Makamu wa Rais aweke *highlight* juu ya jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana uhuru wa vyombo vya habari. Najua upo na tunaposema haya si kwamba hayakuwepo unapodai leo barabara nzuri, siyo kwamba tulikuwa tukipita kwenye mapori, barabara zilikuwepo lakini tunataka barabara zilizoimarika Zaidi. Tunapozungumza tunataka uhuru wa vyombo vya habari siyo

kwamba haukuwepo kabisa lakini tunataka uhuru uliomarika kweli kweli. Hatutaki uhuru ambao mwandishi akiandika jambo anafikiria usiku mzima...

## T A A R I F A

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatibu, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimpe Taarifa kaka yangu Mheshimiwa Khatib kwamba wakati tunapitisha Katiba Mpya Wabunge wa Upinzani waliikataa na wakatoka nje. Nashangaa leo wanavyong'ang'ania Katiba Mpya. Hawa watu wakoje, wanataka nini? Tulikuwa tunaipitisha wakaikataa, leo tumekubaliana, wanaitaka tena. Yote hiyo wanataka kutuvuruga, hatutoki kwenye reli ya maendeleo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu dada yangu Munde. Mahitaji ya Katiba Mpya hayakuwa mahitaji ya Wabunge wa Upinzani, yalikuwa ni mahitaji ya Watanzania. Ninyi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa kuona yale ni mahitaji ya Watanzania ndiyo maana mliipigia kura ikapita kwa kishondo na mkacheza ngoma zote ndani ya Bunge hili. Kwa hivyo, kila tunalolikataa sisi kama na ninyi mnalikataa tuambiane kuanzia leo tujue hayo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuendelea. Katiba Mpya ni ahadi na tayari imepitishwa. Namuomba Mheshimiwa Rais ambaye naye alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba aliangalie kwa jicho pana jambo hili kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niligusia kuhusu uhuru wa vyombo vya habari siyo kwamba haukuwepo, tunapoomba mambo kuboreka ni kwamba tunataka twende mbele. Uhuru wa vyama vya siasa sio kwamba haukuwepo, lakini tunataka zaidi uimarike. Leo tunakuwa marafiki wakati tunazungumza hapa ukifika wakati wa uchaguzi mnabadilika, mnakuwa sura nyingine, tunakwenda wapi? Tunataka mambo haya yaondoke kama alivyosema mama Samia na sasa twende kwenye nchi ya kistaarabu, tufanye siasa kistaarabu, anayeshinda ashinde, anayeshindwa ampe mkono, Tanzania iende mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili natoa wito kwa wale wenzetu wote wanaoisema vibaya nchi hii sasa warudi nyumbani mambo yamenoga. Wasikae huko kuipaka matope, mama Samia yuko. Gwajima amesimama hapa amesema *Konki Fire*, sasa nasema rudini tujenge nchi yetu, tunaambizana hapa, tunasikilizana hapa, tufanye mambo yetu kama Watanzania. Tuache kubaguana kwa vyama, leo tumepiga kura hapa haijapungua hata moja, kwa nini? Tunapowapa mkono wa *aalan wasaalan*, mtoe mkono wa *aalan marhaba*, sawa? Tusiwape mkono mbele mkashika panga nyuma, hatutafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Charles Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Eric Shigongo ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuunga mkono maazimio mawili. Moja, la kumuenzi Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na la pili la kumpongeza Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kuwapa pole Watanzania wote kwa msiba uliotufika. Pia nichukue fursa hii kuwashukuru wote ambao walichukua



jitihada za ziada kuwasiliana nami kunipa pole kwa kuondokewa na kiongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumuenzi, mtu mwema anapofariki na muungwana akaamua kumuenzi Marehemu, njia nzuri ya kumuenzi marehemu ni kutenda yale mema ambayo yeye alipendezwa nayo. Si mara moja au mara mbili; hasa Bunge lililopita nilimsikia, siyo mimi peke yangu Hayati Dkt. Magufuli akisema nawashukuru sana Wabunge kwa kuniunga mkono nikaweza kutekeleza yale niliyoyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge tuna deni. Kama alitushukuru kwa kumuunga mkono sasa tutekeleze kama tulivyotekeleza kwake kwa huyu ambaye amekuwa mrithi wake. Tumuunge mkono Rais mama Samia kama tulivyomuunga mkono Hayati Magufuli. Hili sizungumzi na Wabunge tu, nazungumza na watendaji wa Serikali, nazungumza na wananchi wote Tanzania nzima, Mkoa mzima wa Kagera bila kusahau jimbo langu kwamba yale tuliyotenda kwa miaka mitano dunia ikatushangaa basi kwa kumuenzi na tutende maradufu tunapokwenda kufika mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyeondoka ni rubani mkuu lakini rubani mkuu alipokuwa anga za juu katika mwendo wa mbali alikuwa na rubani mkuu msaidizi. Kumbe hawa wote tulikuwa nao safarini na sisi abiria tulishajua tunakwenda wapi, tulishajua dira. Mwenyezi Mungu akaamua rubani mkuu akaishiwa pumzi, bila mtikisiko rubani mkuu msaidizi bila kuyumba akaendesha chombo na wakati muafaka akatuambia kwamba rubani mkuu hatunaye lakini hatukutetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapompongeza Mheshimiwa Rais, nampongeza kwa hilo. Watu waliyumba, watu walitetereka lakini rubani mkuu msaidizi akakaa kwenye usukani akaelekeza chombo kule kule. Tunakokwenda Watanzania tunakujua, tunakwenda katika ujenzi wa Taifa imara, siyo uchumi wa juu, Taifa imara, Taifa lililoendelea na

uzuri wa bahati, mwenye bahati habahatishi. Kumbe dira ya Taifa mwaka 2010 aliyekaa kupanga mipango mitatu ya miaka mitano mitano ni Dkt. Phillip Isdor Mpango. Sasa yeye anakwenda kuwa rubani mkuu msaidizi chombo kinakwenda kwa kasi ile ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri ukauliza watu wanakuonaje. Watu wanapanga matabaka, huu ni uchumi wa chini, huu ni uchumi wa juu; Dkt. Mwigulu Nchemba alisema Tanzania haikwenda kuomba ili iwe uchumi wa kati, haikuomba Tanzania, walikaa huko wakapanga. Ukitaka kujua demokrasia ya Tanzania ni tabaka gani, waulize Waganda, waulize Wakenya, watakwambia sisi ni demokrasia ya daraja la juu, la kati au lipi. Waheshimiwa Wabunge, kipekee niwaombe tunalo deni kubwa, wale nilioweza kuwaandikia niliwaandikia, Mheshimiwa Spika ni shahidi, tunachopaswa kufanya sisi Wabunge ambao ni viongozi wakubwa, wataalam wa mikakati wanasema ni *kuhold* yaani tushikilie haya mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo katika kujenga maendeleo ya nchi hii kwa miaka mingi iliyopita tulikuwa tunajifunza au tunapambana, sasa yale mafanikio ambayo tumeyapata katika kipindi cha Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tuyahodhi. Tumefanya vizuri katika ujenzi wa shule, tuhodhi. Tunapaswa kuongeza ubora wa watoto mashuleni, tuhodhi twende mbele. Tumeweza kudhibiti ukwepaji wa kodi, tuhodhi. Tumeweza kufanya vizuri, tuhodhi na yote aliyoyasema Makamu wa Rais mtarajiwa, tuhodhi na yote haya yamefanyika kwa mafanikio na kwa ushirikiano wa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono na napongeza yote yaliyoletwa mbele yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Neema Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric Shigongo, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii. Naomba nianze kwa kusema naunga mkono Maazimio yote mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Sekta ya Asasi za Kiraia ambazo mimi ni mwakilishi wao hapa Bungeni kupitia nafasi ya Viti Maalum Chama cha Mapinduzi, napenda kuwasilisha pole za dhati kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kufuatia kifo cha Hayati Rais Magufuli. Vilevile napenda kuwasilisha salamu za pongezi kwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki hii zaidi ya asasi za kiraia 200 kutoka Bara na Zanzibar zimewasilisha tamko la pamoja la pongezi na pole kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Vivyo hivyo, Jukwaa la Wanawake Wakurugenzi wa Asasi za Kiraia kwa maana ya *CSO's and NGO's* na wao pia wametoa tamko la pongezi kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Bunge lako Tukufu kuwa Sekta ya Asasi za Kiraia zina imani kubwa sana na yeye kwa sababu ana uzoefu mkubwa sana wa uongozi. Nitumie fursa hii kutaja maeneo machache.

La kwanza, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alianza ajira yake kwenye mwamvuli wa mashirika yasiyo ya Kiserikali linaloitwa *ANGOZA (Association For Non-Governmental Organizations in Zanzibar)* na kwa mantiki hiyo Mheshimiwa Rais ni mwana Azaki mwenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ana uzoefu mkubwa katika masuala ya uwezeshaji kiuchumi. Kupitia uzoefu huu mwaka 2016 Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bani Ki Moon alimteua Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wa Rais kuwa Mjumbe wa Jopo la Dunia kama mwakilishi wa Afrika lililopewa jukumu la kumshauri kwenye masuala ya uwezeshaji wanawake kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, miaka 25 iliyopita Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akiwa anatokea Sekta ya NGO's alishiriki katika Mkutano wa Beijing uliokuwa unalenga kuleta ukombozi wa usawa wa kijinsia ikiwemo wanawake kwenye nafasi za uongozi na maamuzi. Hivyo kupitia yeye kuwa Rais wetu wa kwanza mwanamke, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameiwezesha Tanzania kuweka historia ya kuwa sehemu ya utekelezaji wa Maazimio ya Beijing. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, nikiwa kama mdau wa lishe, sisi wadau wa lishe tunatambua juhudi kubwa ambazo Mheshimiwa Makamu wa Rais mteule ameweka katika kuhakikisha nchi yetu inaboresha hali ya lishe. Vivyo hivyo, tunatambua pia jitihada kubwa ambazo Makamu wa Rais mteule, Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango ambazo pia ameweka katika eneo hilo la kuboresha hali ya lishe kwa kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinatenga bajeti ya lishe kwa kulingana na idadi ya watoto wenye chini ya umri wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Sekta ya Asasi za Kiraia itampa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza dira yake ya maendeleo ya Taifa letu la Tanzania. Naomba nitumie fursa hii kipekee kuomba kuwasilisha ombi rasmi la kukutana naye kama Sekta ya Asasi za Kiraia ili nasi pia tuwe sehemu ya mafanikio yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumbariki na kumlinda Rais wetu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nasimama hapa jioni hii ya leo kutoa pole

kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa msiba mkubwa ambao umelipata Taifa letu. Natoa pole kwako wewe mwenyewe Naibu Spika na Spika wa Bunge letu. Natoa pole kwa Wabunge na Watanzania wote kwa msiba huu uliotupata. Ni msiba mkubwa ambao kwa kweli umetutikisa, lakini nashukuru kwamba tunaendelea vizuri kama Taifa. Ni jambo la kumshukuru Mungu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya Ijumaa tarehe 26 nilipokea simu kutoka kwa rafiki yangu kutoka Australia. Alinipigia simu kutoka Australia akiniambia kwamba, ameshuhudia bendera katika taifa lile zikipepea nusu mlingoti. Nilifurahi sana moyoni mwangu nilipojua kwamba bendera ile ilikuwa inapepea nusu mlingoti kwa sababu ya rais wangu Hayati John Pombe Magufuli. Ni jambo la kujivunia sana na kwa kweli sio jambo dogo kijana kutoka Chato kufanya bendera za dunia hii zipepee nusu mlingoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kama raia wa nchi hii ambaye nina kila sababu ya kujivuna kuwa na kiongozi kama Mheshimiwa Magufuli ambaye alijitoa sadaka, alijitoa uhai wake, alijitoa nafsi yake kwa ajili ya Watanzania masikini wa nchi hii. Amefanya mambo mengi ambayo siwezi kuyataja yote, wote mnayafahamu. Ameuthibitishia ulimwengu ya kwamba Tanzania inaweza kuendesha mambo yake bila kumtegemea mzungu. Tanzania inaweza kujenga reli yake yenyewe bila kutegemea mkopo. Tanzania inaweza kujenga bwawa la umeme bila kutegemea msaada wa mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni jambo kubwa. Kwa miaka mingi sana tumeishi tukiamini ya kwamba sisi ni watu masikini, hatuwezi kufanya lolote bila msaada wa mzungu, lakini Mheshimiwa John Pombe Magufuli amezunguka nchi hii akiwaambia Watanzania nchi hii ni tajiri. Nimesimama hapa leo napeleka ujumbe kwa dunia nzima wapate kuelewa ya kwamba, mimi Erick Shigongo sitoki Taifa masikini, ninatoka Taifa tajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilifika mahali anakuja mzungu hapa mbeba mizigo tu kule, lakini ukimuona unaona kwamba ni msaada. Sisi Watanzania, sisi waafrika, tunao uwezo wa kujiletea mabadiliko wenyewe bila kumtegemea mzungu wala mtu mwingine yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inakwenda kwa kasi. Nchi yetu leo iko kwenye uchumi wa kati. Ni kweli, ziko nchi zilizoingia uchumi wa kati, lakini baadaye zikarudi nyuma kuwa masikini tena. Kama Watanzania tunapaswa kujituma, kuteseka, kutimiza ndoto za Rais wetu, Hayati John Pombe Magufuli, ambaye ametangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufikiria kwa dakika moja, wakati Mheshimiwa anatuacha alikuwa anafikiria nini akilini mwake. Najua alikuwa anafikiria angetamani kuona Daraja la Busisi magari yanapita, angetamani kuona treni inapita pale *TAZARA*, treni inaenda kwa kasi kwenda Morogoro, hayo yote hayakutokea. Mahali fulani naamini ya kwamba, alikuwa ana *disappointment* kwa sababu ameondoka mapema. Kazi yetu sisi tuliobaki ni kumpa furaha Rais wetu, ni kumpa furaha Hayati Magufuli huko aliko kwa kuyatimiza haya mambo aliyokuwa ameyaanzisha, na inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio la pili ni la Mheshimiwa Rais Suluhu Hassan ambaye, kwa kweli nataka nikuhakikishie moyoni mwangu sina hofu hata kidogo wala sina wasiwasi. Matumaini yangu ni makubwa sana leo kwa sababu naamini uwezo wa mwanamke. Wanawake wana uwezo mkubwa sana, wanaume naomba tukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasayansi walifanya utafiti katika Chuo Kikuu cha Havard wakagundua ya kwamba, mwanamke ana *emotional intelligence* kubwa kuliko mwanaume, na ndiyo maana anaweza kufanya kazi tano kwa wakati mmoja, mwanaume ukipewa kazi moja unateseka. Kama hiyo ni kweli nina uhakika nchi yangu iko katika mikono salama, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan atalivusha Taifa hili mpaka kwenye uchumi wa juu kabisa

badala ya uchumi wa kati. Tumempata na Makamu wa Rais mtaratibu, mnyenyekevu, wote hapa tumetoa kura asilimia 100. Huyu mtu atamsaidia Rais wetu kutumiza ndoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisiongee mambo mengi. Nataka niwaombe wote pamoja tumuunge mkono Rais wetu kuipeleka nchi yetu mahali inapotakiwa kwenda. Ahsanteni kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Dokta Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Halamga. Mheshimiwa Nicodemas Maganga ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika maazimio yote haya mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpa pole Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuondokewa na Rais wetu, na Watanzania wote pia nawapa pole kwa msiba tulioupata, msiba mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba kusema kuwa Mheshimiwa hayati Dkt. Magufuli hakuna mtu ambaye haoni mambo aliyoyafanya. Alifanya mambo mengi mazuri na kweli inabidi tuyaenzi na tumuenzi kwa mambo yote aliyoyafanya. Amegusa kila kitu, kila Nyanja, kila sekta, kila mkoa, amefanya mambo mengi. Siwezi kuyarudia kwa sababu yote yameshasemwa, lakini afadhali niseme machache hasa kama reli ya mwendokasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli ya mwendokasi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ambayo sasahivi ujenzi umeshafika Morogoro nadhani alitamani kuiona, kuingia na yeye kuona anatembea kwenye reli hiyohiyo, lakini Mwenyezi Mungu hakupanga; lakini Watanzania ametuachia naamini Mheshimiwa Mama Samia, Rais wetu, ataendelea pamoja na wengine. Viongozi bado tunao watamalizia wataiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alifanya mambo ya Mwalimu Julius Nyerere ambayo na yenyewe ilikuwa imekaa kwa muda mrefu. Amefufua viwanda, ameanzisha viwanda, Mheshimiwa Rais kwa kweli Hayati Magufuli kila mmoja inabidi amuenzi, kila mmoja ameona aliyoyafanya. Hakuna kipofu kila mmoja ameona aliyoyatenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba tumuombee kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Na ninamalizia kusema amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kusema kuwa Mheshimiwa Rais, Hayati Magufuli ameondoka lakini ametuachia viongozi, ametuachia Mheshimiwa Mama Samia, ametuachia Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia, mama shupavu, mama mahiri, mama mtulivu, mama mnyenyekevu ambaye atatuvusha kwa yale yote ambayo yalikuwa yanafanywa Mheshimiwa Hayati Magufuli. Mheshimiwa Mama Samia alikuwa Naibu wake, Makamu wake na alikuwa anafanya mambo bega kwa bega pamoja na Hayati Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote iliyokuwa inaendelea Mheshimiwa Rais Samia anaifahamu vizuri sana. Mheshimiwa Rais wetu Samia ametembea nchi nzima anajua kila kitu kinachotendeka Tanzania. Kupitia kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi anaifahamu miradi pamoja na watendaji wake wa Serikali. Hatuna shaka Mheshimiwa Rais wetu atatuvusha, tuna imaninaye, tutafika mahali kule Kaanani, tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Mama Samia naamini na Watanzania wanamuamini; na yeye alisema kwenye mambo ya maji ataweza kuwatua. Yeye pamoja na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Mama Samia alikazania sana maji hasa kwa upande wa akinamama. Mheshimiwa Mama Samia tulifanya kampeni naye, wote mlikuwanaye mkoa mingi, mliona mambo mengi aliyokuwa anasisitiza sio tofauti na Mheshimiwa Hayati Magufuli



aliyokuwa anayatenda kwa sababu walikuwa wanafanya kazi pamoja. Kitu cha msingi tuzidi kumuomba Watanzania wote, wananchi wote, Serikali tushikamane nao, Wabunge, kusudi tuweze kufika kule ambapo tumeanza na ambapo tunakwenda. Nani haoni ndege ambazo zinaendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Mama Samia ataendeleza yale yote, tuna imani naye hatuna tatizo. Mnaona hata mijadala kwenye TV, wananchi wote wanamsifia Mheshimiwa Mama Samia hakuna ambaye anasema ooh. Wale ambao wanabeza hawapo, nadhani kama wapo hawajui wanalolisema, Mheshimiwa Mama Samia atafanya kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samia ni mwanamke wa kwanza kuwa Rais hapa Tanzania na Afrika Mashariki. Naamini atafanya; kama wanawake wanaweza na wanaume wanaweza hakuna tofauti. Mwenyezi Mungu alipomuumba Adam na Eva aliwaumba wote sawa. Naamini tutafanya kazi naye na tutampa ushirikiano na tutafika kila kitu kitakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa yote ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Watanzania, naomba tuzidi kumuomba Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, azidi kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninashukuru kwa kumpata Mheshimiwa Dokta Mpango. Tunampa pongezi Dokta Mpango, tunampa pongezi Mheshimiwa Rais wetu kwa kumpendekeza na Kamati Kuu kumpendekeza na Bunge tukampitisha kwa asilimia 100. Mheshimiwa Mpango ni mpole, mchapakazi, anaweza, Makamu anafanya kazi, tunashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana mpaka moyoni mwangu. Nilivyofurahi ndivyo Wabunge walivyofurahi. Nilivyofurahi ndivyo Watanzania walivyofurahi. Napata *message* nyingi kutoka kwa Watanzania. Napata *message* nyingi kutoka kwa wananchi wa Morogoro. Napata *message* nyingi kutoka wanawake wote na wanaume wote

Tanzania. Mwenyezi Mungu aijenge Tanzania. Mwenyezi Mungu ambariki Rais wetu. Mwenyezi Mungu ambariki Makamu wa Rais. Na Mwenyezi Mungu awabariki Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Mwenyezi Mungu tubariki Bunge zima, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Mheshimiwa Asia Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemus Maganga. Mheshimiwa Tawhida Galos Nyimbo ajandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwanza nianze na kuunga mkono azimio hili, maazimio yote mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuenzi na kutambua mchango wa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dokta John Pombe Magufuli. Kweli ni wingu la simanzi lililotawala anga ya nchi yetu kwa kupoteza jemadari wetu wa mapambano, baba yetu, mzalendo wa zama zetu, rafiki yetu na Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kukupa pole wewe na Watanzania wenzangu wote kwa msiba mzito uliokuta Taifa letu kwa kumpoteza Rais wetu mpendwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Sisi vijana wa nchi hii tutamkumbuka Mheshimiwa Magufuli kwa kutuonesha njia sahihi ya kuipenda nchi yetu, kuilinda nchi yetu na kuwa majasiri katika kuitetea nchi yetu kwa gharama yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi vijana tutamuenzi Hayati Rais Magufuli kwenye vitu vikuu vitatu, miongoni mwa vitu vingi alivyoacha alama katika mioyo ya Watanzania, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja uzalendo. Hakuna kati yetu atakayepingana na ukweli kwamba, Hayati Rais

Magufuli alikuwa mstari wa mbele pasipo kupepesa macho au pasipo kuwa na simile ya aina yoyote katika kuilinda na kuitetea nchi yetu dhidi ya adui yoyote wa nchi hii. Uhodari wake katika kulinda rasilimali za nchi hii, leo tuna ukuta wa Mererani, leo tuna *Twiga Cooperation Limited* na mengineyo mengi ikiwemo umahiri na uhodari wa utoaji huduma serikalini na zaidi kutetea dhana na kuaminisha kuwa nchi yetu ni nchi tajiri sana kupitia rasilimali zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, uongozi wenye maono (*Visionary Leader*). Hayati Rais Magufuli ametufunza kuwa viongozi kwa kuangalia kesho na kukubali kufanya kazi ya kutesema ili kesho ya nchi yetu iwe nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutazame miradi mikakati aliyोजना na kuisisitiza na kutimiza kama Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, ili kuzalisha umeme kwetu wa kutosha na hatimaye tunavyokwenda kujenga uchumi wa viwanda basi suala la umeme lisiwe lenye kutatiza tena. Mradi wa reli ya umeme ambayo licha ya kuunganisha mikoa ya kati na bandari yetu tunaenda kuunganisha nchi jirani kwa kuleta tija kwenye kufungua fursa za biashara na kufanya bandari yetu kukua. Vilevile Tunalinda miundombinu ya barabara na zaidi kupunguza muda wa usafirishaji wa mizigo, gharama za usafirishaji na pia kwani usafiri wa reli ni wa gharama nafuu kuliko wowote duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mtaani kuna usemi tulikuwa tunataniwa sana na majirani zetu wa Afrika Mashariki kwa sera nzuri...

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuko katika siku 21 za maombolezo na ndiyo maana binafsi nimeamua kuandika kwa ajili ya kuendelea kuomboleza kifo cha Mheshimiwa Rais, lakini pia kwa ajili ya kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, msinishangae kwa kusoma, kusoma nayo ni sehemu ya utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika hakuna kitabu kitakachotosha kuongelea umahiri na uhodari wa uongozi

wa Rais Magufuli zaidi ya kwamba Hayati Dkt. Magufuli ameacha uongozi wenye alama wa vit una alama ndani ya mioyo ya Watanzania. Nilihakikishie Bunge hili na Watanzania wote kuna kina Magufuli wengi ambao wamezalishwa katika kipindi chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nifupishe kwa kusema, Raha ya Milele Umme Ee Bwana, na Mwamba wa Milele Umuangazie. Apumzike kwa amani, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa na kuunga mkono azimio la kwanza, sasa niende azimio la pili... *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:**...la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...

...kuchekwa pia ni sehemu ya kuendelea mimi kuwa imara. Tuendeleo kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakika sisi kama vijana tunajivunia. Kwanza hatuna hfunaye kwa kuwa tunachokipigania sasahivi kwa Watanzania ni maendeleo na maendeleo hayo hayatoki sehemu nyingine tofauti na kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambayo mwaka 2020 Mheshimiwa Mama Samia alipita kuinadi, na hapa Bungeni ndicho tunachoendelea kukitimiza. Tuendeleo kumpongeza mama yetu na tumhakikishie kama vijana humu ndani tutahakikisha yale yote yatakayoletwa na Wizara na Mawaziri na Serikali juu ya maendeleo ya Watanzania na hasa kwa kuzingatia ilani yetu tutaunga mkono kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Makamu wa Rais Mteule kwa kukalia kiti chake. Hivi karibuni tunaamini anakwenda kuapishwa. Sisi kama vijana hatuna hofu naye, tuna imaninaye kubwa kwa sababu, amehudumu katika Serikali ndani ya nchi na nje ya nchi. Hatuna hofu wala shaka na Dokta Mpango. Hakika

tumepata Makamu wa Rais na sisi kama vijana tutahakikisha tunaunga mkono Serikali yetu na viongozi wetu ili kuendeleza amani, umoja na mshikamano wa Watanzania kwa maslahi mapana ya vijana sisi na vijana wajao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitangulia kwa kusema kwamba, bado nipo kwenye simanzi japo tuna furaha ya kuwapata viongozi thabiti na madhubuti katika taifa letu. Naomba kwa siku ya leo niwe nimeishia hapo, asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Asia Halamga. Waheshimiwa Wabunge, nilimuacha aendelee kwa sababu kuna watu walikuwa wanapata hisia hivi kama akizungumza bila kusoma inakuwaje, yuko vizuri. Nadhani mmeona yuko vizuri, akiamua kuandika sio kwamba, hawezi kuzungumza bila kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nicodemas Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo. Mheshimiwa Januari Makamba ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kuweza tena kupata nafasi hii ya kuweza kuongea yale aliyokuwa akiyafanya marehemu, baba yetu John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mungu, ninamshukuru Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi, Mungu amuweke mahali pema peponi. Kweli haikuwa rahisi kwanza mimi binafsi kuweza kufika kwenye Bunge hili tukufu maana ilikuwa kazi ngumu sana, lakini kwa uwezo wa Mungu na uwezo wake kwa juhudi zake Mheshimiwa nikaweza kufika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge; tarehe 27 mwezi wa pili wakati akitoka Chato Mheshimiwa Rais alipita Jimboni kwangu

Mbogwe, aliacha ahadi sitazisahau daima kwenye maisha yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge tarehe 27 mwezi wa Pili wakati akitoka Chato Mheshimiwa Rais alipita Jimboni kwangu Mbogwe, aliacha ahadi sitazisahau daima kwenye maisha yangu. Jimbo la Mbogwe ni Jimbo moja katika majimbo ya Kanda ya Ziwa lilikuwa limesahaulika sana katika awamu zilizopita zote zile nne, hatukuwa na lami, hatukuwa na taa barabarani, lakini Mheshimiwa alipita akatoa ahadi mbele za wananchi na mimi nilipata fursa ya kuongea na wananchi zaidi ya elfu tatu nikimwambia ukweli jinsi ulivyo katika Jimbo na matatizo ya Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya wiki moja tukamwona mama yetu anatangaza kifo cha Rais wetu, kweli tulipokea kwa masikitiko makubwa. Kwa kawaida sisi asili yetu Wasukuma huwa sio wepesi wa kuamini jambo, hatukuamini yale matangazo ya kwanza na kwa kuwa kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge tuko tofauti tofauti katika Imani, wale wenzetu ambao hawajamwamini Mungu walikataa kabisa, Wasukuma wale wa Kanda ya Ziwa kwamba haiwezekani huyu bwana afe, maana ilikuwa haijawahi kutokea siku moja ameonekana akiwa na *malaria* au akionekana akitibiwa popote pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mlivyokuwa mnaona Waheshimiwa Wabunge mitandao ilivyokuwa iki-*tweet*, kuna mtu anaitwa Kigogo, walikuwa wakisoma sana wananchi wangu hasa wa Kanda ya Ziwa wakihakikisha kwamba huyu jamaa wanamsingizia, ila kwa leo naomba niwape tu neno moja Yohana 14:1 ambalo inatutia moyo sote Watanzania bila kujali itikadi zetu na niwaombe tu baba zangu na mababu zangu wale ambao bado hawajamwamini Mungu tukubaliane tu kwamba hii hali imeshatupata na imeshatokea hakuna haja ya kufikiria wala kudhania kwamba labda tutazama. Tanzania naifananisha kama safari ya wana Israel wakati Musa akiwa anawatoa kwenye nchi ile ya shida, aliinuliwa mtu mmoja Yoshua na niseme tu kwa sasa hivi

dhahiri kabisa, mimi Mama Samia kiukweli nilikuwa sijamfahamu kivile maana nilikuwa ni mfanyabiashara kazi yangu ilikuwa nikukaa ofisini nilikuwa sifuatili sana mambo ya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa Hotuba yake ile ya kwanza tu ya kusema kwamba maumbile yangu ni ya kike imenipa moyo sana na kuzidi kuipenda siasa. Naamini sasa kumbe hata huyu aliyeingia ni mashine ile ile, ni kutwanga na kukoboa. Kwa maana hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge huu sio wakati wa kampeni, ni wakati wa kufanya kazi kama jinsi Rais alivyokuwa anatanadi kwenye majukwaa kwamba, kuisimamia Ilani yenye *page* 303, kuna kazi ambazo zimeainishwa mle, tusiwasahau wananchi wetu waliotufanya kufika huku. Nimeona niwakumbushe tu hilo maana tunaweza tukawa tunasema Katiba labda tukiibadilisha tunaweza tena kushindwa kufika mjengoni, matendo yako ndiyo yatakayokufanya kuja huku au usije kabisa huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo niseme, wewe ni mwanamama vilevile na Rais wetu sasa hivi ni mwanamke, nami nina watani wengi sana hapa Wagogo niwatanie tu kidogo kwa kusema, mtutendee haki sisi wanaume hasa Kanda ya Ziwa, tulishazoea kuoza wanawake wengi sana na nimeangalia mfumo wa Katiba huu kumtambulisha mwanamke ni mmoja tu hapa Bungeni na sisi Wasukuma tunaoa zaidi ya wanawake 10, kwa hiyo kuna kila sababu ya kuifanyia marekebisho hiyo Ibara ili kusudi mwenye wake 11, watano au watatu waweze kutambulishwa kwenye Bunge lako hili Tukufu ili wapate haki zao za msingi na wao ni binadamu. Pia kama mnavyoisoma sayansi wanawake ni wengi wanaume tuko wachache, japokuwa unaweza ukawa wewe una mume mmoja ukawa unaumia sana lakini naongea kwa niaba ya Watanzania ili tusijifiche fiche sana; na kwakuwa akinamama sasa hivi wanasema sasa tayari tumeshawapa rungu wasilitumie rungu lao vibaya ili tukashindwa kuwarudisha tena madarakani miaka ijayo, miaka 2025 na miaka mingine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Makamu kwa Hotuba yake ya mchana aliyoiiongea hapa, yeye kwanza amejitambulisha ni mtoto wa maskini na hasa maskini wanakuwaga na akili nyingi sana kuliko watoto wa matajiri. Kwa maana hiyo atumie hekima na busara sasa kuhakikisha kwanza Chama chetu cha Mapinduzi anatupa heshima ili tuweze kurudi tena humu Bungeni kiurahisi. Wabunge wengi wakipata madaraka pamoja na Waheshimiwa Madiwani na viongozi mbalimbali kupitia vyama huwa wanakisahau Chama. Kwa maana hiyo maneno yake yale aliyoyaongea mchana akiyaishi na sisi tukatembelea mlemle, hata kama utokee upinzani wa namna gani tutashinda tena kwa wingi na Watanzania wana imani na sisi sana hasa Chama cha Mapinduzi na mimi kweli imani imezidi kabisa kuongezeka kwamba hiki Chama kweli kiko imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimwangalia Waziri wa Mambo ya Nje yuko imara, Waziri wa Mambo ya Ndani yuko imara, kwa maana hiyo tusonge mbele kuhakikisha tunalinda rasilimali yetu na heshima ya Taifa letu, asitokee mtu akaja tena kututapeli kwa maneno ama kwa njia moja ama nyingine maana watu wa shetani wamejaliwa kuwa na maneno matamu sana, kama alivyosema Mheshimiwa pale kwamba sasa hivi tuachieni vyama, kweli watu wale wakiachiliwa wana maneno matamu na shetani alikuwa na maneno matamu vilevile hata Edeni pale alipomsogeza Eva akamdanganya Eva kula tena tunda ambalo halina matunda mazuri tukaingia kwenye dhambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo Watanzania tusingie kwenye maneno ya kushawishiwa kama vile Eva alivyoshawishiwa Eden tukahukumikiwa mwishowe tukaambiwa kufa tulikuwa hatufi lakini mpaka leo tunakufa. Kwa kukiamini Chama hiki cha Mapinduzi, lakini vilevile na sisi Wabunge tuko imara tuna uwezo kabisa wa kufanya chochote kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikutoe wasiwasi tu sisi Wabunge wa awamu hii kiukweli kama ni timu ilikuwa



imekuwa *sorted*, tuko tayari kwa lolote lile na ukitaka kujua Uchaguzi mdogo ule uliotangazwa mchana mimi naomba mnitume Buhigwe huko nikapambane na watu wa upinzani wenye maneno mabaya. Kwa maana mimi walinifundisha nazijua siasa za aina yeyote ile, siasa za matusi, siasa za kistaarabu, siasa za maombi, siasa za aina yeyote ile tutaenda kulipigania Jimbo la Mheshimiwa Philipo Mpango kuhakikisha kwamba linarudi kwenye Chama hiki pamoja na marehemu yule wa Kigoma sijui Jimbo gani, hivi alitokea jimbo gani? Nalo tutahakikisha linarudi kwenye Chama cha Mapinduzi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu Chama changu cha Mapinduzi uteuzi uliofanywa na Mama yangu Rais, umefanywa kila mtu kweli ameunga mkono hakuna mtu aliyepinga, maana amechagua chombo ambacho kinakubalika mbele ya Mungu na mbele za wanadamu ndiyo maana hakuna kura iliyoharibika. Wakiendelea kufanya hivyo hata kwenye kura za maoni kuchagua mtu anayetakiwa na Mungu maana uchaguzi wa Mungu mwanadamu hawezi akaushinda lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Nakushukuru sana, naiunga mkono hoja ila naomba Serikali iendeele kutusaidia zile ahadi za *page* 303, zitekelezeke ili turudi kwa urahisi huku. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos atafuatiwa na Mheshimiwa Ali King na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nichukue fursa hii ya kipekee kutoa pole

kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini vile vile nitoe pole kwa familia ya mpendwa wetu Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Pia nitoe pole kwa Watanzania wote, niwape pole Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, niwape pole Waheshimiwa Wabunge wote. Kila mja hakika kwake atarejea, Mwenyezi Mungu ampokee Kiongozi wetu ampokelee kitabu chake kwa mkono wa kulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mambo mengi ya kuweza kuongea kwa mpenzi wetu mpendwa wetu baba yetu Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli, kwetu Watanzania alikuwa kama taa, alikuja kwetu amefanya kazi akiwa kama taa, ameimulika Tanzania, amemulika vijana wa Tanzania, amemulika wanawake wa Tanzania, amemulika rasilimali za Tanzania, amemulika miradi ya Tanzania, amesimamia rasilimali za Tanzania akiwa yeye kama tochi, kama taa yenye mwanga mkali, kila Waziri aliyefanya kazi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliiona taa inapomulika anajua hapa pana jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walisimamia kwa sababu kwetu alikuwa ni taa, lakini simuoni kama taa tu, haitoshi kwetu kuwa taa, alikuwa barabara, alikuwa njia, tumepita viongozi vijana akituonesha na kutufunza huu ndiyo uongozi, akitufunza ujasiri, akitufunza jinsi kiongozi anavyopaswa kuwa, ametufunza kuwa wakakamavu, ametufunza mambo mengi, kwangu nimeona kama ni njia, kwetu amekua njia. Nadhani wengi ni mashahidi Watanzania walipokuwa wakitembea barabarani alikuwa njia, kwetu sisi tumepita kwake kama njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwetu amekua faraja, alikuwa faraja ya wanyonge, alikuwa jibu la wanyonge, alikuwa jibu la maskini, alikuwa jibu la akinamama wajawazito, alikuwa jibu la kumtua mwanamke ndoo kichwani. Kwetu alikuwa jibu, Mungu alimleta kwetu japo amefanya kazi kwa muda mfupi, lakini naamini dhamira yake ya kweli ametuacha sisi tumalize kazi. Tutahakikisha tunamuenzi kwa kupita kwenye njia ambazo yeye alitaka tupite, tutamuenzi kwa kuwa mwanga na sisi viongozi tuliokuwemo humu kama yeye alivyoangaza.

Naamini Waheshimiwa Mawaziri wamekuwa na vitu vingi kutoka kwake wamekuwa na mitazamo mingi kutoka kwake watafuata njia ambayo yeye alitaka sisi tupite

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa jinsi ya kipekee nimpongeze Mama yetu, Mama Samia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, niseme Mama Samia Mheshimiwa Rais alikuwa tuko naye hapa Bungeni, sisi tukiwa kama wanawake hatuna hofu juu yake, hatuna mashaka juu yake, tuna uhakika atatuwusha na tutafika salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka, kama kumbukumbu zangu ziko vizuri, kuna maneno ndani ya nafsi yangu kila ninapokaa yanakuja mara kwa mara, siku Mheshimiwa Mama Samia tuko kwenye kama sikosei kwenye kuapishwa, Waziri Mkuu mara hii tuko Ikulu alipata fursa ya kuzungumza, alizungumza maneno machache, lakini wakati anazungumza Mheshimiwa Rais wetu Hayati Dkt. Magufuli alikuwa yupo amekaa kitako, akatuambia baba umetufunza, tulichelewa kukufahamu, lakini kwa sasa tumekufahamu, tumekuelewa, alimwambia maneno hayo akiwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Magufuli Hayati alikuwa yu hai aliyazungumza mazungumzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazungumzo yale ndani ya nafsi yangu aliyoyazungumza Mama Samia yanaimba ndani ya nafsi yangu nikiamini kama aliweza kuyatamka akiwa yu hai, akisema tumekufahamu, tumekuelewa tutachapa kazi tuko na wewe, naamini hata sasa ndani ya nafsi yake bado maneno hayo yapo na ya hai, yanafanya kazi. Tuseme sisi kama wanawake tunamuunga mkono, kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunamuunga mkono na tutafanya naye kazi. Tuwatoe hofu Watanzania uwezo na ukubwa wa kufanya kazi Mama Samia unatosha, tutafanya nae kazi kwa jitihada zetu zote. Akiwa mama amebeba uchungu wa wanawake wote anao, akiwa mama amebeba uchungu wa watoto, akiwa mama amelibeba Taifa kwa uchungu wa mama anaugua na Taifa akiwa kama mwanamke hatuna

mashaka nae. Tunajua anaumia kama mwanamke, tunajua atapita kwenye misingi aliyopita Rais wetu, tunajua atatembea kwenye misingi ya Rais wetu, hatuna mashaka nae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuseme tunachukua fursa hii tena kumpongeza tunamtakia kila heri, Mwenyezi Mungu amnyooshee, ampe kauli ambazo Taifa letu linataka, ampe majibu ya Watanzania, aendeleo kusimama nae akiwa kama mwanamke, lakini kama alivyosema maneno yake yeye ni mwanamke wa jinsia kwamba yeye ni mwanamke, ila anauwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo maneno machache naomba nichukue fursa hii ya kukushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali King, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka ajjandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetupa uhai, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi. Ingelikuwa inaruhusiwa katika Bunge lako, ningelisema kwamba kitendawili na halafu wangeliniitikia tega, mtanikumbuka, mtanikumbuka, hicho ndio kitendawili ninachokipiga. Maana yake mtajua thamani yangu wakati mie mwenyewe sipo na mtanikumbuka kwa mazuri hamtanikumbuka kwa mabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mwenye kusema maneno hayo huyo ni mtu ambaye anahesabiwa mwenye maono. Je, hivi sasa hivi hatumkumbuki? Tunamkumbuka. Sasa ili tuone kama huyu mtu ana maono tulinganisha katika historia na watu wenye maono duniani ambao waliishi kwa maono na wakafanya maono. Mwenyezi Mungu alimwambia Musa nenda kwa mja wangu ambaye huyu utamkuta nimempa hekima na elimu, fuatana naye umsikilize

atakwambiaje. Musa akaenda akamkuta Hidhri, Hidhri akamwambia tutafuatana, lakini naomba nitakachofanya usiniulize mpaka nitakapokuja kukwambia mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hidhri akakuta Jahazi akaitoboa, Musa akalalamika akasema unatoboa jahazi ambayo wenyewe wanafanyia kazi katika bahari zao, akamwambia nilikwambia usiniulize utajua nini maana yake mwisho. Akakuta kijana, Hidhri akamuua, Musa akasema unaua nafsi? Akamwambia nilikwambia usiniulize, nilikwambia huwezi kusubiri kufuatana na mimi. Akafika Hidhri akaomba chakula mahali wakanyimwa, lakini katika mji ule ulikuwa unajengwa ukuta, baada ya kunyimwa chakula na maji Hidhri akamwambia Musa, tujenge ukuta, Nabii Musa akalalamika akasema khaa! hawa watu jambo waliotufanyia sio zuri, ndio wewe unasema kwamba tuwasaidie? Akamwambia hapa ndio mwisho wetu mimi na wewe, *hadha firakun baini wabaina, saunabi-ukabitaawil maalam tastatwii alaihi swabra.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakwambia maono yangu, ile safina au jahazi niliyoitoboa ilikuwa ya maskini, maskini hawa wakifanya kazi kwenye bahari, lakini mbele kule wanakokwenda kuna mfalme kila jahazi mpya anaichukua yeye, tumeitia aibu ili aiache, hilo ono la kwanza. Kijana tuliyemuua wazazi wake walikuwa ni waumini lakini tulikuwa tunahofia atawaingiza katika shirki, watampenda mtoto zaidi kuliko kumpenda Mungu, kwa hiyo tumetaka kufanya hivyo ili kuona hivyo. Mwisho, ukuta tumejenga ni wa mayatima wawili chini yake kumewekwa hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulinganishe tunaingia katika madaraka, Rais Dkt. John Pombe Magufuli Hayati, alisema nazuia mikutano ya siasa kwa mtu ambaye aliokuwa hajashinda jimbo wala hana nchi, nazuia mikutano watu wakalalamika, lakini je, haya maendeleo ambayo tumeyapata sasa hivi tumeona reli na miradi yote ambayo imefanyika ingelikuwa tunafanya siasa katikati tungefikia maono haya? Mtanikumbuka, huo ni uono wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuangalie katika kubadilisha Sheria za Madini, kuna watu walikaa hapa wakasema tutashtakiwa, ndiyo wale waliokuwa wakilalamika kwamba wanataka waambiwe palepale. Je, sasa hivi hatumiliki rasilimali zetu wenyewe? Tunamiliki, sasa haya ni maono, namzungumzia Dkt. John Pombe Magufuli katika maono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika jambo moja ambalo niliseme la kumuenzi Hayati. Walikuwa wakifanya uzalendo, uadilifu na uwajibikaji kwa sababu wanamstahi na kumwogopa Dkt. John Pombe Magufuli Hayati, ameshafariki na hayupo, lakini kama wale ambao waliokuwa wanakuwa wazalendo, waadilifu na wanachapa kazi na wawajibikaji kwa sababu ya mama Tanzania, basi bado mama Tanzania ipo, hiyo ndio njia ya kumuenzi Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alikuwa ni mja wa Mungu, hivyo kama kuondoka kwake sisi tutarudi tena tuanze kula rushwa, tutakuwa tena wavivu na wazembe? Atakayefanya hivyo hataidhuru nchi yake, atajidhuru yeye mwenyewe. Kwa hiyo, hiyo ndio njia ya kumuenzi Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka Mheshimiwa Nicholas Ngassa ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya kwanza kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia Maazimio yote mawili yaliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu Afrika na dunia nzima imeshuhudia upendo usio na mfano ulioonyeshwa na Watanzania walipojitokeza kumsindikiza, kumuenzi na kumuomba Hayati mpendwa wetu Dkt. John Pombe Joseph magufuli. Upendo waliouonesha Watanzania katika maeneo

ulikopitishwa mwili wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na maombi na dua yaliyofanyika nchi nzima katika maeneo ambapo mwili wa mpendwa wetu haukuweza kufika ni ushahidi tosha kwamba Watanzania walikuwa na imani kubwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wetu wa Awamu ya Tano alifanikiwa kujijengea uhalali wake mara alipochaguliwa na Watanzania kuwa Rais wa nchi yetu. Rais hayati Mzee Benjamin William Mkapa aliwahi kusema: “Kazi ya uongozi ni kuonyesha njia na watu wanakufuata si kwa sababu wanakuogopa ila kwa sababu wanakuamini na imani ya kweli haitokani na maneno bali matendo”. Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matendo ya hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yalimjengea heshima, imani ya Watanzania kumfuata. Kazi aliyoifanya kwa miaka mitano akisaidiana na Mheshimiwa Samia Suhulu Hassan amekijengea chama chetu na Taifa letu uhalali wa kuendelea kuheshimika Barani Afrika na duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi nyote ni mashahidi na Watanzania ni mashahidi kwamba ukiacha kufanya maombolezo tuliyofanya kwa kujitokeza kila mmoja wetu lakini siku ya kumuaga Afrika ilileta Rais wapatao 16 na Mabalazi wasiopungua 51 waliotoka kote duniani. Pia nchi zote dunia ambazo hazikuweza kuleta Mabalazi na Rais walituma salamu kwa Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan kufuatia kuondoka kwa shujaa wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha kwamba maisha ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli siyo tu yaliwagusa Watanzania yaligusa Afrika na dunia yote. Kinachosikitisha ni kwamba wakati mataifa haya yakitupa pole na kuomboleza pamoja nasi bado kuna Watanzania wenye *passport* za Tanzania wanaobeza kazi iliyofanywa na hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kazi yetu ni kuendelea kuwaombea msamaha kwa Mungu awafunulie ili siku moja waweze kujua kweli na warudi kuungana nasi

katika kuweka Utanzania mbele hata kama kwa sasa wanalishwa na hao wenye nia oву na Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii tena kueleza bayana kwamba tunamuenzi Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri aliyofanya na tunampongeza mama Samia Suluhu Hassan kwa kupokea kijiti cha kuendelea kuongoza Taifa letu. Wote wawili hawa wamepata uongozi bila ya kuwa na makundi, bila kutoa hata shilingi. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alichaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa bila kuhonga hata shilingi moja naye alimteua mama Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea mwenza na hatimaye wakaongoza jahazi la nchi yetu kwa muda wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya miaka hiyo mitano mmeshuhudia kiwango cha kura ambacho CCM imeweza kupata katika uchaguzi wa mwaka 2020. Huu ni ushahidi tosha kwamba tulitekeleza Ilani ya Uchaguzi chini ya uongozi wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu uhalali wa uongozi wowote na hasa kwa mujibu wa Mwongozo wa Chama cha Mapinduzi wa mwaka 1981, ibara ya 107 unatokana na uongozi huo kuendelea kuwa tetezi wa kuaminika kwa maslahi ya makundi au kundi lililokuwa kubwa katika nchi yetu. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba kijiti kinapokabidhiwa kwa mama Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa kiongozi kutoka kwenye ngazi za msingi hadi ngazi ya Taifa ya chama chetu na ameongoza Serikali zote mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano na hatimaye Makamu wa Rais, tuna uhakika kabisa nchi yetu ipo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme la mwisho kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*



**NAIBU SPIKA:** Kengele imegonga Mheshimiwa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nina hakika kabisa miaka hii iliyobaki katika unguwe hii ya miaka mitano itakuwa ndiyo miaka mitano ya kwanza ya mama Suluhu Hassan na miaka mitano mingine itakuwa miaka ya unguwe yake ya pili kwa mujibu wa Katiba yetu. Hili tujiandae kifika na kimtazamo kwa watu ambao walikuwa wanafikiri 2025 uongozi utabadilika. Ni zamu yao, sisi Bara tuliongoza miaka 23 ya Mwalimu, tukaongoza miaka 25 tena mingine siyo dhambi...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siyo dhambi sasa kwa Mzanzibar mmoja aliyejipambanua na mwenye sifa kuendelea kuwa Rais katika miaka hii iliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Nicholas George Ngassa, Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa ajiandae.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kupata nafasi hii kuchangia Maazimio yote mawili. Ni kweli tumepata msiba mzito sana kwa nchi lakini pamoja na mataifa mingini, ni pole kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan lakini pamoja na sisi sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kawaida watu wakipatwa msiba hata katika familia zetu ni lazima watayumba sembuse msiba mkubwa kama huu ulioupata taifa, ndiyo maana wengine wameanguka, wengine walikosa matumaini, ni kawaida misiba inapotokea. Pia na matendo ya aliyetutoka, matendo ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambayo amelitendea Taifa hili hasa katika nyanja za maendeleo, miradi mingi imetajwa

pamoja na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali, ndicho kitu ambacho Watanzania wengi sana waliweza kulia na kunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kunukuu maneno ya Mheshimiwa Rais Kenyatta, Rais wa Kenya, wakati amekuja kutoa rambirambi na salamu za mwisho alimuambia Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan kwamba hata wao Kenya wanaona Mheshimiwa Rais hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameshafungua njia. Kwa hiyo, kazi yetu sisi ni kufuata njia ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mashaka yoyote na mama Samia Suluhu Hassan ambaye ni Rais wetu wa sasa. Tumeshanza kuona kwa vitendo namna gani ameanza kazi. Msiba kwa sasa tunao kwa siku zile 21 lakini na kazi zinaendelea. Nampongeza sana Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alivyoanza kufanya kazi zake. Ameanza kidogokidogo kutusahaulisha hata yale machungu na mashaka ambayo watu walikuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi sana kuongelea huyu ni mwanamke, huyu mwanaume, napenda sana kuangalia utendaji wa kazi. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameanza kazi vizuri sana kwenye kikao kile ambacho kilikuwa cha kupokea ripoti ya CAG na wengine walitajwa kidogo baada ya kusomwa ile ripoti siwezi kusema aliondoka na mtu lakini kuna kitu alikiona hakijakaa sawasawa haraka sana aliweza kuchukua hatua na haya ni matarajio ya wananchi wengi katika utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, mara nyingi sana vitu vinavuja kwa viongozi mbalimbali hasa katika kazi za utendaji, kitu kinaweza kikawa ni siri lakini kinavuja. Leo hii watu waliongelea watu wa mitandao hapa, kuna mmoja akamtaja Kigogo na wengine, kwa mara ya kwanza kina Kigogo leo hawakujua hata jina ambalo litaletwa humu. Walitaja majina mbalimbali ambayo wanayajua wao siye hatukuliona humu. Pia nikipongeze Chama changu cha Mapinduzi katika hili kwa sababu Mheshimiwa mama Samia

Suluhu yeye ndiye Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi mpaka tunaingia humu hatujui jina ni la nani litakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan ameanza vizuri mama yetu tuendeleo kumuomba. Kazi hii ni ngumu na ni nzito halafu imekuja ghafla, sisi tuendeleo kumuomba ili aweze kufanikiwa katika majukumu yake na aweze kuliongoza Taifa letu vizuri na mimi sina shaka hata kidogo na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono Maazimio yote mawili kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicholas Ngassa atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa, Mheshimiwa Godwin Kunambi ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Maazimio mawili yaliyopo mbele yetu; azimio la kuenzi kazi za Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Azimio la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe pole kwa Taifa la Tanzania kwa kuondokewa na Rais wetu, nitoe pole kwa familia ya marehemu kwamba tumeondokewa na kiongozi ambaye tulikuwa tunampenda lakini Mwenyezi Mungu amependa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wangu nitaongelea mambo kama mawili au matatu kumhusu Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Mwaka 1775 -1783, Marekani walikuwa katika vita vya mapinduzi vya kujitelea uhuru. Baada ya kupata uhuru Wamarekani walifanya utafiti kupitia chuo kinaitwa *National Institute of Psychology*. Katika chuo kile walifanya utafiti ili kujua unapotaka kufanya mabadiliko

katika nchi au katika taasisi yaani *institutionalization* unatakiwa kufanya vitu gani. Marekani walikuja na vitu saba ambavyo walisema lazima waviweke katika vichwa vya watu wao. Jambo la kwanza walilogundua ni kubadilisha *attitude* na *mindset* za watu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ametusaidia kama Taifa ni kubadilisha *attitude* na *mindset* zetu Watanzania ambapo ilifikia hatua tukawa tunatembea na falsafa kuwa Watanzania siyo maskini na sisi Watanzania siyo maskini na Taifa letu ni tajiri. Jambo hili limeweka msingi mkubwa ambapo imefikia kama taifa tunatumia rasilimali za ndani kuleta maendeleo. Taifa linajiendesha, tunajenga vituo vya afya, tunajenga miundombinu na kila kitu ambacho kinaweka misingi ya maendeleo katika kuhakikisha Taifa letu linasonga mbele. Kwa hiyo, katika hili tutamuenzi Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na hakika tunaendelea kutamba na kutembea kifua mbele kwa ujasiri sisi Watanzania ni matajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni tekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 kwa ufanisi mkubwa sana. Katika hili hakuna ubishi. Unapooengelea Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuna kitu kinaitwa Mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi wa mwaka 2010-2020 ulitaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi itakayoingia madarakani 2015 iweke msingi wa kuhakikisha tunafikia uchumi wa kati ifikapo 2025. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akishirikiana na Makamu wake wa kipindi kile mama Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa na Bunge la Kumi na Moja tulifika uchumi wa kati mwaka 2020, miaka mitano kabla. Hili ni jambo la msingi na la kuenziwa na sisi tunawashukuru mliokuwa katika safari ya Bunge la Kumi na Moja. Kwa hiyo, haya ni mambo makubwa na ya msingi ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyafanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano wamelifanya ni kuhakikisha tunakuwa na mfumo wa malipo Serikalini ya kielektroniki tunasema *e-payment*. Tulihama kutoka mfumo wa *billing system* tukaenda *electronic payment* na tuka-establihi kitu kinaitwa *Government Electronic Payment Get Way* jambo ambalo leo hii tunatamba na kusema tunajitahidi kukusanya mapato lakini ni kwa sababu ya mfumo imara wa ukusanyaji ambao umehakikisha mapato yanatoka na kwenda katika chungu kimoja. Katika hili tunamshukuru Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa upande wa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, nije katika suala la kumpongeza Rais mama Samia Suluhu. Nimesimama hapa kwa niaba wananchi wa Jimbo la Igunga, Mkoa wa Tabora, tunampongeza kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kuwa alikuwa sehemu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tunaamini gurudumu atalipeleka vizuri, tutakwenda vizuri kama Tanzania na sisi wananchi wa Igunga tupo tayari kumuunga mkono. Walituletea maji ya Ziwa Victoria, tuna tenki kubwa la maji Igunga lenye uwezo wa kubeba maji lita milioni mbili na laki tano kwa wakati mmoja. Tunawashukuru na kuwapongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata umeme vijiji 30 na sasa tunakwenda kupata umeme vijiji 30 vingine. Jimbo la Igunga tutakuwa na umeme jimbo zima tunawashukuru sana. Pia tumehakikishiwa na tumeendelea kujengewa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (*VETA*) ambacho kwa mara ya kwanza kiwanja chake kilipatikana mwaka 1995. Serikali ya Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli iliyopita wametoa fedha sasa tunajengewa Chuo kikubwa cha Mafunzo ya Ufundi Stadi katika Jimbo la Igunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi Jimbo la Igunga tunamtakia kheri, tupo naye tutamuunga mkono na tutapigana usiku na mchana kuhakikisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIMWELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami niungane na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Spika wa Bunge na wewe mwenyewe kwa sababu Rais aliyetangulia alikuwa sehemu ya Bunge. Pia nitoe pole kwa wakazi wa Chato na Biharamulo kwa ujumla sababu sisi ndiyo wenyeji zaidi pale kwa hiyo, msiba ule ulikuwa nyumbani na nawashukuru wote walioungana nasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kuchangia ninayo mambo mawili ya kumuelezea Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Cha kwanza kila binadamu anapozaliwa ana mambo mawili makubwa katika dunia hii. *Incident* mbili kubwa katika dunia kwa mwanadamu, kwanza ni kuzaliwa na pili kugundua kwa nini umezaliwa. Watu wengi tunaishi hatujui kwa nini tumezaliwa au kwa nini tupo hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kesi ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aligundua *purpose* ya Mungu kumleta duniani. Nakumbuka mwaka 1990 nikiwa mdogo akiwa anagombea Ubunge kwa mara ya kwanza Biharamulo kila alichokuwa anakifanya au *statement* yake kila mmoja alikuwa anamuelezea. Tukiwa wadogo tunaambiwa kuna mtu anaitwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli *that time* yuko Chato mimi niko Biharamulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa Mbunge kwa mara ya kwanza mwaka 1995 nyote ni mashahidi, Naibu Waziri wa Ujenzi kila alichokigusa aliacha alama. Hakuna sehemu Raisi Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amepita

hakuacha alama. Mmemsikia Rais Jakaya Kikwete juzi kwenye suala la ujenzi, ardhi, uvuvi na hata alipomrudisha ujenzi. Hatimaye Watanzania na Chama cha Mapinduzi kikaona na kumuweka kuwa Rais. Alipokuwa Rais alama ile aliyoiweka katika maisha yake kwamba kila anachokabidhiwa kufanya lazima akifanye kwa *hundred percent* haikukoma. Watanzania wote ni mashahidi ujasiri wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kuamua mambo, ujasiri wa katika kuipigania nchi hii haukuanza akiwa Rais umeanza *back-and-forth* na alipokuwa Rais mambo aliyoyafanya ni makubwa mmeyasikia hatuna haja ya kuyarudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo moja kubwa ambalo nilimuuliza Mungu wakati ule napokea taarifa hizi, nikasema *why God*, kwa sababu niliumia sana nikajuliza kwa nini uruhusu hili jambo katika wakati kama huu? Ila nikarudi katika Maandiko Matakatifu nikamkumbuka Musa alivyopigana na wana wa Israel, najua safari ilikuwa ngumu hata safari ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imekuwa ngumu kwa sababu kipindi anaenda hivi kuna wengine walitaka kurudi nyuma na wengi wamekuwa wanapigana kurudi nyuma lakini hakukata tamaa. Nikakumbuka Musa alipopandishwa katika mlima ule na akaoneshwa nchi ya ahadi kule lakini akaambiwa kazi yako imeishia hapa na hautarudi huko na wala hutaiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kuwaambia ni nini? Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliletwa na Mungu kwa ajili ya kazi maalum katika nchi hii, amemaliza kazi ile ambayo Mungu alimleta aifanye, tuendelee kumuomba na kuyaishi yale aliyofanya. Ninachotaka kuwasihia Watanzania na Wabunge wenzangu baba huyu aliletwa kwa *purpose*, akagundua *purpose* iliyomleta hapa, kafanya sehemu yake na amemaliza. Hata sisi sasa tunachotakiwa tumuenzi nacho kila mmoja ajitafakari ajue *purpose* yangu mimi kuwa duniani ni nini na *purpose* ya wananchi walioniamini kunileta Bungeni ni nini. Tukiyajua hayo basi tukaisimamie Ilani ya Chama cha Mapinduzi ili maendeleo haya ambayo Rais wetu alitamani kuyaona

aweze kuyaona yakifanyika na Watanzania waweze kuyapokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuwasihi Watanzania na Waheshimiwa wabunge wenzangu, baba huyu aliletwa kwa *purpose* akagundua *purpose* iliyomleta hapa kafanya sehemu yake amemaliza. Hata sisi, tunachotakiwa tumuenzi nacho, kila mmoja ajitafakari ajue *purpose* yangu mimi kuwa duniani ni nini? *Purpose* ya wananchi walioniamini kunileta Bungeni ni nini? Ili tukiyajua hayo tukaisimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ili maendeleo haya ambayo Rais wetu alitamani kuyaona aweze kuyaona yakifanyika na Watanzania waweze kuyapokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo labda, nirudi kwenye suala mama pia, kumpongeza mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme neno moja tu; watu wote wameongea katika habari ya wanawake, lakini mimi niseme hakupewa nafasi ya Makamu wa Rais kwa sababu ni mwanamke, alipewa nafasi ya Makamu wa Rais kwasababu *ame-demonstrate* na ameonesha uwezo wa kupata nafasi ile.

Kwa hiyo tunaposimama hapa, tusimame hapa tukijua tunaye Rais mwenye uwezo ambaye aliaminiwa na Chama mwaka 2015 kipindi Magufuli anaingia, akiwa hajulikani kama atayafanya haya halikadhalika Mama Samia aliingia akiwa hajulikani kama atayafanya haya. Lakini chini ya uongozi imara, chini ya Ilani ya CCM wakayasimamia wakatufikisha hapa walipotufikisha. (*Makofi*)

Labda neno moja tu la biblia ambalo nataka niliseme kwa ajili ya Mheshimiwa Rais, nikikaribia kukaa, maana najua wote tumeshaongea mengi. Tuki-refer katika Kitabu cha Ezra 10:4 inasema "Inuka maana kazi hii inakuhusu wewe. Na sisi tu pamoja nawe, uwe na moyo mkuu ukaifanye".



Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Wabunge tuko na Rais wetu, Watanzania wako na Rais wetu, ameambiwa ainuke na maandiko hayo tuko pamoja naye, awe na moyo mkuu akaifanye. Tunachotakiwa ni kumuomba ule moyo mkuu ambao umesemwa, uwe juu yake akaifanye. Nina uhakika itafanyika vizuri na tunashukuru Mungu kwa sababu ya Dkt. Philip Mpango ambaye ameteuliwa leo, Mungu awasaidie watufikishe katika nchi ya maziwa na asali ambayo ilikuwa tamanio la Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na niseme ninaunga mkono hoja hizi ambazo zimetolewa hapa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Godwin Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Kitula Mkumbo tunamalizia na Dkt. Mwigulu Lameck Mchemba.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyenijalia afya njema hata siku ya leo nikawa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja zote mbili, kwa maana ya maazimio yote mawili; lakini pili nijielekeze kwenye azimio la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli sisi, ulimwengu wa kimwili tunaona ametangulia mbele za haki lakini bado yu hai. Bado yu hai kwasababu matendo yake, aliyotutendea watanzania yatadumu milele. Na watu wenye vitendo vya namna hii, wenzetu waingereza wanasema *immortality* ni mtu ambaye anaweza kuishi angali amekufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kazi kubwa ambayo mimi naomba nilishauri Bunge letu Tukufu; amefanya mambo makubwa ndani ya nchi yetu lakini kukumbukwa kwake kutakuwa ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda *South Africa* pale Johannesburg, utaona kuna mnara pale lakini pia kuna sanamu nzuri sana ya Mandela, wanapaita Mandela Square. Kwa kazi kubwa aliyoifanya kuhamisha Makao Makuu yetu ya Nchi kuja Dodoma. Hapa Dodoma kuna eneo tengwa la Serikali na lina haki miliki maeneo ya Chimwaga; na Chimwaga tunafahamu kihistoria. Zaidi ya heka 100 zimetengwa pale kwa ajili ya *recreational park*, eneo la mapumziko. Niombe kushauri Serikali, ingefaa tujenge *monument* pale ambayo wajukuu, watoto wetu na kizazi kijacho kitakuwa kikisema Magufuli ni nani? Wanakwenda pale, na hii itatusaidia kumjengea heshima kubwa aliyotutendea Watanzania. Eneo lipo, zaidi ya heka 100 na lina hati ya Serikali na ni mali ya Jiji la Dodoma, kwahiyo hakuna mashaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kuzungumza haya nijikite kwenye eneo hili la Rais tuliyenaye Mama yetu mpendwa Samia Suluhu Hassan. Waingereza wanasema, *all starts well ends well, all starts well ends well*, mama ameanza vizuri, ametuonesha Watanzania kwamba kazi anaiweza. Mfano mzuri leo hii tumeona jina hapa la Makamu wa Rais. Ukitazama unaona matarajio yetu Watanzania, kwamba sasa yale yote yalioachwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yatakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema haya. Ukiangalia makamu wa Rais yeye amekuwa Waziri wa Fedha, lakini haitoshi, ni bigwa na mbobezi wa kukusanya mapato ya nchi haitoshi pia kubana matumizi. Kwahiyo hii *chemistry* ya Mheshimiwa Rais, mama yetu Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Makamu wa Rais ni sawa na *oxygen*; yaani hydrogen mbili ukijumlisha, wale wana kemia ukichukuwa, ukichukuwa *hydrogen* mbili ukijumlisha na *oxygen* moja unapata maji. Kwa hiyo *chemical reaction* hii hatuna mashaka nayo, lazima maji yatapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nisichukue muda mrefu, itoshe tu kusema kwamba aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt.

John Pombe Joseph Magufuli ametubadilishia fikra Watanzania. Kuna watu tulikuwa tunaamini bila rushwa huwezi kupata huduma ya afya, lakini leo hii Watanzania tunaamini utapata huduma ya afya bila rushwa. Kuna watu tulioamini hakuna uwajibikaji ndani ya Taifa hili, lakini leo hii tunaona Taifa letu uwajibikaji umekuwa wa kutukuka na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nisiseme sana lakini itoshe tu kusema nionge mkono maazimio yote mawili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Mchemba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii kuchangia maeneo haya mawili katika maazimio yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze mchango wangu kwenye hiba. Hiba ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hiba ni urithi au waingereza wanasema legacy. Hili naamini wasomi wataandika kwa muda mrefu ujao kwaajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa; mchango ambao Mheshimiwa Rais wetu wa Tano alitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa duniani maisha yetu ni mafupi, na kifo cha Dkt. Magufuli kinatukumbusha kwamba hapa duniani Maisha yetu ni mafupi sana. Muhimu sana kwa kweli ni kwamba, sio kwamba tutakufa au la, kufa tutakufa, lakini tukifa tunapoondoka tutakumbukwa kwa lipi? Mwenzetu kwa kweli ameondoka akiwa ameacha alama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa duniani tunaambiwa kuwa kuna mambo mawili, kuna kutoa na kupokea. Wengi wetu huwa tunapokea, lakini tunapata baraka kwa kutoa,

mwenzetu ametoa, ametoa maisha yake, ametoa kupitia mchango mkubwa wa kazi zake ambazo tutaendelea kuziishi kwa muda mrefu bila kuorodhesha mambo mengi ambayo ameyafanya ambayo watu wengi wameyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, na uteuzi wa leo wa Makamu wa Rais ni jibu na ujumbe kwamba kazi inaendelea. Hilo ndilo jibu ambalo tunapewa kwamba, ni *stability and continuity*. Kwamba kitabu kinaendelea kuandikwa tunaendelea kwenye ukurasa mwingine. Tunashukuru sana kwa uteuzi ambao Mheshimiwa Rais ameufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kifo hiki kinatukumbusha miaka 20 iliyopita. Tarehe 4 Julai, 2001 nchi yetu ilikumbwa pia na msiba wa Makamu wa Rais Dkt. Omari Ali Juma. Mheshimiwa Mkapa alipomteua Dkt. Ali Mohamed Shein alitoa sababu kwa nini amemteua. Alitoa sababu sita ambazo kwa kweli ukizirejea, ndizo unazoziona leo kwa viongozi wetu wawili wakuu; kwa maana ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, lakini hata uteuzi wa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa ruhusa yako naomba nizirejee hizo sifa sita ambazo zilimuongoza Mheshimiwa Mkapa kumteua Mheshimiwa Ali Mohamed Shein. Yeye alisema kwamba, Watanzania wanatarajia sifa zifuatazo kutoka kwa viongozi wao; na ameandika pia kwenye kitabu chake kwamba ndivyo kigezo cha viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa ya kwanza ni utu na uadilifu. Yamesemwa hapa kuhusu utu na uadilifu wa Mama Samia lakini pia wa Mheshimiwa Dkt. Mpango. Upendo na heshima kwa watu wote. Kupenda kazi na kutumikia wananchi badala ya kupenda kutumikiwa na kukuzwa. Watu wengi wenye vyeo tuna shida moja. Ukiwa na cheo kuna mawili, unataka watu wakikuona wakuone nini? Wakimuona Kitila wamuone Kitila kwanza Waziri baadaye, ama Waziri kwanza Kitila baadaye? Watu wengi wanataka waonwe kwanza kwa vyeo vyao, halafu baadaye wao. Hapa Mheshimiwa Mkapa anasema, kiongozi mzuri ni yule ambaye

anataka kwanza kabla ya cheo chake watu wamuone yeye, na hii ni sifa ya msingi ambayo viongozi wetu wawili wanayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naiweka vile vile namba nne, kuweka mbele maslahi ya taifa na Watanzania badala ya maslahi binafsi, viongozi wetu tunawafahamu vizuri. Unyenyekevu, limezungumzwa sana hili, viongozi wetu wawili Mheshimiwa Rais tangu aanze kazi hii; na watu wanaomfahamu kabla tuliopata nafasi na bahati ya kufanya naye kazi kabla tunafahamu unyenyekevu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho ni kuzingatia misingi ya Taifa; na alitaja misingi tisa; utu, haki, usawa, fursa sawa, amani, umoja, upendo, mshikamano na hii ya mwisho aliandika kwa herufi kubwa MUUNGANO. Kiongozi yeyote katika nchi hii lazima tukimuona, tukimuangalia, tukimsikia tuwe na hakika kwamba Muungano wetu upo salama. Hakuna shaka kwamba kwa viongozi wetu wawili hawa Muungano wetu upo salama sana. Na hilo ni jambo la misingi mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni ukuu wa Katiba yetu. Watu wamelizungumza hili na limezungumzwa sana lakini sidhani ni kwa uzito ambao tunapaswa kuuona. Marekani wameshafiwa na Marais nane, wakiwa madarakani tangu mwaka 1841 na juzi 1993; na muda wote walikuwa na changamoto ya namna ya kumuapisha Makamu wa Rais, wamehangaika wameweza kufanikiwa kufanya mabadiliko 25 mwaka 1967. Sisi walioandika Katiba Mungu awabariki. Katiba yetu ina ukuu wa pekee, tumepita katika kipindi kigumu wala tusijue kwasababu Katiba yetu na misingi ipo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamtakia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais na viongozi wote neema na baraka na mafanikio tele katika uongozi wao. Mungu awabariki sana. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, watoa hoja wajiandae.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia mjadala huu. La kwanza, nitoe pole kwa Watanzania wote kwa msiba huu uliotupata; na nikiri kwamba naunga mkono hoja iliyotolewa na watoa hoja, na kwa kweli wamefafanua kwa kirefu na kwa kina na wameutendea haki mjadala wenyewe huu tunaoujadili, ambao utakaa kwenye kumbukumbu zetu rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza hapo hapo; katika jambo hili lililotokea nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania. Watanzania wametendea haki uhuru wa nchi yetu, wameipa heshima nchi yetu kwa namna walivyomsindikiza kiongozi wetu, kwa namna walivyomuaga kiongozi wetu. Ni kiongozi aliyesimamia waziwazi uhuru wa nchi yetu, ni kiongozi aliyesimamia waziwazi maslahi ya Watanzania, ni kiongozi aliyesimamia waziwazi na aliyeyatoa maisha yake kwa ajili ya Watanzania. Heshima aliyopewa wakati wanamuaga katika maeneo alikopelekwa; mimi niliendelea kupata hata *message* maeneo mengine wakisema tunatamani na majiji mengine apite, tunatamani na huku apite; ni basi tu kwa ratiba ilivyokuwa tukafanya kwa uwakilishi. Ile ilikuwa heshima inayolinda na inayotambulisha uhuru wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na wakati anachaguliwa Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Makamu wake, watanzania walipiga kura kwa siri. Zile zilikuwa kura za siri na asilimia ilizopatikana ile ilipatikana kwa kura za siri. Lakini namna walivomsindikiza wameitangazia dunia kwamba kwa kura ya wazi walikuwa wanamaanisha nini wakati wanapiga kura wakati wa Uchaguzi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu neno la faraja kwa Watanzania, kwamba hili limeshatokea. Niwape neno la Faraja; wakati tunaingia kwenye uchaguzi mwaka 2015, Ilani ya Uchaguzi ambayo imetupa matokeo makubwa haya, ambayo ndiyo ilikuwa ahadi kwa Watanzania wabeba maono, kwenye Ilani alikuwa Dkt. Magufuli na Mama Samia Suluhu. Kwahiyo hakuna namna mafanikio yale tuliyoapata kutoka 2015 - 2020 ukayaongelea bila kumtaja Mama Samia

Suluhu. Ameshiriki kikamilifu na yeye ni sehemu ya mafanikio yale. Na katika mafanikio yale wakiwa wao wabeba maono msimamizi wa maono yale, msimamizi wa kazi alikuwa Waziri Mkuu ambaye yupo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo mmoja wa mbeba maono yupo, msimamizi wa mbeba maono yupo lakini wakati mbeba maono na msimamizi wa wapo, pia mbeba kikapu yule aliyekuwa anawezesha yale maono yatekelezwe Dkt. Mpango naye yupo. Kwa maana hiyo hatuna haja ya kuwa na hofu kwa sababu seti hiyo bado imekamilika, ambayo imetupa mafanikio makubwa haya ambayo tumeweza kuyasimulia leo hii. Tunachotakiwa ni kuendelea kwa wale ambao ni mihimili, Bunge na Mahakama kutoa ushirikiano. Kwetu sisi ambao ni wasaidizi wa Serikalini tumepokea maelekeo na tunasimama kuendelea kupokea maelekezo kama ambavyo tumekuwa tukifanya na kuyasimamia ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata katika utekelezaji, kinachomfanya kiongozi aweze kusimama na kutekeleza wala si jinsia yake, kinachomfanya kiongozi akemee rushwa wala si jinsia yake, ni uadilifu wake; hata mwanaume akiwa mla rushwa hawezi kukemea rushwa; ni uadilifu wake. Sasa fuatilieni historia ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa sasa hivi, hana record yoyote ya kukosa uadilifu, ni muadilifu ambaye anaweza kwa namna yoyote bila uoga kukemea rushwa mahali popote pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiangalia ni mchapa kazi ambaye hapendi kazi ilale. Sisi ambao tumekuwa tukipokea maelekezo tangu muda wote ule tuna uhakika na haya tunayowaelezea. Hata juzi aliposema pale kwetu sisi tayari tumeshapokea yale ni maelekezo. Amesema atasimama imara kwenye mapato na matumizi na masuala ya rushwa. Sisi wasaidizi wake tayari tumeshapigia mstari, na mimi nilishawaelekeza wasaidizi wangu kuendelea kutafasiri yale waendeleo kuyafatilia ili yale ambayo yataenda kinyume na maelekezo yake yaweze kuchukuliwa hatua. Maana yake hapo tayari ni *zero tolerance of corruption no*

*nonsense on public offices and public funds pamoja na kusimamia haki za watu.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa mwanamke katika jamii yoyote, mwanamke ni baraka, mwanamke ni kibali. Tanzania inaenda kupata kibali. Na hata ukienda tu kwenye mifano hata ya kawaida, kwasababu nimeshaona kengele imegongwa, hata kwenye mifano ya Maisha ya kawaida tu, yaani hata simba tu tangia wapate CO mwanamke mambo yao yamewanyookea kweli kweli siku hizi hawang'oi hata viti. Maana yake wanabaraka katika nafasi yao na wanafanya vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona niweke na hili kwa sababu tunaomboleza, watu wasitoke bado wananyong'onyea nyong'onyea ili tuendeleo kuwatia moyo wananchi wetu na Taifa letu liweze kusonga mbele. Naunga mkono hoja na watoa hoja wameielezea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga uhitimisha hoja yako.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nihitimisha hoja ya kutambua na kuenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuanza kusema, hakika kwake mola tumetoka na kwake ni marejeo, Bwana ametoa Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe. Watanzania tumepata pigo tumelia na uchungu kutokana na mapenzi makubwa tuliyokuwa nayo kwa jemedari wetu aliyetangulia mbele ya haki, iliyobaki ni kumuomba dua ili Mwenyezi Mungu ampumzishe salama huko aliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa vile lisilobudi kutendwa naomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tuendeleo na maisha yetu ambayo Mwenyezi Mungu ameturuzuku sisi ambao tuko hapa duniani.



Mheshimiwa Naibu Spika, kutambua na kuenzi mchango wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuongea tu, haitosaidia kitu chochote.

kutambua na kuenzi mchango wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuongea tu haitosaidia chochote. Hivyo basi, niungane na wote waliounga mkono azimio hili kwa lengo la kuendeleza na kudumisha yale yote ambayo tumeyatambua na kukusudia kuyaenzi. Endapo tutafuata njia aliyotuonesha Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli nina imani tutakuwa tumeenzi mchango wake kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Rais wetu, Samia Suluhu Hassan na Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, kuwa azimio hili litaweza kutekelezeka chini ya uongozi wao mahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na uwezo wa kumudu majukumu yao katika Taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Najma, toa hoja ili niweze kuwahoji Wabunge.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na Wabunge wengi. Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji kuhusu Azimio la Kuutambua na Kuenzi Mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa Utumishi wake uliotukuka.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuutambua na Kuenzi Mchango wa aliyekuwa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa utumishi wake uliotukuka lilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda na hakuna waliosema siyo, kwa hiyo azimio hili limepita kwa asilimia mia moja.

Nitalizungumzia baadaye kidogo; nimuite sasa Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama ahitimishe hoja yake pia.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuhitimisha Hoja ya Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Wabunge 23 walipata nafasi ya kuzungumza. lingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kwamba hoja hii ni moja katika hoja chache sana ambazo ndani ya Bunge lako zimepata kibali toka pande zote za Wabunge bila kuyumba. Sababu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wanaamini kwamba mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, hayawezi kutenganishwa kamwe na mafanikio ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambaye alihudumu kama Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo moja limezungumzwa kwa namna ambayo linahitaji kidogo tulifafanue; hoja ya demokrasia na uhuru wa Habari. Kwamba Mheshimiwa Khatib na baadhi ya Wabunge humu ndani kuweza kuhama kutoka kwenye Chama cha CUF na kwenda ACT Wazalendo na kuweza kushiriki katika Uchaguzi na kushinda na kuzungumza ndani ya Bunge hili ni demokrasia ya kiwango cha juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia huanzia ndani ya vyama. Kitendo cha Chama Cha Mapinduzi kuendelea na utaratibu wa kubadilisha wenyeviti wao kila miaka kumi ni kielelezo cha kutosha cha ukomavu wa demokrasia ndani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri vyama vingine vifuate utaratibu huo kwa sababu huwezi kuwa na *legitimacy* ya kupigania demokrasia nje kama hujaimarisha demokrasia ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tafsiri sahihi ya demokrasia; na hapa namnukuu Balozi Dkt. Wilbrod Slaa; demokrasia ya kweli ni demokrasia ya kuwasikiliza na kuwahudumia watu wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Tano alifanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa akishirikiana na Rais wetu wa sasa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Kote walikopita Watanzania wamelilia elimu, maji, huduma za afya, mahitaji ya mitaji kwenye biashara na yale yote yaliyowekwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na hayo yote ndiyo yaliyobebwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji kuhusu hoja ya Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kumpungeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lllipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki kwa hiyo azimio pia limepita kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo tulikuwa na kazi ya kujadili kuhusu maazimio mawili ambayo yote yamepita hapa kwa asilimia mia moja na nadhani ni utaratibu ambao umeanza vizuri leo asubuhi kwa kumpitisha Makamu wa Rais kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mmetoa michango mingi ambayo imeashiria namna ambavyo kama nchi tuko tayari kusonga mbele, lakini katika kusonga kwetu mbele ni pamoja na kutambua kule tulikotoka.

Nizungumze machache kuhusu haya maazimio ambayo tumeyapitisha siku ya leo. Ni dhahiri kutokana na michango yenu Waheshimiwa Wabunge na mengine, kwa sababu wote hapa tunawawakilisha wananchi, mengine ni wananchi walikuwa wanasema huko kwenye maeneo yetu ya uwakilishi na wengine wakati wakitoa salamu zao wameonesha wazi kabisa kwamba kwa niaba ya kundi hili, kwa niaba ya jimbo hili.

Naamini ni kwa sababu ya muda, Wabunge wote wangetamani kupata fursa ya kuzungumza kuhusu Mheshimiwa Rais wetu wa sasa, mama yetu Samia Suluhu Hassan, lakini kwa sababu ya muda hatujapata kuwasikia. Pia wako ambao wangependa kuzungumza kuhusu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli lakini hawajapata fursa. Naamini hawa waliozungumza wametuwakilisha sisi sote na tuamini kwamba salamu zao hizo basi zinatuwakilisha sisi sote. *(Makofi)*

Katika hayo machache ninayotaka kuzungumza, ni dhahiri, hakuna siku ambayo sisi kama Taifa na leo katika michango yenu humu mmedhihirisha ambayo tungekuwa

tayari kwa siku hiyo kwamba sasa Mungu unaweza kumchukua Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; hiyo siku isingekuwepo. Kama michango yenu mingi ilivyoashiria, ni dhahiri huu ndiyo uliokuwa wakati wake sahihi wa kwenda. Kwa namna yoyote ile utakavyoiweka, huu ndiyo ulikuwa wakati wake sahihi kwa sababu watu hapa wamesoma mistari mingi kutoka kwenye vitabu vyetu vya dini, lakini ni dhahiri maisha ya mwanadamu si marefu kama ambavyo tungependu. Wakati mwingine yakiwa marefu vile tunavyopenda pengine hatutatenda yale ambayo Mungu aliyakusudia katika maisha yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo, kwa kuwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikuwa mwanadamu kama wanadamu wengine, hakuwa malaika, hata kama mambo aliyoyatenda ni makubwa sana na yote yameelezwa hapa, lakini ni dhahiri alikuwa mwanadamu. Pamoja na uanadamu wake, sisi wote kwa yale yaliyozungumzwa hapa ni wazi tunakubaliana kabisa na andiko lililo katika kitabu cha Timotheo wa Pili, mlango wa nne, mstari wa saba.

Kama Dkt. Magufuli angekuwa na fursa ya kuzungumza, ya kutuaga Watanzania, naamini angesema hivi; nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda. (*Makofi*)

Watu wamezungumza namna alivyokuwa akimcha Mungu, watu wamezungumza namna ambavyo ameipigania nchi hii; hiyo ilikuwa ni vita yake na yeye ameipiga vilivyo na hatua zake zilezile chache amekwenda sawasawa, na imani yake ameilinda.

Wamezungumza watu hapa kuhusu kutakuwa na kubeza hapa na pale; hayaepukiki kwa sababu yeye alikuwa ni mwanadamu, hakuwa malaika. Kama Mungu mbele zake wapo malaika walioasi, pamoja na sisi kumtazama Mungu wetu kama siyo mtu, ni Mungu. Kwa hiyo yuko juu sana, huwezi hata kukosoa jambo lolote kuhusu Mungu, lakini wapo

malaika huko waliona kuna jambo haliko sawasawa, sembuse kwa mwanadamu.

Kwa hiyo Watanzania tujipe moyo katika mambo makubwa ambayo tunao ushahidi nayo kuhusu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Na tujitie moyo katika hayo, kwamba yeye kazi yake aliyokuwa amepewa hapa duniani ameimaliza salama. Kwa kazi hiyo aliyokuwa ameipewa wakati yuko hapa duniani hakuifanya peke yake, alikuwa na mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambao walifanya kazi kwa karibu sana, kama Katiba yetu inavyosema, yeye ndiye aliyekuwa msaidizi mkuu wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kwa namna hiyo, ule Urais, anapoitwa Makamu wa Rais maana yake lile neno Rais liko pale; yeye ndiye Rais Rais anapokuwa hayupo. Na sisi wote ni dhahiri nchi yetu inakwenda vizuri na sasa mama yetu ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Sasa safari yake ya kuwa Rais ni dhahiri Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mchango wake ni mkubwa, kwa nini, kwa sababu aliheshimu wanawake. Tunapomtaja Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan na sifa zake zote za kustahili kuwa Makamu wa Rais lakini ni dhahiri wako wengi pengine walikuwa na hizo sifa, lakini Dkt. John Pombe Magufuli akasema nitakwenda huyu mama na huyu mama ndiye Rais sasa, ndiye anayetuongoza. *(Makofi)*

Sasa huyu mama anayetuongoza mmeeleza mambo mengi wakati wa kumpongeza hapa ndani. Naamini kwa sababu wakati wote yeye kama Makamu wa Rais alifanya kazi kwa karibu sana na Rais kama msaidizi wake, lakini pia ndiye aliyekwenda kuinadi Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika maeneo mengi zaidi kuliko Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa sababu yeye alikwenda kwenye majimbo mengi kuliko Rais wetu. Rais wetu yako maeneo mengi pia alipita lakini Mheshimiwa Samia alikwenda kwenye maeneo mengi.

Watanzania tujitie moyo. Ilani iliyopita ya 2015 - 2020, yale tunayoyasema yaliyotekelezwa Mheshimiwa Samia

alikuwa sehemu ya hayo. Hata hii ambayo imeanza 2020 kuelekea 2025 ni dhahiri tutaona utekelezaji kama ule ambao tuliuzoea na kuzidi maana huyu sasa aliyeko madarakani ni mama, kwa hiyo siyo Rais wa kawaida. *(Makofi)*

Kwa kusema hayo ndugu zangu muda wetu umekwenda sana, lakini mniruhusu, kwa sababu niko katika kuwatia moyo Watanzania, niwasomee maneno kidogo tu ambayo yanaashiria safari yetu ni njema na leo tumempata Makamu wa Rais ambaye sote kwa nia moja, kwa lugha moja tumemuunga mkono Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwamba chaguo ulilolileta tunakuunga mkono, sisi kama Wabunge na wawakilishi wa wananchi tumeahidi leo kwamba tumemuunga mkono mama kwa kumpa asilimia mia moja za yule msaidizi aliyemleta hapa. *(Makofi)*

Ni dhahiri sisi kama wawakilishi wa wananchi tuko tayari kumuunga mkono mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuelekea kule ambako anatupeleka yeye pamoja na Dkt. Mpango.

Ndugu zangu, safari huwa ni ndefu na kuna kufika, kuna kuishia njiani, lakini safari hii Watanzania tutafika salama. Sasa tutafika salama kwa maneno haya ambayo nataka niyasoma kwenu muda huu.

Maneno haya ambayo Musa alikuwa ameshamuandaa Joshua kwa ajili ya safari. Kama ambavyo sisi wote ni mashahidi, mama yetu ambaye ni Rais sasa aliandaliwa. Kwa sababu unapomfanya mtu kuwa Makamu wa Rais maana yake uko tayari awe Rais wakati wowote. *(Makofi)*

Katika maandalizi yale ambayo yamefanywa maneno haya tukiyasema, ambayo Mungu alimwambia Joshua ndiyo ambayo kwa michango yenu Waheshimiwa Wabunge na sisi tunatamani tumwambie mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Joshua moja mstari wa tano mpaka wa saba, halafu nitasoma wa tisa.

“Hakuna mtu yeyote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja nawe; sitakupungukia wala sitakuacha.

Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa.

Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda kulingana na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiache, kwenda mkono wa kulia, au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako.

Mstari wa tisa; Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.” *(Makofi)*

Haya maneno ndiyo ambayo kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge wanatamani wamwambie mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwamba safari hii tutafika salama kwa sababu mama yetu uliandaliwa vizuri kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa utumishi huo ambao walifanya kazi kwa pamoja, mama Samia Suluhu Hassan na sasa mama anaanza safari, yeye pamoja na Dkt. Mpango watakwenda vizuri. Tanzania ipo salama, ipo katika mikono salama, tutavuka salama, tutafika salama kule tunakotaka kwenda. Hatuna haja ya kuwa na shaka yoyote.

Ndugu zangu, katika mambo yote haya tujifunze mambo mawili; moja, kama viongozi, lakini pia kama wananchi, ni vizuri sana kuheshimiana kwa sababu hatuifahamu kesho yetu. Pengine wako watu walikuwa wanamtazama Makamu wa Rais kama ataendelea kuwa makamu hivi, sasa ameshakuwa Rais, ni funzo kwetu sote kuheshimu kila mtu umwonaye kwa sababu huifahamu kesho yako. *(Makofi)*



Pia kwa kile kilichotokea leo asubuhi hapa kwa mwenzetu, ama tuseme aliyekuwa mwenzetu, Mheshimiwa Dkt. Mpango, sasa alikuwa Waziri na humu ndani tulikuwa tunazungumza kwa namna fulani hivi, sasa ameshakuwa Makamu wa Rais. Tuheshimiane kwa sababu hatujui kesho yetu. *(Makofi)*

Jambo la pili na la mwisho ni kwamba, wanadamu hatutadumu milele. Ni vizuri kujitahidi kuufanya utumishi wako wakati huu, usisubiri kesho maana kesho si yako; na sisi wote humu ndani ni watumishi wa wale waliotuchagua, tujitahidi kuwapa utumishi uliotukuka ili na sisi yumkini tuwe tumejifunza kwa maisha haya mafupi ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Baada ya kumaliza hayo Waheshimiwa Wabunge, namtakia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa niaba yenu nyote tunamtakia utumishi mwema na tunamuahidi sisi kama Bunge, sisi kama wananchi, vijana wa nchi hii, wanawake wa nchi hii, wanaume wa nchi hii, watoto wa nchi hii kumuunga mkono kama ambavyo tulikuwa tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyepita.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.58 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 31 Machi, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*